

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA MBILI

Kikao cha Arobaini na Nne – Tarehe 13 Agosti, 2008

(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaanza shughuli nilikuwa napenda tutambue hata kwa kipindi hiki cha Maswali kuwepo kwa Mheshimiwa Jaji Mkuu wa Mahakama ya Rufaa Tanzania, akiwa ni mgeni mashuhuri ambaye tuliyeh naye hapa. Karibu sana Mheshimiwa Jaji Mkuu, tunafarijika sana kuwepo kwako hapa ndani. Amefuatana na Waheshimiwa Majaji saba, baadaye nadhani saa 4.00 tutawezeku watambua vizuri. (*Makofi*).

Tunaendelea, Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria.

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:-

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009.

MHE. RAMADHANI A. MANENO (k.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA):-

Taarifa ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu utekelezaji wa Wizara ya Katiba na Sheria, kwa Mwaka wa Fedha uliopita pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009.

MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:-

Taarifa ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuhusu utekelezaji wa Wizara ya Katiba na Sheria, kwa Mwaka wa Fedha uliopita, pamoja na maoni ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009.

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, swali la kwanza kwa siku ya leo linaelekezwa Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika na linaulizwa na Mheshimiwa Fuya Godwin Kimbita, Mbunge wa Hai. Hayupo kwa hiyo tunaendelea, swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Mtutura, Abdala Mtutura, Mbunge wa Tunduru.

Na. 383

Wilaya ya Tunduru Kuzalisha Zao la Pamba

MHE. MTUTURA A. MTUTURA aliuliza:-

Kwa kuwa, mazingira ya kijiografia na hali ya hewa ya Wilaya ya Tunduru yanafanana na yale ya mikoa ya Shinyanga na Mwanza ambayo ni maarufu kwa uzalishaji wa zao la pamba; na kwa kuwa, kuna dalili nyingi zinazoonesha Wilaya ya Tunduru kuweza kuzalisha pamba nyingi kwa hekta kuliko ilivyo mikoa ya kanda ya ziwa:-

- (a) Je, ni kweli Serikali imeweka pingamizi kwa wananchi wa wilaya za mpakani mwa Tanzania na Msumbiji kuzalisha pamba?
- (b) Kama ndivyo. Je, ni sababu zipi za msingi zilizoilazimisha Serikali kuchukua hatua hiyo?
- (c) Je, ni mambo gani yakitimia Serikali itatoa ruksa kwa wananchi wa Tunduru kulima zao hilo?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura, Mbunge wa Tunduru, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kilimo cha pamba katika mikoa ya Kusini ikiwa ni pamoja na mikoa ya Ruvuma, Mtwara, Lindi na baadhi ya maeneo ya mkoa wa Mbeya, kilizuiliwa tangu mwaka 1946 kuititia gazeti la Serikali namba 265 la mwaka 1946 baada ya mdudu anayejulikana kwa jina la funza mwekundu kuonekana katika mashamba ya pamba ya majaribio na mimea ya pamba pori katika vichaka.

Aidha, utafiti uliofanyika kuanzia mwaka 2004/2005 umethibitisha kuwepo kwa mdudu huyo katika mikoa hiyo ya Rukwa na Mbeya hadi sasa. Baadhi ya vijiji vilivyoonekana mdudu huyo ni pamoja na Mbala, kanga, Magamba, Galula na

Chang'ombe katika Wilaya ya Chunya na kijiji cha Wanyala katika Wilaya ya Mbozi, Ikumbi katika Wilaya ya Mbeya, vijiji vya Ruweje na Mpiluka katika wilaya ya Nachingwea. Kijiji cha Nyamihungo katika wilaya ya Masasi, kijiji cha mtopwa katika wilaya ya Newala, Kibutuka katika wilaya ya Liwale, vijiji vya Chikomo na Ligoma katika wilaya ya Tunduru, Muze katika wilaya ya Sumbawanga na Kasansa katika wilaya ya Mpanda ambayo ipo nje ya eneo la karantini.

(b) Mheshimiwa Spika, sababu za msingi za kuweka karantini hiyo ni kumzuwia mdudu huyu asisambae katika maeneo mengine yanayolima pamba ili kulinda uzalishaji na tija ya pamba nchini kutokana na athari zinazoletwa na mdudu huyu katika zao hili la pamba. Mdudu huyu ambaye ameshaanza kuonekana nje ya eneo la karantini ana uwezo wa kuzaliana kwa wingi katika kipindi kifupi na kusababisha uharibifu mkubwa kwa kushambulia matunda ya pamba na kusababisha hasara kubwa. Tabia ya mdudu huyu kula akiwa amejificha ndani ya tunda la pamba, hufanya udhibiti wake kuwa mgumu na wa gharama kubwa. Taarifa ya kitaalamu ya mchanganuo wa gharama hizo itakamilika mwaka huu wa 2008/2009.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali itaruhusu kilimo cha pamba wilayani Tunduru na sehemu nyingine za mikoa ya Kusini pale itakapodhihirika kwamba mdudu huyu hayupo tena katika maeneo ya Kusini mwa nchi yetu.

Aidha, tathmini ya kiuchumi inafanyika ili kuona ni gharama kiasi gani mkulima atalipa kupambana na mdudu huyu iwapo ataruhusiwa kulima pamba na kama kilimo hicho kitakuwa cha maslahi kwa wakulima wa maeneo hayo.

MHE. MTUTURA A. MTUTURA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nalazimika kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri, amekiri kwamba karantini hii iliwekwa toka mwaka 1946, sasahivi ni takribani miaka 47 toka tupate uhuru. Serikali yetu ilichukua hatua zifi toka baada ya kupata uhuru hadi matokeo ya utafiti yapatikane mwaka huu au mwakani? Je, Serikali itakubaliana na mimi kwamba kwa kiasi kikubwa haikuwa makini katika kuhakikisha kwamba inafanya utafiti wa kutosha ili kumuangamiza mdudu huyu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mtutura, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nilisema kwamba Serikali wakati wote iko makini katika kutekeleza mambo yake.

Mheshimiwa Spika, la pili ni kama nilivyosema utafiti huu umeanza mwaka 2004/2005 na wamegundua kwamba mdudu huyu bado yupo. Na kwa kuwa mdudu huyu yupo na amegundulika kwamba bado anaendelea kusambaa na kama ilivykuwa

imeelezwa mwaka 2004/2005 mdudu huyu alikuwa hajafika Mpanda, sasahivi mdudu huyu amefika Mpanda ambako alikuwa hayupo. Kwahiyo sasa kinachofanyika sio kwamba tunazuwia watu wa Kusini wasilime pamba lakini kinachofanyika ni lazima tuangalie pia usalama wa zao hili la pamba katika nchi yetu hii. Kinachofanyika sasahivi ni kufanya tathmini ili tuweze kujuwa kwamba mkulima akiruhusiwa kulima pamba ataingia hasara kiasi gani. Sasahivi kuna vijiji vinne nya wilaya ya Chunya, wanafanya majoribio ili kuona watatumia gharama kiasi gani.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa mdudu huyu yuko Msumbiji na Malawi, lakini kiasi cha dawa wanachotumia, wanapiliza mara name wakati sisi hapa mikoa ya Mwanza na Shinyanga wanapuliza mara nne na wengine hawapulizi kabisa.

Sasa wale wanatumia gharama kubwa katika kumdhhibit mdudu huyu na bado wanatafuta njia ya kumtokomeza kabisa lakini imeshindikana. Sasa hatutaki tukaingiza nchi kwenye matatizo, ni lazima tufuate ushauri wa wataalamu ili tuweze kulinda mazao yetu makuu. (*Makofi*).

SPIKA: Kwa bahati njema Mheshimiwa Kimbita, amewasili humu ndani ya ukumbi namwona. Kwa hiyo, namruhusu aulize swali lake sasa.

MHE. FUYA G. KIMBITA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Naomba sasa swali langu namba 382 lijibiwe.

SPIKA: Nilikutazamia uombe radhi kwa kucheleta, lakini wewe unaichukua huruma ya Spika kuwa ni *given, ipo tu*. (*Kicheko/Makofi*).

MHE. FUYA G. KIMBITA: Mheshimiwa Spika, samahani ni Kanuni tu.

Na. 382

Mikakati ya Kuongeza Uzalishaji wa Zao la Kahawa

MHE. FUYA G. KIMBITA aliuliza:-

Kwa kuwa ni nia ya Serikali ifikapo mwaka 2010 nchi iweze kuzalisha si chini ya tani 120,000 za kahawa kwa mwaka:-

- (a) Je, ni mikakati gani inayoendelea ya kuongeza miche bora ya kahawa?
- (b) Je, ni mikakati gani iliyopo ya kuongeza wataalam wa kilimo? (*Extension Officers*).
- (c) Je, Serikali imeweka mikakati gani kushawishi uanzishwaji wa *Central Pulpuries*?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika napenda nijibu swali la Mheshimiwa Fuya G. Kimbita, Mbunge wa Hai, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Serikali imejiwekea lengo la kufikia uzalishaji wa tani 120,000 za kahawa kwa mwaka ifikapo mwaka 2010. Ili kutimiza azma hii Serikali ina mikakati ifuatayo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Kahawa, *TaRI*, Serikali imeweeka mkakati wa kuzalisha miche bora ya kahawa inayokinzana na magonjwa ya chule buni na kutu ya majani kwa kutumia vikonyo vya miti bora ya kahawa.

Kama sehemu ya utekelezaji wa mkakati huo, katika mwaka 2007/2008 jumla ya miche 4,980,000 ilizalishwa sawa na 99.7% ya lengo la kuzalisha miche bora 5,000,000. Miche hiyo inatosheleza hekta 6,123 za mashamba ya kahawa. Serikali pia katika mwaka wa 2007/2008 iliipatia *TaCRI* 500,000,000/= kwa ajili ya kazi hiyo. Ktika mwaka 2008/2009 lengo ni kuzalisha miche 10,000,000.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa utaalamu katika kuboresha na kuendeleza mazao ikiwa ni pamoja na zao la kahawa na ili kuendana na lengo kuu la kuwa na kilimo cha kisasa ifikapo mwaka 2025, mwaka 2007/2008 Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ilianza kutekeleza mpango wa kuimarisha huduma za ugani nchini. Lengo ni kuajiri wataalamu wapya 11,703 ili kufikia wataalamu 15,000 ifikapo mwaka 2010/2011 ili kukidhi mahitaji ya kuwa na mtaalam mmoja kwa kila kijiji, Kata na Tarafa.

(c) Mheshimiwa Spika, kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya, Vyama vya U shirika na wawekezaji wengine ndani ya sekta ndogo ya kahawa, Serikali kupitia *ASDP* imewezesha na kuhamasisha uwekezaji katika kuanzisha *central pulperies*. Katika kutekeleza kazi hii mchango mkubwa umetokana na uwekezaji binafsi na Halmashauri za wilaya kwa kutumia mipango shirikishi ya *DADPs*, ambapo hadi sasa kuna mitambo 76 yenye uwezo wa kuzalisha jumla ya tani 1,250 za kahawa bora kwa mwaka ikilinganishwa na mitambo 55 iliyokuwapo mwaka 2000.

MHE. FUYA G. KIMBITA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi hii pia nitumie nafasi hii niombe radhi.

Mheshimiwa Spika, naomba niulize maswasli mawili ya nyongeza. La kwanza, kwa kuwa bado katika mashamba yetu na sehemu nyingine mbali na kule wilayani Hai, bado kuna mibuni ya zamani ambayo inahitaji kutumia madawa mengi na haya madawa ni ghali sana. Je, Serikali haiwezi kutoa ruzuku katika haya madawa ili kuendeleza hili zao la kahawa katika ile mibuni michache iliyobakia pamoja na azma ya Serikali kuotesha mibuni mipyä?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Kwa kuwa huu uendelezaji wa miche mipyä ya kahawa kwa kiwango kikubwa ni fedha za wahisani, isingekuwa ni bora zaidi kuanzisha mfuko maalum ambao hili zoezi litakuwa ni endelevu hata baada ya hawa wahisani kujitoa?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Kimbita, Mbunge wa Hai, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nikiri kwamba Serikali ingependa itoe mahitaji yote ambayo mkulima anayahitaji ikiwemo pembejeo za madawa, mbolea, na miche. Lakini kutokana na ufinyu wa Bajeti kahawa tumeipa ruzuku ya miche, chai tumeipa ruzuku ya miche, pamba tunaipa ruzuku ya madawa, korosho tunaipa ruzuku ya madawa na maeneo ya tumbaku yanapewa ruzuku ya mbolea.

Mheshimiwa Spika, sasa miche hii ambayo inazalishwa kwa sasa hivi ndio ambayo tunaitolea 500,000,000/= sasa katika suala la kuendeleza kuwa na miche mingi zaidi pia *TACRI* ambayo tumetoa hiyo 500,000,000/= mwaka huu tunatoa 600,000,000/=.

Lakini *TACRI* pia ina *Extension Officers* ambao wanakwenda kule kuwafundisha watu katika vijiji na katika mashamba yao kwenye Kata na katika vituo vile sita vya kudumisha zao hili la pamba ili waweze kuzalisha miche mingi zaidi kwa kutumia vikonyo na kutumia vipandikizi.

Mheshimiwa Spika, pili. Suala la mfuko maalum ni suala ambalo linaongeleka. Tunaweza tukaliongea baada ya kuwasiliana na Mheshimiwa Mbunge, kwamba yeye ana mawazo gani zaidi ili tudumishe kile ambacho tunacho.

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Hapo miaka ya nyuma kidogo wakulima wanaolima zao la minazi waliletewa miche ambayo ilisemekana ni miche bora lakini walipolima haikuchukua muda mrefu sana. Ilizalisha sana lakini baada ya miaka michache ikafa. (*Makofi*)

Sasa wakulima wa zao la kahawa, na kwasababu kwangu tunalima sana kahawa, wana wasiwasí na hii miche ya kuzalisha yaani vikonyo vya miche ambayo inapandikizwa, wana wasiwasí hayo sana. Inazalisha sana lakini uhakika wake hatunao, tuna wasiwasí kwamba inawezekana ikarejea ileile ambayo iliwapata wakulima wa zao la minazi. Je, Waziri atawahakikishia wakulima wa kahawa kwamba miche hiyo ni bora na haitakuwa na mabadiliko au athari zozote hapo baadaye?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika napenda kujibu swali la Mheshimiwa Zambi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Zambi na wakulima wetu nchini kwamba miche hii imejaribiwa tangu mwaka 1984. Mwaka 1984 mpaka leo nadhani ni miaka 25, kama sikosei na sasahivi bado inazalisha vizuri. Kwa hiyo, nikuhakikishie Mheshimiwa na wananchi wanaoniskiliza kwamba miche hii ya kahawa ni bora na imeshachunguzwa kwa muda mrefu kabisa, itakuwa inazalisha kwa tija na itakuwa inakinzana pia na magonjwa kwa muda mrefu. Katika suala la minazi ni kweli ilitokea hivyo lakini sasa hivi tunawashauri wananchi walime minazi inayoitwa *east african tall*.

Na. 384

Udhamini wa Serikali kwa Mashirika ya Umma

MHE. DR. WILLBROAD P. SLAA aliuliza:-

Kwa kuwa taarifa ya *CAG* kifungu cha 6 (2) (10) inayoonesha kuwa, udhamini wa Serikali kwa Mashirika ya Umma umezidi kuongezeka licha ya kwamba, Mashirika hayo yamebinafishwa/kukodishwa, mathalani udhamini umeongezeka toka Shs. 64.8 bilioni mwaka 2004/2005 hadi Shs. 73.1 bilioni mwaka 2005/2006 na kufikia kiasi cha Shs. 202.5 bilioni mwaka 2006/2007 sawa na ongezeko la 177%:-

(a) Je, ni mashirika gani kwa majina yanendelea kupata udhamini huo, na ni kisi gani kwa kila shirika; na kati ya hayo ni yapi bado yapo hai?

Mathalani Shirika la *SUKITA* linafanya kazi gani na Wakurugenzi wake ni akina nani?

(b)Kwa kuwa, *CAG* awali alishauri kuwa, hatua madhubuti zichukuliwe kuhakikisha kuwa kabla mashirika husika kudhaminiwa kupata mkopo yanafanyiwa tathmini ya kutosha kuona kama yanakopesheka.

Je, ni mashirika mangapi yalifanyiwa tathmini ya kina kabla ya kudhaminiwa? Na ni nini athari ya udhamini bwa Mashirika hayo kwa Serikali iwapo yakifilisika na kushindwa kulipa mikopo iliyodhaminiwa?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIA S. SUMARI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Fedha na Uchumi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa *Dr. Wilbroad Slaa*, Mheshimiwa Mbunge wa Karatu, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kudhamini mikopo ya mashirika na kampuni mbalimbali kwa kuzingatia manufaa, umuhimu wa huduma zinazotolewa na mashirika na makampuni hayo kwa wananchi, nchi na uchumi wa Taifa. Kiasi cha mikopo kilichotolewa na vyombo mbalimbali vya fedha nchini chini ya udhamini wa Serikali ni kama ifuatavyo:-

1. *TANESCO* Tshs. 139,314,978,184/=.
- 2.. *ATC Ltd.* Tshs. 72,000,000,000/=.
3. *State Motor Corporation (SMC)* Tshs. 2,898,840,716/=.
4. Mamlaka ya Mkonge (*TSA*) Tshs.1,024,933,969/=.
5. *SUKITA* Tshs. 10,139,494,513/=.
6. Chama Cha Ushirika Mara Tshs. 8,502,977,181/=.
7. Kiwanda cha Nguo cha Urafiki Tshs.25,781,394,288.75/=.
8. *Genaral Tyre East Africa* Tshs. 12,530,800,000/=.
9. Chama Cha Ushirika cha Nyanza Tsh.1,370,509,071.27/=.

(b) Mheshimiwa Spika, tathmini ya kina kwa kila shirika au Kampuni hufanywa na wataalamu wa Serikali kabla ya kutoa udhamini wa mikopo ili kuainisha uwezo wa mradi, shirika au kampuni wa kulipa deni linalodhaminiwa na faida na hasara kwa jamii, taifa na uchumi wa nchi kwa ujumla.

Serikali inafahamu kwamba kutoa udhamini ni kuzidisha uwezekano wa kuongezeka deni la taifa. Serikali inayo Kamati ya Taifa ya Mdeni, chini ya sheria ya Mikopo Dhamana na Misaada ya serikali, *Government Loans Guaranteens & Grants Act, 1974 as revised 2004*, ambayo wajumbe wake ni Makatibu Wakuu wa Wizara mbalimbali, Benki Kuu na Mhasibu Mkuu wa Serikali. Kazi kubwa ya Kamati hii ni kutathmini kwa kina Shirika au Kampuni inayoomba udhamini wa Serikali na hatimaye kumshauri Waziri wa Fedha na Uchumi ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, athari ya udhamini ni kwa pale shirika au kampuni inaposhindwa kulipa deni lililotokana na dhamana iliyotolewa, Serikali itatakiwa kulilipa deni husika. (*Makofi*)

MHE. DR. WILBROAD P. SLAA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi niulize maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa shirika kama *TANESCO* peke yake linadaiwa bilioni 139. Na kwa kuwa shirika la *TANESCO* kwa dhahiri kabisa ni shirika la wananchi, shirika la nchi, shirika linalogusa maisha ya watu wengi. Ili kupunguza makali ya umeme ni kwanini Serikali sasa isifute deni hili na kulichukua moja kwa moja ili *TANESCO* iweze kupunguza makali yake kwa wananchi na labda hata bei ya umeme kupungua katika nchi? (*Makofi*).

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa shirika kama *SUKITA* lilishafilisika siku nyingi na kwa bahati mbaya Waziri, hakusoma hata hiyo sehemu ameiruka, sijui ni kwanini ameiruka? Kwa kuwa sehemu hiyo haikusomwa na shirika limefilisika, maana yake ni Serikali inatakiwa kulipa deni hilo. Na kwa kuwa utafiti unaonyesha kwamba sehemu kubwa ya deni hili lilitokana na kiuingiza nchini makontena ya pombe kali pamoja na matairi kwenye miaka ya 85 kwenda kwenye miaka ya 90 na waliolifilisi shirika hili wanajulikana na Serikali. Sasa kwa kuwa limefilisika Serikali, maana yake Taifa, litalipa hili deni. Kwanini Serikali haijachukua hatua kwa wale wote waliohusika kulifikisha shirika katika hatua ambayo limefikia? Hizi ni hela nyingi zingetosha kujenga madarasa mengi sana.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIA S. SUMARI): Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa *Dr. Wilbroad Peter Slaa*, Mbunge wa Karatu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kuhusu kufuta madeni ya *TANESCO*. Nakubaliana naye ni fedha nyingi kweli ambazo zimedhaminiwa na Serikali hapa. Lakini ufutaji wa madeni ya Serikali una taratibu zake na pale itakapofikia kwamba Serikali inaona ni busara kufanya hivyo basi ninaamini hilo litafanyika. Kuhusu *SUKITA*. Ni kweli *SUKITA* ilifilisika na iko chini ya mfilisi ambaye bado anaendelea na kazi yake. Moja ya kazi za mfilisi ni kutafuta wale wanaodai shirika husika na wale wanaodaiwa na *SUKITA* yenye na baadaye kulipa wale ambao wanadai kutokana na makusanyo ama mauzo ya rasilimali ambazo zitakuwa zimekutwa kwenye lile shirika. Sio lazima kwamb hatimaye Serikali itatakiwa ilipe kutokana na dhamana ile kutokana na sheria za ufilisi.

MHE. JOHN M. CHEYO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana na hongera kuwa *President* wa *CPA*. Kwa kuwa inaonyesha wazi kwamba udhamini huu umeongezeka kwa kasi kubwa sana kutoka 73.1 bilioni mpaka 202.5 bilioni. Na kwa kuwa hata jana pameonekana pamekuwa na udhamini wa aina mbalimbali ambao unatolewa na Serikali. Mheshimiwa Waziri, haoni kwamba kuna haja ya kuleta Muswada hapa Bungeni, ili kuzuia kiasi fulani *at the minimum level* ya udhamini huu ili Serikali isiendelee kutoa fedha nyingi sana ambazo baadaye itadaiwa na itazuwia miradi mingine ya Maendeleo kwa sababu inapaswa kulipa?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIA S. SUMARI): Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Cheyo, Mbunge wa Bariadi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli udhamini wa mikopo wa serikali kwa Mashirika na Makampuni umeongezeka. Lakini si ajabu kwamba umeongezeka. Tumesikia hapa na tumeambiwa kwamba uchumi wa nchi umekuwa, pato la taifa limekuwa. Lilikuwa kwa 7.1% mwaka jana tunategemea *GDP* itakuwa kwa 7.8% mwaka huu. Na udhamini huu unaongezea haya Mashirika na Makampuni uwezo wa kushiriki na kukuza uchumi wa taifa. Kwa hiyo, ni lazima tukubali kwamba kwa kadiri uchumi utakavyokuwa unakuwa udhamini nao pale unapohitajika ni lazima uchumi utaongezeka. (*Makofi*).

Mheshimiwa Spika, la pili. hatuwezi kukuza uchumi wa taifa letu kwa *currency notes*, kwa pesa taslimu, ni lazima tu-create credit. Na hii ndio hiyo tunafanya, we are creating credits for the economy. Ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana, tunaendelea Waheshimiwa Wabunge swali linalofuata ni Wizara ya Katiba na Sheria linaulizwa na Mheshimiwa Savelina Mwijage, naomba nichukue nafasi hii kukupa pole kwa yote, ni mtihaniwa Mungu mimi sikuwapo wakati

wote. Kwa hiyo, sikupata nafasi ya kukupa pole. Pole sana na Mwenyezi Mungu akupe ujasiri.

MHE. SAVELINA S. MWIJAGE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Na. 385

Upungufu wa Mahakimu za Mwanzo

MHE. SAVELINA S. MWIJAGE aliuliza:-

Kwa kuwa, idadi ya watu inaongezeka kwa kasi katika maeneo yote ya Mijini na Vijijini, hali inayosababisha kuongezeka kwa vitendo vya uvunjaji wa Sheria na kwa kuwa, Hakimu wa Mahakama za Mwanzo hasa maeneo ya Vijijini kuhudhuria zaidi ya Mahakama moja ni kutu kinachosababisha kesi kuchukua muda mrefu sana katika Mahakama za Mwanzo bila kusikilizwa na hivyo haki za watusika kuwa mashakani.

Je, Serikali haioni kuwa huu ni wakati muafaka wa kuongeza idadi ya Mahakimu na Mahakama za Mwanzo?

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Savelina S. Mwijage kama ifuatavyo.

Serikali inakiri upungufu wa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo unaosababisha Hakimu mmoja kuhudhuria zaidi ya Mahakama moja na hivyo kuathiri utendaji wake wa kazi kwa kusababisha kesi kukuchukua muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, nilipokuwa najibu swali namba 149 katika Kikao cha Tarehe 2 Julai, 2008 la Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, nililiambia Bunge lako Tukufu kwamba Serikali kupitia Mahakama ina mikakati ya kutatua tatizo la upungufu wa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo kwa kufanya yafuatayo:-

- (a) Kuajiri wahitimu wa Stashahada ya Sheria kutoka Chuo cha Lushoto.
- (b) Kuwaajiri kwa mkataba Mahakimu waliokwisha staafu na wenye sifa nzuri. Serikali inaamini kwa kupitia mkakati huu inaweza kumaliza kabisa tatizo kubwa la uhaba wa Mahakimu Mahakama za Mwanzo na hivyo kuongeza ufanisi wa kusikiliza kesi na kutoa huduma bora kwa wananchi.

(c) Kwa sasa Serikali inalifanya kazi wazo la kuajiri Wanasheria wenye digrii kuwa Mahakimu wa Mahakama za mwanzo.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaamini kwa kupitia mkakati huu inaweza kumaliza kabisa tatizo kubwa la uhaba wa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo na hivyo kuongeza ufanisi wa kusikilizwa kwa kesi na kutoa huduma bora kwa wananchi.

MHE. SAVELINA S. MWIJAGE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa kuwa bado Wizara hii ina mikakati hiyo ya kuwaajiri hao wa Stashahada. Je, hawaoni kwamba hao wananchi ambao wana kesi zao kwa muda mrefu wanapata matatizo na wanaendelea kusota Magereza au Mahabusu hasa katika Mkoa wa Kagera?

La pili, Wizara haioni kwamba ni uchache wa mahakimu unachochea sana Mahakimu wachache kula rushwa mara kwa mara?

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Savelina S. Mwijage, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, nimekiri uhaba wa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo kwa kweli hili ni tatizo na nimeeleza mikakati ambayo tunaifanya ili kujaribu kupunguza matatizo ambayo Mheshimiwa Savelina S. Mwijage ameyasema.

Naomba Mheshimiwa Savelina S. Mwijage aniamini na akubali kwamba mikakati hii ni ya dhati na kwa kweli tutaifanya kazi hii na matatizo anayoyasema ya watu kusota kwa muda mrefu wakisubiri kesi zao zikamilishwe yatakwisha pindi tutakapoanza hasa utaratibu wa kuajiri hawa *graduates* kwenda kwenye Mahakama za Mwanzo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu rushwa ni kwamba rushwa ni suala la mtambuka katika nchi yetu na haipo Mahakamani tu, iko sehemu zote tu. Lakini Mahakama inachukua hatua kali sana kwa Mahakimu ambao wanajishughulisha na rushwa pale tunapowapata. Lakini kama nilivyosema rushwa ni suala la mtambuka na nchi ina mkakati kwa nchi nzima kupambana na rushwa. (*Makofit*)

MHE. MGANA I. MSINDAI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swalii moja la nyongeza.

Kwa kuwa, kwa kweli tumeona Serikali inajitahidi kutumia njia mbalimbali kuongeza Mahakimu.

Je, itatumia njia zilezile kuwajengea nyumba na kuwapa vitendea kazi vingine ili wakiajiriwa wasipate taabu?

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Mgana I. Msindai, kama ifuatavyo.

Nashukuru kwamba ameona juhudii zetu tunazozifanya katika kuongeza Mahakimu, sasa nataka kumweleza ni mkakati mwingine ambao tunataka kuuleta ndani ya Bunge hili katika Bajeti ambayo nitaisoma leo wa kujaribu kuzitaka Halmashauri zetu zishiriki katika utaratibu wa kujenga Mahakama na nyumba za Mahakimu pale tunapojenga Mahakama hizo.

Kwa utaratibu huo naamini kabisa tutaweza kutekeleza yale ambayo Mheshimiwa Mgana I. Msindai ameyaomba.

Na. 386

Utaratibu wa Kuajiri Wataalamu wa Afya

MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE aliuliza:-

Kwa kuwa, utaratibu wa ajira ya watumishi wa afya unafanywa na Wizara ya Afya kwa maana ya kutangaza nafasi, kusaili na baadaye kugawa kwenye Halmashauri mbalimbali nchini.

(a)Je, Serikali haioni kuwa utaratibu unasababisha wataalamu wengi kutokwenda kwenye Halmashauri?

(b)Je, Serikali iko tayari kukubali utaratibu wa kuajiri wataalamu ufanywe kwenye Halmashauri husika?

SPIKA: Hawa Wabunge vijana huwa wanafurahisha sana maana wanaondoka kwa mikogo wakati wa kusimama. Sasa sikuweza (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Waziri majibu tafadhali!

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa George B. Simbachawene, Mbunge wa Kibakwe, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8 ya mwaka 2002 pamoja na marekebisho yake ya mwaka 2007, Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003, Makatibu Wakuu wa Wizara, Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakurugenzi wa Majiji, Manispaa, Miji na Wilaya ni Mamlaka halali za ajira. Hivyo, wao ndiyo wenye wajibu wa kuajiri watumishi mbalimbali wakiwemo watumishi wa afya kwenye Mamlaka zao.

Mheshimiwa Spika, kutokana na tatizo la upungufu mkubwa wa watumishi wa afya nchini na kutokana na uhaba wa watumishi hawa katika soko la ajira, kwa makusudi kabisa Serikali iliamua kulegeza masharti ya ajira ya watumishi wa afya kwa kuondoa sharti la usaili.

Aidha Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii imepewa jukumu la kurahisisha upatikanaji wa watumishi kwa kutangaza na kuwapangia vituo vyta kazi watumishi wa afya kulingana na kibali kilichoidhinishwa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi

wa Umma. Kibali hicho hutokana na majadiliano kati ya Halmashauri/Mkoa husika na Menejimenti ya Utumishi wa Umma, kwa kuzingatia mahitaji ya Halmashauri au Mkoa.

Hata hivyo, pamoja na amfanikio yaliyopatikana ya kuwapata watumishi na kuwapanga kwenye Halmashauri bado tatizo la baadhi ya wataalamu kutokwenda linaendelea. Ili kuondoa tatizo hili, Wizara imeweka utaratibu kila kanda zikishirikiana na Mikoa husika na Halmashauri kuweka matangazo katika maeneo yao na kisha kupokea maombi yao, kuiyaorodhesha na kuwasilisha Wizarani.

Zoezi hili limelenga kusaidia kuwapatia watumishi na kuwapanga. Zaidi ya hapo, utaratibu huu umepunguza adha ya mtumishi mtarajiwu kuandaa nauli ya safari na pia punde anapoajiriwa kutopata usumbufu wa kuchelewa kwa mshahara akiwa ugenini zoezi hili kwa ujumla limesaidia kuwapata wataalamu mapema baada ya kumaliza mafunzo yao.

Naomba kuchukua nafasi hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge na Viongozi wa Halmashauri kuwa makini wakati wa kujadili kibali na menejimenti ya Utumishi wa Umma kulingana na mahitaji yao halisi. Aidha, watoe ushirikiano wa karibu kwa Mikoa, kanda na Wizara wakati wa kutangaza kuandaa orodha ya waombaji na kuwasilisha Wizarani.

MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa niipongeze Serikali kwa namna ambavyo inahangaika sana na jambo hilo la upungufu wa watumishi wa afya.

Lakini pia nimpongeze Naibu Waziri kwa majibu mazuri ambayo kwa kweli amekubaliana na mimi kwamba upungufu huu ni mkubwa na hili tatizo ni kubwa na ni janga. Lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

La kwanza, hali ilivyo sasa katika Wilaya ya Mpwapwa si nzuri kwa sababu katika kibali ambacho tulikuwa tupatiwe watumishi 117 amba waliomba na kukubaliwa na Wizara waliofika na kuripoti ni tisa (9) tu.

Hali hii ni mbaya inasababisha Zahanati zilizojengwa na wananchi kukosa watumishi na wananchi kuona kwamba wamepoteza nguvu zao bure lakini pia wanapata matatizo. Zahanati ya Seruka, Kikuyu, Ikuyu, Ruhundwa, Kituo cha Afya cha Kibakwe na Rudi vina upungufu. Sasa mimi nauliza. Je, Serikali inafikiri zaidi ya hapa tufanye nini?

La pili, kwa kuwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatoa wajibu na haki kwa kila Mtanzania na Katiba hii inaweka Wajibu wa kila Mtanzania kutumia elimu yake na ujuzi wake kuweza kuwatumikia wengine. Hawa amba wanapata ujuzi lakini hawautumii. Je, Serikali haioni kuna haja ya kuwalazimisha kutoka Vyoni wapangiwe kwenda moja kwa moja kwenye sehemu zenye upungufu na iwe ni lazima wao kufanya hivyo maana yake ni wajibu wa Kikatiba?

NAIBU WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshiwa George B. Simbachaweweze, kama ifuatavyo:-

La kwanza, ni kweli kabisa kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa watumishi waliokwenda ni tisa tu dhidi ya wale 117 amba waliotakiwa kwenda kule. Lakini kama nilivyosema kwamba Serikali inajitahidi ili kuweza kuhakikisha kwamba hawa amba tunawapangia tunawapeleka kule lakini vile vile tumetoa mbinu mbadala ili wao wenyewe Halmashauri wakiweza basi waweze kutangaza. Ninachowea kusema tu ni kwamba mimi nawashauri Waheshimiwa Wabunge na vilevile waweze kuangalia katika Halmashauri zao uwezekanao wa kuweza kuweka mazingira mazuri ili wale wafanyakazi wanaokuja kufanya kazi kule waweze kuvutika kukaa kule kwa sababu wengi wanaokwenda kule huwa wanaogopa wakienda kule wanakosa mahali pa kukaa na kadhalika. Kwa hiyo, inakuwa ni vigumu kwao kubakia kutokana na mazingira magumu.

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile ningewashauri kwamba tuwe na utaratibu basi hata Ma-*DMO* na wenyewe waweze kwenda katika vyuo na kuangalia ni nani na kuweza kuwashawishi kwa sababu hata huu ushawishi pia ni kitu kizuri mtu unamhakikishia kwamba akifika kule atakuwa na maisha mazuri zaidi kwa sababu wengine kwa mfano mtu hawezi kujuua Ruhundwa ni wapi ukimwambia aende Ruhundwa Kibakwe inawezekana pengine akawa na wasiwasi kidogo. Lakini Serikali itajitahidi kuhakikisha kwamba hawa wanafika walikopangiwa.

Mheshimiwa Spika, lakini swali la pili ni kweli kabisa mtu aliyesomeshwa ana haki kwa sababu amepewa elimu na Umma. Lakini vilevile kuna ile haki ya mtu ambayo baada ya soko huria kulilegezwa masharti kwamba mtu anaweza kufanya kazi mahali popote na yeche pia ni haki yake kuchagua mahali pa kukaa na kufanya kazi kwa maslahi yake.

Lakini nadhani imefikia wakati sasa tuliangalie upya kama Serikali kama tulivyokuwa tunafanya zamani tulipokuwa tunawawekeza watu *bonds* ili tuone kwamba huyu mtu ambaye anamaliza chuo na ambaye amesomeshwa na Serikali tutambana vipi ili aweze kwenda kufanya kazi nadhani hii itapunguza adha hii ambayo tunaipata sasa.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofî*)

Na. 387

Vifo Vinavyotokana na Uzazi

MHE. PARMUKH SINGH HOOGAN aliuliza:-

Kwa kuwa, tatizo la akina mama kufariki wakati wa kujifungua limeongezeka sana na limekuwa la kutisha sana hapa nchini na hata kule Tanzania Zanzibar na kwa kuwa, tatizo hilo limeonekana kuongezeka siku hadi siku na akina Mama wengi wanaendelea kupoteza maisha yao na kuhofia Wanawake wengi kupoteza maisha yao

siku zijazo; na kwa kuwa, tatizo hilo lilnasababishwa na upungufu mkubwa wa wataalamu wa matatizo ya Wanawake katika nchi yetu hasa huko Tanzania Zanzibar.

Je, Serikali haioni kuwa iko haja ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ya Tanzania Bara kushirikiana na Wizara ya Afya ya Tanzania Zanzibar kwa pamoja kutafakari mbinu za kukabiliana na tatizo hilo ambalo limeonyesha madhara makubwa kwa wananchi wa pande zote za Muungano?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan, Mbunge wa Kikwajuni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tatizo la vifo vya Mama wajawazito na watoto Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar nchi yetu inakabiliwa na tatizo kubwa na vifo vya wazazi na watoto, kwa ulingano sawa kwa upande wa Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar. Takwimu zilizopo zinatoa wastani wa akina Mama 578 kupoteza maisha, kati ya 100,000 wanaojifungua watoto hai. Takwimu hizi ni za Makadirio. Hata hivyo, kulingana na malengo ya milenia lengo ni kupunguza vifo hivi kwa 50% ifikapo 2015.

Mheshimiwa Spika, ili kufanikisha kufikia lengo hili wataalam wa Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar watakutana na kuandaa. Utaratibu wa kutekeleza mpango kabambe wa kupunguza vifo hivyo, mpango unaofahamika kwa jina la *Road Map to Accelerate the Reduction of Maternal and Newborn Mortality in Tanzania*. Maandalizi hayo yatabainisha yapi yanatekelezeka Zanzibar na yapi yatakelezeka Bara, na pia kuainisha raslimali watu, fedha, dawa na vifaa vitakavyohitajika, pamoja na kutambua washirika wakuu wa Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, hili litafuata mfumo uliotumika katika kubadilishana uzoefu katika kupambana na malaria ambapo, kwa kutumia mafanikio ya Zanzibar, Bara wameweza kuzuia milipuko ya malaria kwa Wilaya mbili za Mkoa wa Kagera.

Mheshimiwa Spika, maandalizi yanaendelea kupanua mafanikio haya kwa Wilaya nyingine za Bara. Naomba kuchukua nafasi hii kuwaagiza wataalam wa Tanzania Bara kukutana na wenzao wa Tanzania Zanzibar na kuanza mipango ya kulishughulikia hili, hasa ikizingatia kuwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muunganowa Tanzania alikwisha zindua mpango huo, ambao sasa uko tayari kwa utekelezaji ili sote tufikie malengo ya milenia.

MHE. JAMES P. MUSALIKA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa, kwa upande wa Tanzania Bara vifo vya akina mama wajawazito sababu mojawapo inayosababisha vifo hivyo ni kukosekana kwa magari ya wagonjwa katika vituo vya afya. Je, Serikali iko tayari kwa wataalam wake na Watendaji wake

kupunguza semina na makongamano, safari za nje zisizo za lazima ili pesa itakayookolewa inunue magari ya wagonjwa katika vituo vya afya na kuanzia kuyagawa kwenye Wilaya zenye watu wengi kama Geita hususan kituo cha Afya cha Nyang'wale, Kasamwa, Katoro na sehemu nyingine hapa nchini?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa James P. Musalika la kama ifuatavyo.

Ni kweli kabisa sababu mojawapo ya vifo vya akina mama ni kukosekana kwa usafiri kuwatoka katika maeneo ambayo wanatakiwa kwenda kupata rufaa na hii inashindikana kwa sababu ya kutokuwepo na *Ambulance* katika baadhi ya vituo.

Tunakubaliana kabisa kwamba *Ambulance* ni muhimu lakini Serikali kwa kushirikiana na TAMISEMI tunapanga mikakati mojawapo ikiwa ni kupunguza yale matumizi ambayo hayana ulazima. Lakini vilevile Wizara ya Afya inachukua jukumu la kutoa elimu kuwafundisha akina mama ili waanze kliniki mapema na wale akina Mama wenye matatizo waweze kuambiwa wapi kwa kujifungulia ili waweze kuijandaa wasije wakapata matatizo wakati wanapopata uchungu.

Kwa hiyo, hili tunalichukua kama ni changamoto lakini vilevile na elimu itaendelea ili akina Mama wachukue tahadhari mapema. (*Makofi*)

MHE. ANIA S. CHAUREMBO: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa, katika jibu la msingi Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kwamba akina mama wengi wanafariki kwa ajili uzazi na kwa kuwa kwa hapa Tanzania Bara kina mama hawalazimiki kwenda na *delivery kits* hospitali au kulipa malipo wakati wa kufanyiwa *operation* inapohitajika.

Na kwa kuwa, upande wa Zanzibar kina mama wajawazito wanalazimika kwenda na vifaa vya kujifungulia na wanalazimika wakati wa *operation* kulipa 40,000/= na hii inaongezea sana tatizo la vifo vya akina mama kwa kuwa wengi wanakuwa hawana uwezo wa kulipa ada hizo.

Je, Serikali iko tayari kuishawishi Serikali ya Zanzibar kuondoa ada hizo kwa ajili ya uzazi wa akina mama kwa upande wa Zanzibar ili kupunguza vifo?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, napenda kaujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ania S. Chaurembo, kama ifuatavyo.

Kama alivyosema kwamba Zanzibar akina mama wanalazimika kulipia għarama za kupasulia tofauti na Tanzania Bara. Kama nilivyosema kwamba Serikali kwa ujumla wake na nimewaagiza wataalam wa Tanzania Bara waende wakazungumze na Serikali ya Zanzibar ili kuzungumzia ile mikakati ambayo nimesema ni hii *Road Map to Accelerate the Reduction of Maternal and Newborn Mortality in Tanzania* kwa hiyo, hili

tutalichukua kama changamoto tutakapokuwa tumekaa na wale wenzetu tutazungumza nao ili tuweze kuona ni jinsi gani basi tutasaidiana katika kutimiza huu mkakati ili kuweza kupunguza vifo vya akina mama na kama ikibidi basi wao waweze kupunguziwa badala ya kulipia Serikali ya Zanzibar iweze kuchukua jukumu hilo.

Lakini siwezi nikatamka hapa kwamba niwaagize Zanzibar kwa sababu bado hatujakaa na tukapanga.

Na. 388

Mradi wa Umwagiliaji

MHE. ESTHER K. NYAWAZWA - K.n.y. MHE. KABUZI F. RWILOMBA
aliuliza:-

Kwa kuwa vijiji vya Isima, Nyarugaye, Saragulwa, Buzanaki, Magenge, vina mbuga nzuri kubwa za kuzalisha mpunga wa kutosha hata kuuza nchi jirani:-

Je, ni lini Serikali itawaunga mkono wananchi wa maeneo hayo kwa kuwapelekea mradi wa umwagiliaji ili waweze kuzalisha zaidi?

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Kabuzi Faustine Rwiomba, Mbunge wa Busanda, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, utaratibu uliopo hivi sasa ni kwamba miradi ya umwagiliaji katika ngazi ya kijiji huibuliwa katika ngazi hiyo na kuwekwa katika mapendekezo ya Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya (*DADPS*). Miradi inayopendekezwa na kupata fedha ni ile ambayo kwa kawaida gharama za utekelezaji hazizidi shilingi milioni 50 kwa mradi mmoja.

Mheshimiwa Spika, tayari Serikali imeanza kuwasaidia wakulima wa maeneo aliyyoyataja Mheshimiwa Mbunge kwa kuwapatia vifaa vya umwagiliaji kwa njia ya matone kupitia mradi uliogharamiwa na Serikali ikishirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Chakula na Kilimo (*FAO*) na Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Japan (*JICA*). Halmashauri ya Wilaya ya Geita imewahamasisha wananchi kuunda vikundi vya wakulima wa umwagiliaji.

Katika vijiji vya Saragulwa na Nyarugaye tayari wakulima wameshaunda vikundi hivyo. Halmashauri ya Wilaya ya Geita imewagawia wakulima vifaa vinavyojumuisha pampu, mipira ya kuvuta maji, jozi za vifaa vya umwagiliaji kwa njia ya matone (*drip irrigation kits*) na pampu za miguu pamoja na mipira yake ya kuvuta maji, na ile ya kumwagilia.

Mheshimiwa Spika, utafiti wa awali umefanyika katika kijiji cha Isima mwezi Mei, 2008. Wizara yangu itatuma wataalam kutoka Ofisi ya Umwagiliaji Kanda ya Ziwa waweze kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Geita kufanya upembuzi yakinifu katika kijiji cha Isima kwa utekelezaji zaidi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Kabuzi F. Rwilomba, Mheshimiwa Ernest Gakeya Mabina na Mheshimiwa James P. Musalika ni wafuatiliaji hodari kwa niaba ya wananchi wa Geita kuhusu masuala ya maji na umwagiliaji. Nawahakikishia ushirikiano mkubwa wa Wizara yangu. (*Makofî*)

MHE. ESTHER K. NYAWAZWA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri lakini kinachonikasirisha hapa ni kwamba kilimo cha mpunga kinatakiwa kuwa na maji mengi sasa anavyoniambia kwamba kuna mradi wa matone hapa nachanganyikiwa kabisa.

Je, Serikali imejipanga vizuri kuhakikisha kwamba zao la mpunga linalimwa katika maeneo tajwa katika swali la msingi kwa kutumia njia maalum siyo ya matone?

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Esther K. Nyawazwa kama ifuatavyo:-

Kwanza, namwomba asiwe na masikitiko Serikali yake iko imara. (*Makofî*)
La pili ni kwamba nilichosema ilikuwa ni kwa ujumla pamoja na umwagiliaji wa matone katika moja ya vijiji alivyovitaja Mheshimiwa Kabuzi F. Rwilomba lakini namhakikishia kwamba wataalam wa umwagiliaji kanda ya Mwanza kwa kushirikiana na wataalam wa Halmashauri ya Geita tayari wamefanya tathmini ya awali yaani *reconnaissance survey* ya maeneo ambayo tunaweza tukajenga mabwawa kwa ajili ya umwagiliaji hasa kwa kilimo cha mpunga na mabwawa hayo tunaweza kuyajenga katika maeneo ya Isima, Ibanda, Nyawirimirwa, Saragulwa, Kakola, Mimbili na Nzela.

Kwa hiyo, ni maeneo mengi zaidi tu ya yale ambayo tunaweza kutumia *drip irrigation*. (*Makofî*)

Na. 389

MAJI SAFI NA SALAMA KILWA KUSINI

MHE. SALIM HEMED KHAMIS aliuliza:-

Kwa kuwa, wananchi wa Kata ya Limaliyao kwenye vijiji vya Mwembemtungi na Pande Ploti huko Kilwa Kusini hawajapata maji safi na salama tangu tupate uhuru na kwa kuwa maji wanayokunywa hivi sasa hayafai hata kwa matumizi ya wanyama;

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia wananchi hao maji safi na salama ili nao waonje matunda ya uhuru?

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mbunge wa Chambani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mwaka 1980 Serikali ilikamilisha ujenzi wa mradi wa maji kwa ajili ya Kitongoji cha Mwembe Mtungi kilicho katika kijijicha Pande Ploti Kata ya Pande. Mradi huu ulifanya kazi hadi mwaka 2000 ambapo mashine ya kusukuma maji iliharibika, na baadaye chanzo cha maji ambacho ni chemchem kilikauka.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2001 mradi wa kisima katika kijiji cha Pande Ploti ulijengwa kwa msaada wa Serikali ya Japan kuititia Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Japan (JICA). Mradi huu unafanya kazi hadi sasa.

Katika mipango yake ya mwaka 2008/2009 Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa imetenga Shilingi milioni 35 kwa ajili ya utafiti na uchimbaji wa kisima kingine. Kazi hii inatarajiwaa kuanza mwezi Septemba, 2008.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis ni Mbunge wa Chambani, Mkoani Kusini Pemba, kwa kuuliza swalii linalohusu kitongoji cha Mwembemtungi, kijiji cha Pande Ploti, Kata ya Pande, Jimbo la Kilwa Kusini, inathibitisha kwamba hali ya Muungano wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni imara. (*Kicheko/Makofit*)

MHE. SALIM HEMED KHAMIS: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali madogo ya nyongeza.

Kwa kuwa, wanakijiji cha Mwembemtungi wenyewe wanakiri kwamba maji wanayokunywa sasa hivi hayafai hata kwa matumizi ya wanyama na kwamba toka uhuru hawajaonja hasa matunda ya maji safi na salama.

Na kwa kuwa, wanalamika kwamba kuna uwezekano wa kuwa afya zao zimeathirika kutokana na matumizi hayo ya maji yasiyo salama. Je, Serikali iko tayari sasa kuhusisha taasisi mbalimbali kufanya uchunguzi wa afya zao ili kubaini ni kiasi gani wameathirika na kupatiwa matibabu?

Kwa kuwa, Serikali imekiri kwamba kuna kisima cha *JICA* katika kijiji cha Pande Ploti, lakini ukweli ni kwamba kisima kile hakitoshelezi mahitaji ya Pande Ploti *south* ya Kijiji cha Mwembemtungi.

Kwa nini Serikali imechelewa muda wote huo kufanya utafiti na kuchimba visima vingine kiasi kwamba tafiti zinaonyesha kwamba hata shughuli nyingine za Maendeleo zimekwama kiasi kwamba Wanawake inabidi wasafiri masafa marefu mno kutafuta maji safi na salama?

Mheshimiwa Slpika, ahsante sana. (*Makofî*)

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Salim Hemed Khamis Mbunge wa Chambani yaliyohusu Kilwa Kusini kama ifuatavyo:-

Kuhusu afya za wananchi nadhani Mheshimiwa Salim Hemed Khamis alisikiliza hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya kuhusu mpango wa kuboresha afya za wananchi nchini ikiwa ni pamoja na wananchi wa Kilwa Kusini.

Kwa hiyo, hilo limeshachukuliwa na wenzetu wa afya kwa hiyo litatekelezwa kama alivyosikiliza hotuba ya Waziri wa Afya kwa niaba ya Serikali.

La pili kuhusu kisima kisichotosheleza nadhani nimemwahidi kwamba kisima kingine kinajengwa kwa hiyo ni juhudhi moja ya Serikali lakini vilevile kwa upande wa wa Kilwa kwa ujumla tumepeleka shilingi milioni 103,950,000/=kwa ajili ya matatizo ya dharura ambayo yanaweza kutatuliwa na fedha hizi zinaweza kutumiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa kwa ajili ya eneo hilo na maeneo mengine.

Lakini niseme vilevile kwamba Kilwa ni moja ya Wilaya zile nilizozitaja 82 katika kauli yangu ya tarehe 9 Julai, 2008 kwamba wameruhusiwa kuanza mchakato wa utekelezaji wa vijiji kumi (10) baada ya Benki ya Dunia kutoa kibali cha sisi kuendelea na mradi huo.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kutangaza kwamba katika hotuba yangu au katika kauli yangu ya tarehe 9/7 nilisema kulikuwa na Halmashauri 17 ambazo tuliwarudishia tathmini wafanye upya kabla hatujapeleka maombi yao tena Benki ya Dunia, naomba kutangaza kwamba sasa zile Halmashauri 17 zimepata kibali na kuanzia jana (12/8/2008) tumeshatoa taarifa katika magazeti na sasa Halmashauri 99 tayari zinaweza kuanza mchakato wa utekelezaji wa vile vijiji 10 mbali na zile 33 ambazo tayari tumeomba watangaze upya.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. (*Makofî*)

SPIKA: Ahsante sana, natumaini baina ya Halmashauri hizo Mheshimiwa Waziri na Urambo ipo. (*Kicheko*)

Kwa hiyo, tunaendelea na Wizara ya Nishati na Madini na swali linaulizwa na Mheshimwa Fred Tungu Mpandazoe, Mbunge wa Kishapu.

Kupeleka Umeme Makao Makuu ya Kishapu

MHE. FRED M. TUNGU aliuliza:-

Kwa kuwa Mji wa Kishapu ni moja kati ya Miji ambayo haijapata huduma ya umeme na kwa kuwa umeme unaweza kuchochea maendeleo na kukua kwa huduma nyingine za jamii:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka umeme Makao Makuu ya Wilaya ya Kishapu?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Fred Mpandazoe Tungu, Mbunge wa Kishapu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kitongoji cha Kishapu kilipata umeme mwaka 1996. Hata hivyo, mahali ambapo panajengwa Ofisi za Wilaya katika Kitongoji hicho hakuna umeme. Umbali kati ya mahali panapojengwa Ofisi za Wilaya na inapoishia miundombinu ya umeme ni kilomita tatu.

Mheshimiwa Spika, kwenye Kitongoji cha Kishapu kuna zahanati ambayo tayari imefikiwa na huduma ya umeme. Kufuatia Kitongoji cha Kishapu kutangazwa kuwa Makao Makuu ya Wilaya, majengo mbalimbali ya utawala yanahitaji umeme ili kutekeleza kwa ufanisi majukumu ya kiutawala. Hivi sasa Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya inaingia gharama kubwa ya kuendesha jenereta hasa ikizingatiwa bei za mafuta zinavyopanda.

Mheshimiwa Spika, gharama za kufikisha umeme mahali panapojengwa majengo ya Ofisi za Wilaya ya Kishapu ni Sh. 199,158,566.40. Kiasi hiki cha fedha kitatumika katika ujenzi wa njia ya umeme ya msongo wa KV 33, njia ndogo ya kusambaza umeme yenye urefu wa kilomita mbili, ujenzi wa *substation* ya KV 33 na uwekaji wa *transfoma* ya *KVA* 100 KV 33/0.4.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaangalia uwezekano wa kufikisha umeme katika majengo ya Ofisi za Wilaya ya Kishapu kupitia ufadhilli wa Wakala wa Nishati Vijini (*REA*). Hivyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge pamoja na wananchi wa Kitongoji cha Kishapu wavute subira wakati Serikali inatafuta fedha za kufikisha umeme katika maeneo ya Kitongoji cha Kishapu pamoja na vitongoji vingine vya Wilaya ya Kishapu ambavyo bado havijapatiwa umeme.

MHE. FRED M. TUNGU: Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali kwa mipango ya kupeleka umeme katika Makao Makuu ya Wilaya ya Kishapu kama alivyoeleza Mheshimiwa Naibu Waziri lakini nina swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa

Serikali itatekeleza Mradi wa Umeme Vijijini kama alivyoeleza Mheshimiwa Naibu Waziri na kwa kuwa Wilaya ya Kishapu upande wa Mashariki kuna Mji wa Ndoleleji, Shagihilu na Mangu na upande wa Magharibi kuna Miji ya Mwigumbi, Mipa na Bubiki: Je, Serikali ipo tayari kuiingiza Miji hiyo kwenye mkakati wakati inashughulikia suala la umeme katika Mji wa Kishapu?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa nilishaandikia Wizara kumwomba Mheshimiwa Naibu Waziri atembelee Wilaya ya Kishapu na kuangalia matatizo au kero za umeme katika Wilaya hiyo: Je, Naibu Waziri atatoa *commitment* leo kwamba baada ya Bunge lako Tukufu atafanya ziara katika Wilaya hii?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mpendazoe kwamba maombi yake ya vijiji vya Njololeje na vijiji vingine vilivyotajwa tumeyapokea.

Lakini labda niseme kwa ufupi kwamba Kitongoji cha Njololeje kipo kama kilomita thelathini hivi kutoka pale ambapo umeme umeishia Kishapu, kwa hiyo ni lazima *TANESCO* wafanye tathmini ya kujua gharama iliyopo halafu baada ya hapo katika maswali yetu tuna kawaida ya kupeleka miradi yote ya vijiji ya umeme lakini matarajio ni kwamba *REA* wanafanya tathmini ya viability ya miradi yote hii. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie kwamba nitachukua vijiji vyote alivyoorodhesha na nitawakabidhi *REA* wavifanyie tathmini ili tujue utekelezaji wake utakuwaje.

Mheshimiwa Spika, la pili, kweli Mheshimiwa Mpendazoe aliwahi kuja Wizarani na aliomba tutembelee Wilaya yake kwa masuala pia ya wachimbaji wadogo wadogo. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie kwamba baada ya Bunge lako Tukufu tutafanya ziara hiyo Wilayani Kishapu kwa ajili ya kuangalia masuala yanayohusika na madini na masuala yanayohusika na umeme pia.

SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha lakini limebaki swali moja tu. Kwa hiyo, tunakwenda Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi na nimeelezwa kwamba swali lililokuwa liulizwe na Mheshimiwa Mpina litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Luhahula.

Na. 391

Wananchi Kotonufaika na Hifadhi za Taifa Zinazowazunguka

MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA (k.n.y. MHE. LUHAGA J. MPINA)
aliuliza:-

Pamoja na Serikali kujenga mahusiano na ujirani mwema kwa wananchi waishio kandokando ya Hifadhi za Taifa lakini bado hawanufaiki vyema na rasilimali hiyo, mfano, Hifadhi ya *Maswa Game Reserve* iliyoko Meatu, wananchi wana malalamiko ya kuharibiwa mazao yao na wanyama kama vile tembo na hawapatiwi msaada wa haraka

maeneo ya kilimo na ya malisho ya mifugo, shughuli za utamaduni kuchukuliwa, kukamatwa na kuwekwa mahabusu muda mrefu bila kosa kusikilizwa na huduma za kiuchumi kuboreshwa taratibu mno:-

Je, ni lini Serikali itatenga maeneo ya malisho ya mifugo, sanjari na kuchimba malambo kwa matumizi ya binadamu na mifugo kwa vijiji vya kandokando Jimboni Kisesa na sehemu nyingine?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI alijibu:

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, Mbunge wa Kisesa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Meatu inapakana na Hifadhi ya Taifa ya Serengeti na Pori la Akiba la Maswa (*Maswa Game Reserve*) kwa kuzungukwa na vijiji 29, Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Meatu na kwa kushirikiana na Taasisi isiyo ya Kiserikali ya *Frankfurt Zoological Society (FZS)* imekamilisha uandaaji wa mipango ya matumizi bora ya ardhi katika Vijiji saba vya Makao, Mwangundo, Irambandogo, Mbushi, Sapa, Mwabagimu na Mwanjoro. Hadi sasa jumla ya hekta 228,296 zimepimwa kwa ajili ya makazi, kilimo, misitu, wanyamapori na malisho. Kati ya ardhi hiyo hekta 100,728 za ardhi zimetengwa kwa ajili ya wakulima/wafugaji (*Agro pastoralists*) ambapo maeneo hayo yapo katika Vijiji vya Makao hekta 21,230; Mwangundo hekta 2,603; Irambandogo hekta 16,078; Mbushi hekta 23,449; Sapa hekta 8,068; Mwabagimu hekta 10,160 na Mwanjolo hekta 19,135. Serikali itaendelea kutenga na kupima maeneo ya malisho kutegemeana na upatikanaji wa fedha kwa vijiji vyote kandokando ya mapori niliyoyataja pamoja na vijiji vingine.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa uchimbaji wa malambo ya maji, Serikali inaendelea kutekeleza jukumu hilo kupitia Mpango wa Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya (*DADPs*). Kwa mfano, mwaka 2006/2007, Wilaya ya Meatu imechimba malambo manne katika Vijiji vya Mwangundo, Mwabagimu, Mbushi na Mwanjolo. Aidha, katika mwaka 2008/2009, Halmashauri ya Wilaya ya Meatu inatarajia kujenga malambo matatu katika vijiji vya Lata, Mwakasumbi na Mwakisandu kwa jumla ya Sh. 105m/= ikihusisha nguvu za wananchi wa vijiji husika.

MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu hayo, inaonyesha jinsi gani Serikali inatekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi katika Wilaya ya Meatu. Maswali, kwa kuwa utekelezaji huu umeonekana na matumizi bora ya ardhi yamesemwa na kuainishwa: Je, Serikali kwa sababu tunapochimba malambo ni lazima yaende sambamba na majosho: Je, katika mwaka huu watu wa Kisesa mtawajengea majosho?

Mheshimiwa Spika, la pili, kwa kuwa katika hotuba ya Waziri wa ardhi niliongelea suala la kutenga matumizi ya ardhi bora katika Wilaya ya Bukombe na katika Wilaya ya Bukombe tunapakana na hifadhi na wafugaji wa Bukombe wanapata shida

sana kupata malisho. Je, Wizara hii kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi mwaka huu watakuja kutenga maeneo ya wafugaji wa Bukombe ili wasihangaike?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, napenda kuwahakikisha wananchi wa Kisesa na Meatu kwamba ili kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi majosho matano yanatarajiwa kujengwa katika Wilaya ya Meatu. Kati ya hayo, matatu yatakuwa katika Jimbo la Kisesa ambayo yatachimbwa katika Vijiji vya Mwakaluva, Magaye na Luviga na mawili yatajengwa katika Jimbo la Meatu ambayo yatajengwa katika Vijiji vya Minyanda na Usiulize. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, ndiyo jina la kijiji hicho.

SPIKA: Endelea tu Mheshimiwa Waziri hakuna shaka.

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, kuhusu upimaji wa ardhi, kwa ujumla Serikali imedhamiria kuhakikisha kwamba wananchi wanapimiwa ardhi ili kwa shughuli mbalimbali tutenge sehemu ya kilimo na sehemu ya mifugo. Kwa sababu hiyo basi, nataka kumhakikisha Mheshimiwa Mbunge kwamba, kama fedha zitapatikana, hatutasita kushirikiana na Wizara ya Ardhi na Halmashauri ya Wilaya yake kupima maeneo ya ardhi kwa ajili ya matumizi mbalimbali.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha na muda wa maswali umepita. Matangazo nikianza kama kawaida na wageni, Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Mathias Meinrad Chikawe anao wageni mmojawapo ni Mheshimiwa Jaji Mkuu ambaye nilikwishamtambulisha kwenu na alisimama. Tunarudia kumshukuru tena kwa hatua hii aliyochukua ya kuja hapa Bungeni katika Ukumbi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Jaji Mkuu amefuatana na Mama Sada Ramadhani ambaye ni mkewe, naomba tafadhalii asimame ili tumtambue. Ala, nadhani ana udhuru!

Pia yupo Mkewe Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria ambaye anaitwa Profesa Amandina Lihamba. Yule pale. Karibu sana Mheshimiwa. (*Makofi*)

Yupo Naibu Mwanasheria Mkuu na Katibu Mkuu Bwana Sazi Salula. Yule pale ndiye Katibu Mkuu wa Wizara, karibu sana. (*Makofi*)

Wapo vilevile Majaji kama ifuatavyo: Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu Kanda ya Dodoma, Mheshimiwa Mary Shangali, mwenyeji wa Jaji Mkuu. Jaji Mfawidhi Mahakama Kuu Kitengo cha Biashara Mheshimiwa Catherine Orio. Hakuna hata vigelegele leo humu! Sijui namna gani! (*Vigelegele/Makofi*)

Pia wapo Mheshimiwa Jaji Alice Chinguwile, Mheshimiwa Jaji Mwanaisha Kwariko, sijui nimepatia jina, naona kuna tatizo. Mkuu wa chuo cha Uongozi wa

Mahakama Lushoto Mheshimiwa Jaji Emilian Mushi, Mheshimiwa Jaji Shaban Lila, Msajili Mahakama ya Rufaa, Mheshimiwa Ferdinand Wambali; Msajili Mahakama Kuu, Mheshimiwa Eliamini Mbise; Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Mheshimiwa Jaji Kiongozi Mstaafu Amir Manento; Makamu Mwenyekiti wa Tume ya Hazi za Binadamu na Utawala Bora, Mheshimiwa Mahafudha Aley Hamid, yule pale. (*Makofi*)

Vilevile, wapo Waheshimiwa Makamishna wa Tume ya Haki za Binadamu kama ifuatavyo: Mheshimiwa Sofia Masoud Khamis, Mheshimiwa George Francis Mlawa, Mheshimiwa Wakili Joacline Demelo, Mheshimiwa Zahoro Juma Khamis na Mheshimiwa Benardeta Gambishi. (*Makofi*)

Pia wapo Kaimu Katibu wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Mama Mary Masey, Mwenyekiti wa Tume ya Kurekebisha Sheria, Mheshimiwa Profesa Ibrahimu Juma; Waheshimiwa Makamishna wa Tume ya Kurekebisha Sheria, Mheshimiwa Jaji Edward Mwesumo na Mheshimiwa William Mdundo, Kaimu Katibu wa Tume ya Kurekebisha Sheria, Bi Angela Bahati; kwa kweli kwa uwakilishi wa kijinsia Wizara hii inaonyesha njia na ni vizuri sana Wizara ya Sheria yenye kufuata Katiba na Sheria. (*Makofi/Kicheko*)

Vilevile, wapo Mkurugenzi wa Mashtaka Bwana Elieza Mbuki, huyu ndiye Mkurugenzi wa Mashtaka Bwana Elieza Mbuki nadhani ina jina lingine, yule Fereshi ndiye Mkurugenzi, huyu nadhani mwakilishi wake. Mkurugenzi wa Sera na Mipango Bi. Christina Sonyi, Kaimu Mwandishi Mkuu wa Sheria Bi. Esther Manyesha, bado anakaimu tu, ehee! Haya!

Vilevile kuna Kaimu Mkurugenzi wa Katiba na Haki za Binadamu Bwana Mathew Mwaimu, Kaimu Mkurugenzi wa Utawala Bi. Diodata Makani, Mkurugenzi Msaidia wa Madai, Bwana Abraham Semvuji, Mkurugenzi Msaidizi wa Sheria za Kimataifa Bwana Julius Maraba, Kaimu Afisa Mtendaji wa *RITA* Bwana Phillip Saliboko, Mratibu wa *Program* ya Maboresho ya Sekta ya Sheria, Bwana Venalis Motete. Hao ndiyo wageni wa Mheshimiwa Waziri katika siku yake ya kuwasilisha hotuba yake. Kumbe kuna wengine wameongezeka hapa, yupo Ndugu Eddy Fusi, Naibu Mkurugenzi na Mama Manongi Mhasibu Mkuu, Ndugu M. G. Mzuna wameandika hapa *PRM Incharge* na Ndugu T.K. Simba *DRM Incharge*. Karibuni sana wageni wetu kutoka sekta ya Katiba na Sheria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Waziri Captain John Chiligati ana wageni wawili amba ni Bwana Mohammed *Oais*, Mwenyekiti Mtendaji wa Kampuni ya *COSMOS* na Bwana Vinesh, Patel Afisa kutoka Kampuni ya *COSMOS Group*. Hatukuelezwu zaidi kampuni hii na maudhui yake lakini nahisi wanatoka nje. *You are warmly welcome to Dodoma and especially to the Chamber, we are happy to see business leaders who are doing business with us in Tanzania to visit us in the Parliament. Thank you.* (*Makofi*)

Mheshimiwa Ephraim Madeje - Mbunge wa Dodoma Mjini, ana wageni wake pia amba ni Ndugu Jumanne Ndege, Diwani kutoka Kata ya Chamwino, akiwa

ameambatana na Mabalozi hamsini wa CCM wa Kata ya Chamwino. Ahsante sana wenyeji wetu, Chamwino sio mbali sana na najua kuna sehemu kadhaa za burudani ambazo Waheshimiwa Wabunge huwa mnawakaribisha huko, mwendelee na ukarimu huo huo. (*Makofi*)

Wageni wa Mheshimiwa Suleiman Ahmed Sadiq ni wanafunzi 65 na walimu watano kutoka shule ya msingi ya Mtibwa Morogoro, sijui wako hapa! Nadhani wapo katika ule ukumbi mwingine pale *basement*.

Wapo wanafunzi thelathini kutoka shule ya msingi Santhome walioambatana na walimu wao. Nao nadhani wapo *basement*.

Wapo wanafunzi 50 kutoka Shule ya Msingi Kizota walioambatana na walimu wao. Ahsante sana vijana na walimu, tunawatachia mema katika masomo yenu na walimu mwendelee kufanya kazi kwa bidii, tisisikie mambo ya migomo migomo, hayatusaidii, mtakuwa mnatuadhibu wananchi bure.

Wapo wanafunzi thelathini kutoka Chuo cha Mafunzo ya Ufundu na pia wapo wanafunzi thelathini na tatu kutoka shule ya msingi ya Mtakatifu Margareth walioambatana na walimu wao. Hawa wana sare nadhifu sana, watoto wa Mtakatifu Margareth. Karibu sana tunawatachia mema, nayo haitajwi ni wapi sijui ni Dodoma au sijui ni wapi. Tunashukuru sana, karibuni na tunawaombea mema. (*Makofi*)

Sasa ni matangazo ya kazi. Kwanza Waheshimiwa Wabunge niwakumbushe tu nimemtaka Katibu wa Bunge awasambazieni utaratibu wa wageni, tumeanza kuwa tunapata wageni wengi sana kwa ghafla, sasa taarifa zinatakiwa, kama mnaleta wageni 50 mathalan, tukijua siku hiyo hiyo inakuwa ni vigumu sana kuweza kuwasaidia, kwa hiyo, kuna mawasiliano yanahitajika. Kwa hiyo, Herman Berege, Msaidizi wa Katibu atasambaza katika visanduku vyetu vya barua tuupate vizuri utaratibu wa wageni ili tupunguze usumbufu kwao na fadhaa kwa Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa William Shellukindo, Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini anawaita wanakamati wake leo saa tano asubuhi katika Ukumbi Na. 231.

Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa (*LAAC*), leo saa tano asubuhi anahitaji wajumbe wote wa Kamati hiyo wakutane katika Ukumbi Na. 219.

Mheshimiwa Elieta Switi, Katibu wa *TWPG*, Chama cha Wabunge Wanawake katika Bunge letu anahitaji leo saa saba mchana wanawake wote wanachama wa chama hicho wakutane katika Ukumbi wa Pius Msekwa.

Waheshimiwa Wabunge, nimepokea salaam nyingi sana za hongera kwa kuwawasilisha kule Malaysia na kupewa heshima ya kuwa Rais wa *CPA*. Kilichopewa heshima hiyo ni nchi yetu, mimi nimetokea tu kwa bahati kuwa ndiyo Spika kwa wakati huu. Kwa hiyo, nashukuru kwamba jina la nchi yetu ni kubwa na kila jitihada zifanyike

kuweza kuhifadhi sifa hiyo ya nchi yetu. Hawezi kuchaguliwa mtu katika nafasi hizi akiwa anatoka nchi yenye vita ya wenyewe kwa wenyewe au Serikali haifanyi kazi vizuri au hali ya ovyo ovyo tu. Kwa hiyo, hii ni sifa ya nchi yetu na napenda nitamke wafuatao tuliokuwa nao kule Kuala Lumpa, Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni, Mheshimiwa Job Ndugai, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mheshimiwa Zainab Vullu, Mheshimiwa Tatu Ntimizi na Mheshimiwa Pindi Chana. Walifanya kazi nzuri sana na kubwa na imetusaidia sasa kuwa sisi ndiyo wenyehi wa Mkutano Mkuu wa Chama cha Jumuiya ya Madola ambaa utafanyika Arusha tarehe 21 – 29 Septemba, 2009. Nimekaa huko siku nane kwa sababu ya mambo haya ya uchaguzi. Kwa hiyo, nilipenda mjue kwamba nimewa-miss sana. (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, nilipata faida moja nikiwa kule nayo ni kwamba, kuna Wabunge wawili walinikabili wakasema, wameona siku ambayo humu ndani ya Bunge kuna changamoto kuna viatu fulani vimechakaa chakaa, huwa ndiyo navaa. Sasa nikashangaa kumbe, nilidhani sisi *Presiding Officers* mnatuangalia tu juu juu kumbe mnaangalia mpaka viatu. Nikawaambia wala haifuatani na hivyo, viatu vya zamani unakuwa umevizoea, kwa kuwa unakaa muda mrefu, basi ndiyo hivyo lakini haiambatani na imani yoyote, ni jambo la kawaida tu.

Waheshimiwa Wabunge, hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria imepatwa na matatizo ya usafiri, ilivyochapishwa kule Dar es Salaam kufika hapa imechelewa kidogo lakini nahakikishiwa kwamba mnamo saa tano itakuwa imefika hapa. Kwa hiyo, wakati Waziri anaisoma tutakuwa tumepokea nakala za kitabu cha hotuba. Kwa hiyo, niliona ni vema mfahamu hilo kwa sababu naona zimekwishagawiwa hotuba za maoni ya Kamati na ya Kambi ya Upinzani kabla ya hotuba yenyewe lakini hotuba aliyoiweka Mezani Mheshimiwa Waziri ni hii hapa, Spika ameipokea na kwa kanuni ni sahihi kabisa. Nadhani vitabu vya hotuba vimekwishafika na mttagawiwa wakati Mheshimiwa Waziri anasoma. Ahsanteni sana.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009 - Wizara ya Katiba na Sheria

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea, kujadili na kuitisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Umoja wa Nchi za Afrika. Kuteuliwa kwake kumedhihirisha imani kubwa waliyonayo viongozi wa nchi za Afrika kwake binafsi na Taifa letu kwa ujumla. Pia, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kufanikisha Mkutano wa *Leon Sullivan* uliofanyika Arusha mwezi

Juni, 2008 ambao umeweza kuwakutanisha wafanyabiashara wa Tanzania na wale wa Marekani kwa lengo kuu la kukuza uwekezaji katika sekta mbalimbali za maendeleo ya kijamii na kiuchumi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru tena kwa namna ya pekee Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete - Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa imani aliyioonesha juu yangu na heshima kubwa aliyonipa kwa kunateua kuongoza Wizara hii nyeti ya Katiba na Sheria. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Rais na Watanzania wote kwa ujumla kwamba nitajitahidi kwa uwezo wangu wote kuhakikisha kuwa nafanikisha malengo ya Wizara hii na ya Taifa kwa ujumla.

Aidha, naendelea kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo langu la Nachingwea kwa kuendelea kunipa ushirikiano mkubwa. Nafahamu wangependa sana niwe nao kwa muda mrefu zaidi kuliko ilivyo hivi sasa lakini naamini wanayaelewa majukumu ya Kitaifa yanayonikabili. Napenda niwahakikishie kuwa tupo wote katika kuleta maendeleo ya Wilaya yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda - Mbunge wa Mpanda Mashariki kwa kuteuliwa kwake na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hatimaye kupitishwa kwa kura nyingi na Bunge hili Tukufu kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Napenda pia kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wenzangu waliopewa nyadhifa za kuongoza Wizara mbalimbali katika Serikali hii ya Awamu ya Nne. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda nichukue nafasi hii pia kukupongeza wewe kwa kuchaguliwa kwako kuwa Rais wa CPA. Hii ni heshima kubwa sana kwako, kwa Bunge hili a kwa nchi yetu. Nawapongeza pia na Waheshimiwa Wabunge ambaو uliongozana nao waliosaidia kufanikisha hayo. Hongereni sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Benedict Ngalamu Ole-Nang'oro kwa kuchaguliwa kwake kuwa Mbunge wa Jimbo la Kiteto (CCM). Ushindi aliopata ni ishara tosha ya imani kubwa waliyonayo wananchi kwa Chama cha Mapinduzi na kwake binafsi. Aidha, nawapongeza Waheshimiwa Al-Shymaa Kwegyir na Mchungaji Dr. Getrude Lwakatare kwa kuteuliwa kuwa Wabunge.

Aidha, napenda pia kumpongeza Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala kwa kuchaguliwa kushiriki kwenye Kamati hii. Napenda kuishukuru kwa dhati Kamati hii chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa George Malima Lubeleje - Mbunge wa Mpwapwa kwa maoni na ushauri wao. Maoni hayo yamesaidia sana kuboresha Makadirio ya Bajeti ya Wizara yangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kutoa pongezi za pekee na kuwashukuru kwa dhati Mawaziri waliotangulia kuwasilisha hoja zao hapa Bungeni, hususan Waziri Mkuu - Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda - Mbunge wa

Mpanda Mashariki na Waziri wa Fedha na Uchumi -Mheshimiwa Mustafa Mkulo - Mbunge wa Jimbo la Kilosa kwa hotuba zao nzuri ambazo zimetoa mwelekeo wa ujumla katika masuala ya Mipango, Uchumi, Mapato na Matumizi na shughuli za Serikali kwa kipindi kijacho cha mwaka wa fedha 2008/2009.

Aidha, napenda niwashukuru Waheshimiwa Wabunge waliochangia Hotuba za Mawaziri waliotangulia. Maoni na Ushauri wao huo utasaidia sana kuboresha mipango ya Serikali katika sekta mbalimbali ikiwemo Wizara ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kuitia Bunge lako Tukufu kumpongeza Mheshimiwa Jaji Salum Massati aliyeulewa na Mheshimiwa Rais hivi karibuni kuwa Jaji Kiongozi wa Mahakama Kuu na Waheshimiwa Majaji wapya wanenye wa Mahakama ya Rufaa na 11 wa Mahakama Kuu. Aidha, nampongeza Mwenyekiti mpya wa Tume ya Haki za Binadamu pamoja na Waheshimiwa Makamishna sita na wasaidizi wao wawili wa Tume hiyo kwa kuteuliwa kwao kushika nyadhifa walizopewa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2007/2008, nchi yetu ilishuhudia matukio mbalimbali ya ajali za vyombo vya usafiri na kufunikwa kwa wananchi katika mashimo ya *Tanzanite* huko Mererani, Arusha. Ajali hizo zilisababisha vifo vya wananchi wengi na kifo cha ajali ya gari kwa aliyekuwa Naibu Waziri wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto na Mbunge wa Viti Maalum - Hayati Salome Mbatia. Aidha, Bunge hili pia lilipoteza Mbunge mwenzetu aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kiteto - Hayati Benedict Losurutia na hivi majuzi tumempoteza Mbunge mwenzetu Mheshimiwa Chacha Zakayo Wangwe aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Tarime. Kwa masikitiko makubwa, napenda kutoa pole na salamu zangu za rambirambi kwa familia zote zilizopoteza ndugu, jamaa na marafiki zao katika matukio yote haya. Mungu azilaze pema peponi roho za Marehemu hao, Amina.

Mwisho kabisa, napenda kumshukuru kwa dhati kabisa Mheshimiwa Jaji Mkuu wa Mahakama ya Rufaa Tanzania kwa kukubali kuhudhuria Kikao hiki cha Bunge leo hii.

Mheshimiwa Spika, hii ni mara ya kwanza kabisa katika historia ya nchi yetu kwa Kiongozi wa Muhimili wa Mahakama kuhudhuria Kikao cha Bunge lako Tukufu. Namshukuru sana Jaji Mkuu pamoja na Majaji wote walohudhuria leo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa Maelekezo Mbalimbali ya Serikali, Maelekezo ya Ilani ya CCM 2005. Suala la kuundwa au kutokuundwa kwa Mahakama ya Kadhi ndani ya mfumo wa Mahakama ya Tanzania limezungumzwa sana nje na ndani ya Bunge lako Tukufu. Ndani ya Bunge, suala hili lilianza kuzungumzwa na Mheshimiwa Mikidadi, ndani ya *LEGCO* mwaka 1958. Mheshimiwa Mikidadi alikuwa akidai uanzishwaji rasmi wa Mahakama ya Kadhi. Wakati huo Utawala wa Waingereza nchini Tanganyika ulikuwa ukijadili namna bora ya kuleta ufanisi katika Mahakama ya Waafrika (*Native Courts*), hususan namna ya kutenganisha shughuli za kiutawala kutoka shughuli za utoaji wa haki katika ngazi za Mahakama za Waafrika.

Mheshimiwa Spika, katika Mabunge ya kuanzia 1995-2000, 2000-2005 na hili la sasa, suala la uanzishwaji wa Mahakama ya Kadhi limekuwa likiibuliwa na Waheshimiwa Wabunge mbalimbali. Serikali imekuwa makini katika kuzingatia hoja hizi na kutokutoa uamuzi wa haraka kwa sababu suala lenyewe linahitaji kutafakariwa kwa makini ili kuchelea kuibua hisia za kidini na kuligawa Taifa

Mheshimiwa Spika, wakati akijibu hoja za Waheshimiwa Wabunge Manju Msambya, Hasan Rajab Khatib, Juma Suleiman N'hunga na Mohamed Hamis Missanga pamoja na Shoka Hamisi Juma, Mheshimiwa Waziri Mkuu alizungumzia kwa kirefu na kwa kina sana jambo hili. Nitakuwa ni mtovu wa nidhamu na mfujaji wa muda nikianza kuyarejea yote aliyojasema Mheshimiwa Waziri Mkuu. Mheshimiwa Waziri Mkuu kama kiongozi wa Serikali amekwishatoa mwelekeo wa kufikia tamati kuhusu jambo hili.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, niruhusu, nirejee moja tu kutoka katika yale aliyojasema. Mheshimiwa Waziri Mkuu alisema kwamba, jambo hili sasa lipo kwenye Tume ya Kurekebisha Sheria likifanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, sasa napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Tume ya Kurekebisha Sheria sasa imekamilisha utafiti wake na tayari imewasilisha taarifa na mapendekezo yake Serikalini kwa Mujibu wa Sheria. Hivi sasa Serikali inaitafakari sana taarifa hiyo kabla ya kufanya maamuzi. Bunge lako Tukufu litafahamishwa uamuzi wa Serikali mara tu utakapotolewa.

Mheshimiwa Spika, nafurahi kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba Serikali tayari imeanza kutekeleza mpango wa kuwa na ofisi za Mahakama Kuu katika kila Mkao. Kwa kuanzia Kanda mpya za Mahakama Kuu, Iringa na Sumbawanga zimeanzishwa. Vile vile, taratibu za awali za ujenzi wa jengo la Mahakama Kuu kanda ya Shinyanga zimekamilika kwa kumpata mkandarasi wa kazi hiyo na ujenzi umekwishaanza. Aidha, Mikoa mingine inayohusika na mpango huo ni Kigoma, Mara, Lindi, Morogoro, Pwani, Singida, Dodoma na Manyara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na utekelezaji mpango wa kuanzisha Kanda za Mahakama Kuu kwa kila Mkao Serikali imeendelea kuimarisha mazingira ya utendaji kazi katika Mahakama zote hapa nchini kwa kununua vifaa vya ofisi na vyombo vya usafiri. Jumla ya magari 52 yamenunuliwa kati ya mwaka 2005 hadi 2007 na kupelekwa Wilayani kwa ajili ya ukaguzi wa Mahakama za Mwanzo. Halikadhalika, ujenzi wa jengo la Mahakama ya Rufani Dar es Salaam, Mahakama Kuu ya Bukoba, Mahakama ya Hakimu Mkazi Babati na Mahakama ya Wilaya Mpwapwa utakamilishwa. Ujenzi wa Mahakama ya Wilaya Bunda umesimama kutokana na Mkandarasi kutokizingatia vigezo vya ubora wa kazi hivyo kuilazimu Mahakama kumsimamisha. Jambo hili likishapata utatuzi, basi ujenzi wa Mahakama hiyo utaendelea.

Mheshimiwa Spika, kuhusu marekebiso mbalimbali ya Sheria hususan zinazowakandamiza wanawake, Serikali, kuitia Tume ya Kurekebisha Sheria, imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuzitazama upya sheria hizi, kwa mfano, Sheria ya Mirathi na Sheria ya

Ndoa. Tume ya Kurekebisha Sheria ilifanya tafiti na imetoa mapendekezo yake kwa Serikali.

Halikadhalika, Serikali katika kuchambua mapendekezo haya imebaini kuwa Sheria hizi zinagusa maeneo muhimu mawili, eneo linalohusu mahusiano ya kijamii na kiutamaduni kwa kuzihusisha mila, desturi na imani za watu na kwa upande mwingine sheria hizi zinahusisha maendeleo ya kijamii katika dunia ya sasa. Kwa kuwa maeneo yote hayo mawili ni nyeti na muhimu, Serikali imeamua kuchukua hatua za awali za kuandaa Waraka unaolenga kuwashirikisha wananchi walio wengi zaidi kwa kuwapa fursa ya kuweza kutoa maoni yao kwa uhuru na uwazi kabisa, kabla ya marekebisho hayo kufanywa kwenye sheria hizi husika. Aidha, zoezi la kukamilisha Waraka wa Serikali unaoendana na kukusanya maoni ya wananchi na taasisi mbalimbali, utakamilishwa ndani ya mwaka huu wa fedha wa 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, katika kulinda maslahi na haki za watoto, Serikali imezipitia kwa kina sheria zote zinazohusu watoto na kuona kuwa, ingawa zipo nyingi, kila moja ya sheria hizi ni muhimu katika eneo lake na hivyo, sio vyema kuzifuta na kutunga sheria moja ya watoto. Hivyo, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara Elimu na Mafunzo ya Ufundı, Wizara ya Maendeleoya Jamii, Jinsia na Watoto na Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, inaandaa marekebisho ya sheria zote zinazohusu mtoto ili yaletwe ndani ya Bunge lako Tukufu haraka iwezekanavyo.

Sheria tulizoziangalia ni ile *the Education Act, the Penal Code, the Criminal Procedure Code, the Employment and Labour Relations Act, the Law of Marriage Act, the Adoption Act* na *the Affiliation Act*. Marekebisho haya yanafanywa katika msingi wa ustawi wa mtoto yaani tunazingatia *the welfare principle*. Serikali inakusudia kufanya marekebisho ya Sheria hizo kwa kuzingatia mapendekezo yaliyotolewa na Tume ya Kurekebisha Sheria pamoja na wadau mbalimbali. Aidha, mchakato wa kuboresha sheria hizi umekwishaanza na marekebisho yanatarajiwa kuwasilishwa Bungeni katika mwaka huu wa fedha wa 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, marekebisho ya sheria nyingine zinazokandamiza jamii na ambazo zimepitwa na wakati bado zinaendelea kufanyiwa tafiti kupitia Tume ya Kurekebisha Sheria. Aidha, Tume ipo katika hatua mbalimbali za tafiti za sheria zinazohusu Mila (*Customary Law*), Sheria za Kutetea Haki za Watu Wenye Ulemavu (*Disability Law*), Sheria ya Ushindani wa Haki katika Biashara (*Fair Competition*), Sheria inayolinda ugunduzi na uhamishaji wa Teknolojia; (*Industrial Property and Transfer of Technology*), Sheria ya adhabu ya kifo, viboko na vifungo vya muda mrefu (*Capital Punishment, Corporal Punishment and Long Sentences in Tanzania*).

Sheria ya Makosa ya Kujamiiana [*Sexual Offences - Special Provision*) Act No. 4 of 1998]. Mfumo wa kiraia wa Mahakama (*Civil Justice Review*), Sheria ya Maadili ya Viongozi (*Public Leadership Code of Ethics Act 1995*); na mfumo wa kisheria kwa kutumia utaalam wa vinasaba vya binadamu nchini Tanzania (*DNA*). (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kiliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii italeta Muswada wa Sheria unaohusu *DNA* ndani ya Bunge lako Tukufu wakati wowote kuanzia sasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Tume ya Kurekebisha Sheria pamoja na kufanya tafiti bado imeendelea kutoa elimu ya sheria kwa jamii kwa njia mbalimbali kwa kutumia vyombo vyaa habari na vijarida ili kuwapatia wananchi uelewa mpana kuhusu maboresho ya sheria hapa nchini. Aidha, natoa wito kwa wananchi kuendelea kuipa Tume msaada wa kutosha katika zoezi la kuboresha mfumo wa huduma za kisheria hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2007/2008, Miswada 34 imeandaliwa na Miswada 23 ilipitishwa na Bunge na kuwa sheria na Sheria 17 zilitiwa saini na Mheshimiwa Rais ili kuwa sheria. Kati ya sheria zilizopitishwa, sheria 12 zilifanyiwa marekebisco. Sheria ya Hifadhi ya Mazingira, Sura ya 191, ilitafsiriwa kutoka lugha ya Kiingereza kwenda Kiswahili na Katiba ya nchi imetafsiriwa kutoka lugha ya Kiswahili kwenda Kiingereza. Sheria Ndogo 422 ikiwa pamoja na Hati za Serikali, zimeandikwa au kuhakikiwa na baadaye kuchapishwa katika Gazeti la Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kuanzisha Mfumo wa Kuwasaidia Wananchi Wasiojiweza Kupata Msaada wa Kisheria. Mabadiliko ya muundo mpya wa Wizara yaliyofanywa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hivi karibuni yatawezesha Wizara yangu kuanza kutoa msaada wa kisheria kwa wananchi wanaohitaji baada ya kuanzishwa kwa Idara mpya ndani ya Wizara inayoshughulikia malalamiko mbalimbali ya kisheria kutoka kwa wananchi na taasisi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kuweka mfumo utakaowezesha kutumika kwa wanasheria wa awali katika Mahakama za Mwanzo. Tume ya Kurekebisha Sheria tayari imekwisha kamilisha utafiti kuhusu matumizi ya wanasheria wa awali (*paralegals*) katika Mahakama za Mwanzo na kuwasilisha ripoti yao Wizarani. Wizara tunaliangalia hili pamoja na uwezekano wa kutumia wanasheria wahitimu wa shahada (*Graduates*) katika Mahakama hizi kama mahakimu. Kwa vyovypole vile uamuzi utakaotolewa utakidhi maelekezo ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya kutoa huduma kwa wananchi wengi kadri inavyowezekana.

Mheshimiwa Spika, naomba kupitia Bunge lako Tukufu nitoe taarifa ya utekelezaji wa maelekezo ya Mheshimiwa Rais alipotembelea Wizara yangu mwezi Februari 2006. Katika kuhakiksha kuwa Haki inatolewa kwa usawa hapa nchini, tumechukua hatua mbalimbali ikiwemo kuongeza uwezo wa Mahakama ya Rufani kuendesha vikao vyake toka vikao vitatu badala ya viwili kutokana na kuongezeka kwa idadi ya Majaji walioteuliwa hivi karibuni. Idadi ya Majaji 34 walioteuliwa, kati yao Majaji wanne ni wa Mahakama ya Rufani na wengine 30 ni wa Mahakama Kuu ambao walipangia kazi katika Mahakama mbalimbali zikiwemo za vitengo vya Mahakama ya Biashara, Mahakama ya Ardhi na Mahakama ya Kazi. Pia wameajiriwa Mahakimu Wakazi 95 na Mahakimu 128 wa Mahakama za Mwanzo.

Aidha, vikao vya kusikiliza kesi vimeongezeka tofauti na ilivyo kuwa hapo awali. Hatua hii itasadida sana kuongeza kasi ya usikilizaji wa kesi na hivyo kupunguza mlundikano wa kesi katika Mahakama za ngazi zote.

Mheshimiwa Spika, hatua nyingine nyingi zilizochukuliwa ni pamoja na kutumia vyombo vya habari kama redio, luninga na vipeperushi vinavyoelimisha wananchi juu ya haki zao na sheria zake. Aidha, kwa kushirikiana na vyombo vingine vya kutoa sheria, tumefanya marejeo ya sheria mbalimbali ikiwemo Sheria mpya ya Rushwa iliyoanza kutumika tarehe 1 Julai, 2007. Ukaguzi wa mara kwa mara umeimarishwa katika kanda za Mahakama na Mahakama za Mwanzo kwa ratiba ya miezi mitatu mitatu. Vilevile, Kamati za maadili katika ngazi ya Mikoa na Wilaya zinazoshughulikia malalamiko dhidi ya Mahakimu zimekuwa zikikutana na kuchukua hatua zinazostahili kwa wale wanaokiuka.

Mheshimiwa Spika, katika kuondokana na tatizo la haki kuchelewa kutendeka kwa kesi kuchukukua muda mrefu sana Mahakamani, aidha kwa sababu ya upelelezi, Wizara imechukua hatua ya kutenganisha jukumu la upelelezi na mashtaka. Lengo ni kuhakikisha kesi zinakamilishwa kwa haraka na kwa ufanisi. Utaratibu huu utaanzia katika Mikoa sita ya Arusha, Dar es Salaam, Mwanza, Ruvuma, Shinyanga na Tanga na utahusisha jumla ya Wilaya 24.

Mheshimiwa Spika, ili kuondokana na tatizo la Mahakimu kukaa muda mrefu sana katika sehemu moja, hasa kule kijiji, Jumla ya Mahakimu Wakazi 87 na Mahakimu 100 wa Mahakama za Mwanzo wamehamishwa kwa kubadilishwa vituo vyao vya kazi. Jukumu hili litaendelea kutekelezwa kadri ya uwezo wa fedha utakavyoruhusu.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha utoaji wa ushauri wa kisheria hasa kwenye mikataba, Muundo wa Wizara umepitiwa upya na kutenganisha kazi za Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na zile kazi za Wizara. Natumai utekelezaji wa muundo huu mpya uliopitishwa tarehe 4 Aprili, 2008 na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano utasaidia sana kuboresha eneo hili la utoaji wa ushauri wa kisheria kwenye mikataba. Vilevile, tunatarajia kupata msaada wa kifedha utakaowezesha wanasheria wetu kupatiwa mafunzo mbalimbali ya kuwajengea uwezo yakiwemo yale ya utaalamu wa kuandaa, kujadili, kutafsiri na kuchambua mikataba ambayo Serikali itakuwa inaitekeleza.

Mheshimiwa Spika, hali ya utendaji kazi katika Wizara na changamoto zilizopo. Uhuru wa Utoaji Haki kwa Mahakama zetu. Wizara imeendelea kuimarika katika kusimamia suala la uhuru wa utoaji haki kwa Mahakama zetu. Hata hivyo, Mahakama kama muhimili mmojawapo wa Dola umekuwa ukipewa msukumo mkubwa na Serikali bila kuingiliwa katika maamuzi yake tofauti na inavyotafsiriwa kuwa maamuzi yake yamekuwa yakitokana na matakwa ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, hali hii sio kweli kabisa kama ilivyowahi kusemwa na Mheshimiwa Mstaafu Jaji Joseph Masanche katika hotuba yake ya kustaafu ya tarehe 27 Juni, 08. Nanakuu “*throughout my career in the judiciary, I never got influenced by the*

executive, and I commend them for that. Tanzania judiciary is one of the most independent judiciaries in Africa, it is my conviction.” Usemi huu una maana ya kwamba katika utumishi wake wote Mheshimiwa Joseph Masanche hajawahi kuelekezwa au kushawishiwa na watendaji wa Serikali kutoa maamuzi wanayoyataka. Hivyo, namshukuru kwa hilo. Pia Mahakama ya Tanzania ni Mahakama pekee katika Afrika iliyo na uhuru kamili wa kutoa maamuzi yake bila kupata ushawishi toka kwa watendaji wa Serikali. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, bado kumekuwepo na changamoto mbalimbali zinazokabili uendeshaji wa Mahakama zetu. Hata hivyo, Serikali imeendelea na jitihada za kuongeza Watendaji katika Mahakama kwa kuteua Majaji zaidi, kuajiri Mahakimu wa Wilaya na Mikoa, Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo, Mawakili wa Serikali na Watumishi wa kada nyingine na kuwapatia vitendea kazi. Pia, umekuwepo ushirikiano wa kuridhisha kwa Mahakama zetu kutenda kazi zake kwa uhuru zaidi bila kuathiri utendaji wa Serikali au wa Mahakama yenyewe.

Mheshimiwa Spika, Kukuza, Kulinda na kuhifadhi Haki za Binadamu na Utawala Bora katika Jamii. Katika kuboresha huduma za kulinda na kuhifadhi haki za binadamu katika jamii, Serikali imeendelea kujenga jamii ya watu inayozingatia haki na utamaduni ambamo haki na misingi ya utawala bora inakuzwa, inazingatiwa, inatekelezwa na inahifadhiwa.

Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora imekuwa inahamasisha umma kuhusu hifadhi ya haki za binadamu na wajibu kwa jamii kwa mujibu wa Katiba na Sheria za nchi; kupokea na kuchunguza malalamiko ya uvunjwaji wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora. Halikadhalika, Tume inaanisha upungufu wa sheria kwa kufanya tafiti, kutoa na kueneza elimu kwa umma kuhusu haki za binadamu na misingi ya utawala bora. Aidha, Tume imekuwa inapitia Miswada/sheria mbalimbali kwa lengo la kuainisha mapungufu yanayohusiana na haki za binadamu na misingi ya utawala bora na kuishauri Serikali. Katika kufanya hivyo, tutakuwa tunadumisha amani, haki na utulivu wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2007/2008 Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ilijiwekea lengo la kushughulikia asilimia 80 ya malalamiko yote yaliyopokelewa. Hadi kufikia mwezi Juni, 2008, Tume ilikuwa imepokea jumla ya malalamiko 10,324. Kati ya malalamiko hayo, mapya yalikuwa 2,660 na malalamiko ya zamani ambayo yalitokana na Tume ya PCB yalikuwa 7,664. Aidha, malalamiko 10,017 yalipokelewa na Ofisi za Tume Tanzania Bara na malalamiko 307 yalipokelewa na Ofisi za Tume kule Zanzibar. Jumla ya malalamiko 2,372 yalihitimishwa sawa na asilimia 23, ambapo malalamiko 2,285 yalihitimishwa na Ofisi za Tume Tanzania Bara ambayo ni sawa na asilimia 23 na malalamiko 87 yalihitimishwa na Ofisi za Tume Zanzibar ambayo ni sawa na asilimia 28.3.

Mheshimiwa Spika, miadhara ilifanyika katika Wilaya 24 za Tanzania Bara, Mikoa mitano na Wilaya zote 10 za Unguja na Pemba kwa lengo la kutoa elimu kwa umma kuhusu haki za binadamu na misingi ya utawala bora. Mikutano mingine ya kuelimisha

wananchi kuhusu uhusiano kati ya Hifadhi za Taifa na Mbuga za Wanyama na vijiji vinavyopakana na sehemu hizo ilifanyika kwa wafanyakazi katika Hifadhi za Taifa, mbuga za wanyama na wakazi wa sehemu zinazopakana na mbuga na hifadhi hizo katika Wilaya 19 za Tanzania Bara. Tume ilifanya pia mikutano ya hadhara kati ya viongozi na wananchi katika Mikoa mitano na Wilaya zote 10 za Unguja na Pemba.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza jukumu lake la kukagua sehemu wanamohifadhiwa watu kwa mujibu wa sheria, kwa nia ya kutoa mapendekezo kuhusu hali ya haki za binadamu na utawala bora, Tume ilikagua vituo vya polisi 31, Tanzania Bara 5 na 26 Zanzibar. Aidha, Magereza na vyuo vya mafunzo 14 vilikaguliwa. Tanzania Bara Magereza tatu na Zanzibar vyuo 11 vya mafunzo vilikaguliwa. Taarifa zinazolezea kero za askari, wafungwa na mahabusu na mapendekezo ya kuboresha sehemu hizo zilitolewa.

Aidha, Tume imefanya utafiti Tanzania Zanzibar juu ya utekelezaji wa haki za watoto katika Mikoa mitano ambapo Wilaya sita zililusika na utafiti huu. Tume vile vile imetoa mafunzo kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii wa Halmashauri na Asasi zisizo za Kiserikali katika Kanda ya Ziwa juu ya ufuutiliaji katika kulishughulikia tatizo la wananchi kutoa taarifa za uvunjwaji wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora. Vipeperushi 34,250 kuhusu kuitangaza na kuifahamu Tume, mabango 1,068 kuhusu haki za mahabusu, majorida 4,969 na vijitabu vya "Mwananchi Tambua Haki Yako" 3,566 vinavyoorodhesha haki za binadamu zilizotajwa ndani ya Katiba, viligawiwa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na malalamiko ya wananchi na mapendekezo ya Waheshimiwa Wabunge, Tume ilitembelea Hifadhi za Taifa na mbuga za wanyama 10 katika Mikoa saba na Wilaya 20 za Tanzania Bara kwa makusudi makuu matatu: Kutoa elimu ya awali ya haki za binadamu kwa wananchi wa vijiji vinavyozunguka hifadhi na mbuga hizo ambao wako katika mazingira ya kipekee; kuona uhusiano kati ya wananchi wa vijiji na vitongoji vinavyozunguka hifadhi hizo na wafanyakazi wa hifadhi na kusikiliza kero za wananchi na kuzishughulikia. Changamoto iliyopo katika eneo hili ni kuendelea kuongeza idadi ya vituo na kuajiri wataalamu wa kutosha na wenyewe ujuzi ili waweze kusimamia suala la utoaji wa haki za binadamu na utawala bora katika jamii kwa kuwafikia wananchi wengi zaidi na kwa wakati. Pia, kutoa mafunzo ya awali juu ya uchambuzi wa malalamiko kwa maofisa uchunguzi wote kwa kutumia mfumo wa kompyuta na watumishi wa kada mbalimbali katika ngazi mbalimbali za elimu.

Mheshimiwa Spika, Tume itaendelea kufanya tafiti na kutoa taarifa juu ya Haki za watu wenyewe ulemavu wa ubongo (*Mentally Challenged*) pamoja na matatizo ya mimba za utoton. Tume pia imepanga kufungua Ofisi ya Tawi huko Pemba.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kwa hivi karibuni imekuwa ikipata changamoto mbalimbali za kulalamikiwa juu ya uratibu na utoaji wa mikataba mibovu. Hata hivyo, jitihada za dhati za kutoa mafunzo kwa vitendo kwa Mawakili wa Serikali katika eneo la kujadili na kuandaa Mikataba, hususan, Sekta inayohusu Madini na Nishati, Maliasili, Maji, Mawasiliano, Viwanda, Fedha na Miundombinu pale Bajeti ya

Serikali inaporuhusu yamekuwa yakifanyika kwenye Asasi za kisheria zilizobobea katika masuala ya uandaaji na kujadili mikataba ya aina mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, ukweli bado utabaki kuwa suala la Mikataba huandaliwa na jopo la wataalam mbalimbali wakiwemo Wanasheria, Wachumi, Wahandisi, Wahasibu na kada nyingine kutoka sekta mbalimbali kulingana na mahitaji ya mkataba husika. Hivyo, mafunzo yatakayokuwa yanatolewa pia yatawahusisha wataalamu wa kada hizo katika sekta husika ili kuondoa dhana na kasoro zinazoanza kujitokeza za kudhani kwamba mikataba yote mibovu husababishwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kukosa uwezo kitaaluma wa kujadili na kuandaa mikataba.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudhi hizo zilizokwishaanza kuchukuliwa na Serikali, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliliomba Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (*UNDP*) kusaidia kujenga uwezo wa wataalam wetu, hususan, Wanasheria katika eneo la kujadili na kuandaa mikataba ya uwekezaji nchini. Ninayo heshima kubwa kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Shirika hilo limeridhia ombi la Mheshimiwa Rais na hivi karibuni nchi yetu imeshiriki katika uzinduzi wa mradi wa ujenzi wa uwezo wa kujadili na kuandaa mikataba ya uwekezaji katika nchi tano za Afrika, Tanzania ikiwa mionganoni mwa nchi hizo zilizokutana nchini Liberia na kuwekeana mkataba na *UNDP*. Aidha, mazungumzo ya awali na wataalam wa *UNDP* kuhusu uandaaji na utekelezaji wa mradi huo yamekamilika. Hivi sasa Wizara imekamilisha mapendekezo ya mradi “*Project Proposal*” na kuiwasilisha *UNDP* ili kuanza utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na changamoto ilizokabiliana nazo bado iliendelea kutoa ushauri wa kisheria kwa Serikali na taasisi zake kuhusu masuala ya madai na sheria za kimataifa na mikataba ya biashara. Maombi 268 ya ushauri wa mikataba yalipokelewa, kati ya hayo 217 yalifanyiwa kazi na maombi 51 yaliyobaki yanaendelea kushughulikiwa.

Aidha, Ofisi imekuwa ikishiriki katika majadiliano ya mikataba baina ya Serikali na makampuni, Taasisi na Serikali za nchi nyingine na Jumuiya za Kimataifa na Kikanda, kwa mfano: Jumuiya ya Afrika ya Mashariki (*EAC*) na ile ya Nchi za Kusini mwa Afrika (*SADC*); Umoja wa Afrika (*AU*) na Umoja wa Mataifa (*UN*). Ili kuongeza ufanisi zaidi katika Idara hii ya Uratibu wa Mikataba, Wizara yangu inashauriana na Ofisi ya Rais Utumishi ili kuona uwezekano wa kuunda kitengo mahsusni katika Idara hii ya Uratibu wa Mikataba ambacho kitakuwa na kazi moja tu kubwa ya kushughulikia mikataba tangu pale majadiliano kuhusu mikataba hiyo yanapoanzishwa mpaka kufikia kudhibiti na kusimamia utekelezaji wa mikataba hiyo.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine linalotoa changamoto katika Wizara yangu ni suala la ukamilishaji wa Sera ya Sekta ya Sheria ambayo haikuwahi kuwepo. Kukamilika kwa Sera hii kutatuwezesha kuwa na dira au mwongozo wa sheria zetu tunazoziaandaa na zile tunazozifanyia maboresho. Hata hivyo, kwa sasa tayari tunayo rasimu ilijojadiliwa na Wadau wa Sekta ya Sheria ikiwa ni pamoja na Mawakili wa Serikali na kutolewa maoni. Hatua inayofuatia ni kushirikisha wadau wengi zaidi toka Taasisi mbalimbali, Sekta

binafsi na Vyama vya Hiari ili kupata maoni zaidi kabla ya kuandaa Waraka wa Baraza la Mawaziri. Ni imani yangu kuwa zoezi hili litakamilika ndani ya mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza maelekezo haya ambayo pia ni lengo la ilani ya uchaguzi ya CCM la kuziimarisha na kuziboresha Mahakama zetu, Wizara imekuwa ikishirikisha sekta binafsi pamoja na nguvu za wananchi katika kutoa huduma ya kukarabati na kujenga Mahakama zetu. Jitihada hizi zinazoendelea bado zimekuwa na changamoto kwa baadhi ya Mahakama kuendelea kuwa na ukosefu na uchakavu wa majengo na uhaba wa vitendea kazi. Aidha, kwa kutambua uwepo wa changamoto hizo, Wizara imekuwa ikichukua hatua mbalimbali za kujenga majengo mapya na kukarabati majengo ya zamani kwa Mahakama za ngazi zote hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Mahakama za Mwanzo 28 na Mahakama ya Wilaya ya Hai umekamilika. Halikadhalika, wananchi wameonesha uzalendo zaidi wa kushiriki kikamilifu katika kujenga Mahakama za Mwanzo nane huko Kiomboi-Iramba, Nandembo na Nalasi-Tunduru., Kibutuka- Liwale, Ulaya – Kilosa, Ruanda na Litembo – Mbinga, na Kenya – Serengeti. Ujenzi huu kwa nguvu za wananchi unaendelea katika Mahakama tisa za Iguguno – Iramba, Mkongo – Songea, Robanda – Serengeti, Tingu - Mbambabay, Mbondo- Nachingwea, Kirando, Sopa, Laila na Msanzi – Sumbawanga. Vilevile, ujenzi wa jengo la Mahakama Kuu ya Bukoba na Mahakama Kuu Shinyanga bado unaendelea. Ujenzi wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Manyara na Mahakama ya Wilaya ya Mpwapwa uko katika hatua za kukamilisha majengo.

Aidha, ujenzi wa Mahakama ya Wilaya ya Mafia upo katika hatua za awali na upanuzi wa jengo la muda la Mahakama ya Rufani kwa ajili ya shughuli za Utawala na Uhasibu unaendelea. Majengo ya Mahakama ya Hakimu Mkazi Moshi na Mahakama za Mwanzo 33 nchi nzima yamekarabatiwa.

Mheshimiwa Spika, ukarabati wa jengo kwa ajili ya Masjala ya Divisheni ya Biashara ya Mahakama Kuu Mwanza umekamilika na kupatiwa vifaa muhimu vya huduma za mawasiliano. Uzinduzi wa Masjala hiyo umefanyika na kesi za biashara zimeanza kufunguliwa. Halikadhalika, katika kuimarisha utendaji wa kazi hasa usafiri, Waheshimiwa Majaji wa Mahakama ya Rufani na Mahakama Kuu wamepatiwa magari isipokuwa majaji 11 walioteuliwa hivi karibuni. Aidha, magari 53 yamenunuliwa kwa ajili ya ukaguzi wa Mahakama za Mwanzo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudni zote hizi bado tunahitaji Mahakama nyingi na nzuri zaidi. Ili kufanikisha lengo hili, Wizara yangu inafanya mazungumzo na Ofisi ya Waziri Mkuu ili kuona ni jinsi gani ujenzi wa mahakama na nyumba za Mahakimu unaweza ukaingizwa katika utaratibu wa *D by D* ambapo tuna imani kuwa Halmashauri zetu zinaweza kutekeleza jukumu hili la kujenga Mahakama za Mwanzo hadi za Wilaya na kuiachia Serikali Kuu ujenzi wa Mahakama Kuu peke yake. Kwa upande wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ukarabati wa Ofisi za Kanda za Dar es Salaam na Mwanza unaendelea, ambapo katika Ofisi za kanda za Moshi, Tabora, Shinyanga, Songea na Tanga ukarabati wake umekamilika.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imekuwa mratibu na mtekelezaji wa Programu ya Maboresho ya Sekta ya Sheria hapa nchini. Utekelezaji wa programu hii umekuwa ukihusisha zaidi taasisi 15 zikiwemo Wizara saba, Idara na Taasisi za Serikali na zisizo za kiserikali zinazotoa huduma za kisheria. Aidha, shughuli nyingi za programu hii zimelenga hasa katika kuimarishe uwezo wa utoaji wa huduma za kisheria kwa taasisi zote zinazotekeleza programu hii.

Mheshimiwa Spika, yapo maeneo sita muhimu yaliyoainishwa na programu hii ambayo yanaleta changamoto kubwa kwa Wizara yangu katika kuyaratibu na kuyatekeleza. Mfano, lipo eneo linalolenga katika kuainisha na kuhuisha sheria zinazowezesha kukua kwa sekta ya biashara nchini, sheria zinazozingatia haki kwa wanyonge, utenganishaji na uimarishaji wa shughuli za mashitaka na upelelezi nchini. Eneo hili pia linahusika na uimarishaji wa utafiti wa masuala ya sheria na uboreshaji wa sheria kwa ujumla.

Eneo la pili ni lile linalohusu kutoa haki kwa wasiojiweza na hivyo kuwezesha kupunguza mlundikano wa kesi, kwa kutoa mwongozo ya jinsi ya kuendesha kesi za wanyonge nchini; kutoa mafunzo kwa watumishi wanaohusika na utoaji haki kwa maskini, wanyonge na wasio na uwezo wa kuwakilishwa.

Pia eneo hili linalenga katika kuanzisha kamati za mienendo ya kesi katika Mahakama za Mwanzo na kuziimarishe zile za Mahakama za ngazi za juu. Maboresho katika eneo hili vilevile yanalenga katika kuanzisha mtandao wa msaada wa kisheria nchini, uanzishwaji wa taasisi za kutoa misaada ya kisheria katika Kata, Wilaya, Mikoa na Kitaifa na kutoa mafunzo kwa watu wasio na taaluma ya kisheria yaani wale *Paralegals*.

Mheshimiwa Spika, eneo la tatu la Programu ya Maboresho ya Sekta ya Sheria linahusu kutoa mwongozo utakaozingatiwa na wasimamizi wa utekelezaji wa sheria ya uangalizi wa masuala ya haki za binadamu nchini, utayarishaji na usambazaji wa vijitabu vilivyorahisishwa ili kueleweka kwa haraka na watekelezaji wa masuala ya haki za binadamu. Halikadhalika, eneo hili litashughulikia utayarishaji wa programu ya elimu kwa umma juu ya haki za binadamu.

Eneo lingine la nne linahusu kuimarishe na kujenga uwezo wa kutoa elimu kwa kuanzisha Sekretariati ya kudumu ya Baraza la Elimu ya Sheria, kuanzisha na kuendeleza Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo.

Mheshimiwa Spika, lipo eneo la tano linalohusu kuainisha na kuanzisha mfumo wa kuratibu kwa pamoa masuala ya miundombinu kwa sekta zote za sheria. Maboresho ya Sheria katika eneo hili pia yanahusu kuainisha taratibu zitakazowezesha upatikanaji wa nyumba za Mahakimu, Polisi na Maofisa Magereza. Aidha, eneo hili linahusu uimarishaji wa maktaba za sheria nchini, ukarabati na ujenzi wa mahakama za wilaya, Hakimu Mkazi, Mahakama Kuu, Mahakama ya Rufaa; jengo la Makao Makuu ya Wizara, Ofisi za Kanda na Ofisi zote za msajili wa kisheria. Halikadhalika, eneo la sita

la maboresho haya lipo katika uimarisaji wa taasisi zinazotekeleza programu ya sekta za sheria pamoja na uwezeshaji wa uandaaji wa Sera ya Sekta ya Sheria nchini.

Mheshimiwa Spika, katika kuandika nyaraka mbalimbali za kisheria (*legislative instruments*) ikiwemo Miswada ya Sheria, Sheria ndogo za Halmashauri ya Majiji, Halmashauri ya Manispaa za Wilaya na za Miji, uandishi na usimamizi wa hati mbalimbali za Serikali zikiwemo hati za kuanzisha mamlaka mpya za Serikali kama vile Wakala wa Serikali na Mamlaka zinazojitegemea, changamoto imekuwepo katika kupata wataalamu wa kutosha na wenye ujuzi na uzoefu katika taaluma ya sheria na kada nyingine. Jitihada za kuajiri watumishi wengine 89 wenye sifa na taaluma ya sheria katika mwaka huu wa fedha wa 2008/2009 zitafanyika.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (*RITA*) umeendelea kujiimarisha katika shughuli za usajili wa vizazi na vifo; ndoa na talaka; kusimamia mirathi na ufilisi; kusajili miunganisho ya wadhamini na kusajili watoto wa kuasili. Hata hivyo, uimarisaji wa shughuli zake katika utoaji wa huduma, umekuwa ukikwamishwa na sheria na taratibu mbalimbali zilizokuwa zimepitwa na wakati. Serikali imeendelea na jitihada za kuboresha utaratibu uliokuwa unamlazimisha mtu kwenda kuandikishwa katika Wilaya alikozaliwa. Sasa hivi mtu aliyezaliwa nje ya Wilaya anakoishi anaweza kupata huduma katika Makao Makuu ya Wakala alipo Msajili Mkuu. Utaratibu huu umewarahisishia wananchi wanaotaka huduma ya vyeti kwa matumizi mbalimbali ya ajira, mikopo, kujiunga na masomo au kupata hati za kusafiria.

Mheshimiwa Spika, Wakala umeanzisha mpango wa huduma ya papo kwa papo katika Makao Makuu ya Wakala ambapo huduma inatolewa na kupatikana katika muda wa siku moja hadi tatu tofauti na ilivyokuwa zamani. Aidha, Wakala umeanza kutekeleza mpango wa uboreshaji huduma za usajili katika mfumo wa elektroniki kuitia mradi wa “*Vital Registration Transformation Project*”, utakaoanza kutekelezwa katika Wilaya saba za Bagamoyo, Temeke, Kibaha, Mtwara, Hai, Magu na Makete. Vile vile, punguzo limetolewa kwa gharama ya uchukuaji wa fomu ya maombi ya cheti cha kuzaliwa kwa vizazi vilivyochelewa kuandikishwa ili kuwaondolea kero wananchi.

Mheshimiwa Spika, Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa mwaka 2007/2008 na malengo ya mwaka 2008/2009. Katika mwaka 2007/2008, Wizara kwa kushirikiana na taasisi zilizo chini yake na wadau wa sekta iliendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi ikiwa ni pamoja na kusimamia suala la utoaji wa haki na utawala bora nchini, kutoa ushauri wa kisheria, kubuni sera, mikakati na programu za kisekta na kusimamia utekelezaji wake.

Wizara imeendelea kuhakikisha kuwa huduma za kisekta zinaimarishwa na kuendelezwa kwa kuzingatia malengo ya kitaifa ambayo ni pamoja na Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2005, MKUKUTA na Mkakati wa kushirikiana na Wahisani (*Joint Assistance Strategy for Tanzania – JAST*). Wizara imeendelea na utekelezaji wa maelekezo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete alipotembelea Wizarani mwezi wa Februari, 2006, maagizo mbalimbali ya Bunge na Viongozi wa Serikali. Aidha, Wizara imezingatia

miongozo na kanuni za kimataifa kama Malengo ya Milenia (*MDGs*), Mikataba na makubaliano ya Taasisi na Mashirika mbalimbali ya Kimataifa yanayohusu Serikali yetu.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha utoaji wa haki na utawala bora, ushauri wa kisheria kwa Serikali na Taasisi zake, muundo wa zamani uliokuwa wa Wizara umerejewa upya na kutayarishwa mwingine mpya uliopitishwa rasmi na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 4 Aprili, 2008. Kwa muundo huu mpya, Ofisi ya Mwanasheria Mkoo wa Serikali imetenganishwa na Wizara kiutawala na kuwa taasisi inayojitegemea kama ilivyo kwa Taasisi nyingine zilizo chini ya Wizara. Aidha, majukumu ya muundo huu yametenganisha kazi za Naibu Mwanasheria Mkoo wa Serikali na zile za Katibu Mkoo wa Wizara. Kazi za Katibu Mkoo wa Wizara zitahusu usimamizi wa masuala yote ya fedha na ya kiutawala ambapo kazi za Naibu Mwanasheria Mkoo wa Serikali zitabaki za kumsaidia Mheshimiwa Mwanasheria Mkoo wa Serikali katika kutoa ushauri wa kisheria kwa Serikali na Taasisi zake. Kwa upande wa Wizara muundo umeanzisha Idara ya kupokea malalamiko na utoaji wa msaada wa kisheria kwa wananchi na pia Kitengo cha Kuratibu Programu ya Maboresho ya Sekta ya Sheria.

Mheshimiwa Spika, ni matarajio yangu kuwa mabadiliko haya yaliyofanywa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yataiwezesha Wizara kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa majukumu yake. Pamoja na mabadiliko hayo hatua za kujaza nafasi za uongozi zilizo wazi za Wakuu wa Idara, Vitengo na Sehemu kulingana na Sheria ya Utumishi wa Umma Na.8 ya mwaka 2002 zitatekelezwa ili kukidhi mabadiliko ya miundo yote miwili katika mwaka huu wa fedha wa 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa Programu ya Maboresho ya Sekta ya Sheria Nchini mwaka 2007/2008, programu hii itafanikisha ununuzi wa mabasi na magari kwa ajili ya usafiri wa mahabusu na wafungwa toka Magerezani kwenda Mahakamani. Magari hayo ya kisasa ni sehemu ya utaratibu mpya wa Jeshi la Magereza katika kusimamia na kuratibu upelekaji wa mahabusu Mahakamani, ambao kwa kuanzia umeanza kutekelezwa katika Mkoa wa Dar es Salaam na baadhi ya Wilaya za Mkoa wa Pwani.

Aidha, vifaa seti 17 za kamera (*moving cameras*), pikipiki 50 na magari 20 vilinunuliwa kwa ajili ya shughuli za upelelezi zinazofanywa na Jeshi la Polisi. Vile vile, ununuzi wa magari mengine manane ya Ofisi za Kanda za Mwanasheria Mkoo wa Serikali, ununuzi wa vifaa na samani katika shule ya maadili (*Reform School*) iliyoko Mbeya, Kitengo cha Usajili (*Legal Registry*) cha RITA, Kitengo cha Usajili cha Ofisi ya Msajili wa Vyama (*Registrar of Societies*) na Msajili wa Hati (*Registrar of Titles*) utafanyika mwaka huu wa fedha 2008/2009. Aidha, mtandao wa huduma ya kisheria kuitia taasisi ya *Tanganyika Law Society* utakamilishwa mwaka huu wa fedha 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa nyumba nane za Polisi Kigoma umekamilika. Pia, nyumba nane za Maafisa wa Chuo cha Magereza Ukonga zinajengwa na ukarabati wa

Mahakama za Mwanzo saba umefanyika katika maeneo ya Shelui – Iramba, Ilagalulu – Tabora, Kirua Vunjo – Moshi, Ikama Masoko – Tukuyu, Bereko – Kondoa, Kilolo – Iringa na Bassotu-Hanang. Aidha, ukarabati na ujenzi wa Mahakama za Mwanzo na shule ya watoto watukutu huko Mbeya ulikamilishwa. Maandalizi ya awali ya uchambuzi wa mkandarasi wa ujenzi wa Mahakama ya Rufani na Makao Makuu ya Wizara yamekamilika, Programu itakarabati nyumba 38 na kujenga nyingine 25 za Polisi. Aidha, nyumba 24 za Maafisa wa Magereza zitajengwa katika mwaka huu wa fedha 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2007/2008, Wizara kupitia programu hii imefanikiwa kupata kiwanja cha kujenga Taasisi ya Mafunzo ya Sheria kwa Vitendo (*Law School of Tanzania*) Dar es Salaam. Ujenzi unatarajiwa kuanza katika mwaka huu wa fedha 2008/2009. Aidha, mafunzo ya awali ya uendeshaji wa mashtaka kwa Mawakili wapya 157 yametolewa, Maafisa Upelelezi wa Polisi 195 walipatiwa mafunzo yanayoendana na mfumo mpya wa upelelezi na mafunzo ya muda mfupi yametolewa kwa Maafisa 70 toka taasisi zinazotekeleza programu hii ili kuongeza ufanisi katika utendaji kazi wao.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha uendeshaji wa kesi na utoaji wa haki nchini. Wizara, kupitia programu ya kuboresha mfumo wa sheria, inaendelea na mchakato wa kutenganisha shughuli za upelelezi na uendeshaji wa mashtaka nchini hadi kufikia ngazi za Wilaya. Hatua zilizofikiwa mpaka sasa ni pamoja na kuimarisha miundombinu ya Ofisi katika mikoa ilijojumuishwa katika hatua ya kwanza ya utekelezaji, yaani mikoa ya Arusha, Tanga, Dar-es-Salaam, Shinyanga, Ruvuma na Mwanza. Halikadhalika, Sheria ya Kusimamia Mfumo wa Mashtaka nchini (*National Prosecution Services Act*) imepitishwa kuwa Sheria tarehe 30 Januari, 2008 na imeanza kutumika tarehe 9 Juni, 2008. Sheria hii imeweka mfumo wa usimamizi wa shughuli za mashtaka na namna ya kuratibu shughuli za upelelezi katika jitihada za kuboresha utoaji wa haki katika mashauri ya jinai na madai.

Mheshimiwa Spika, jumla ya Mawakili wa Serikali 157 wameajiriwa na kusambazwa katika kanda 12 za Mikoa ya Tanga, Dar es Salaam, Mwanza, Tabora, Sumbawanga, Mbeya, Iringa, Ruvuma, Arusha, Moshi, Mtwara na Kagera. Katika mwaka huu wa fedha 2008/2009, mwongozo wa mashtaka (*Prosecution General Instructions*) na ule wa upelelezi (*Investigations General Instructions*) utakamilishwa.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikikisha kwamba nchi inatoa huduma bora ya kisheria kwa wananchi wake na kwa wakati, Wizara imeanzisha Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania, chini ya Sheria Na. 5 ya Mwaka 2007 na ambayo tayari imeanza kutumika kuanzia mwezi Mei, 2007. Hatua ya kuundwa kwa Bodi ya Uendeshaji wa Taasisi iliyozinduliwa tarehe 4 Januari, 2008 imechukuliwa. Kuanzishwa kwa taasisi hii ni matokeo ya utekelezaji wa Programu ya Maboresho katika Sekta ya Sheria.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Taasisi hii imeanisha majukumu mbalimbali ya kuandaa, kuendesha na kutoa mafunzo ya uanasheria kwa vitendo, kwa lengo la kuboresha ujuzi na viwango vya utendaji kazi mionganii mwa Wanasheria wote waliopo

hana nchini katika utoaji haki kwa kushirikiana na Baraza la Elimu ya Sheria nchini (*The Council of Legal Education*). Aidha, mafunzo haya yamelenga kuwaendeleza wahitimu wa shahada ya kwanza ya sheria ambao wanatarajia kujiunga na Utumishi wa Umma na kwa wale wanaohitaji kufanya kazi za uwakili binafsi.

Mheshimiwa Spika, Taasisi tayari imeandaa Mitaala na Kanuni za Uendeshaji na kupitishwa na Bodi. Maombi ya mikopo ya elimu ya juu kwa ajili ya Wanafunzi watakaojiunga na Taasisi hii yamepokelewa na yanashughulikiwa na Taasisi. Wizara ya fedha na Uchumi imetoa mkopo wa shilingi bilioni mbili kwa wanafunzi wa Taasisi hii. Hata hivyo, wanafunzi 274 wa awali wameandikishwa na wameanza masomo yao katika majengo ya muda ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Kitivo cha Sheria. Kwa mwaka 2008/2009, taasisi inatarajia kuandikisha wanafunzi 300 na kuajiri wakufunzi.

Mheshimiwa Spika, dhana za demokrasia na utawala bora misingi yake ni madaraka ya wananchi, utawala wa sheria, uwajibikaji na uadilifu katika kusimamia utekelezaji wa utoaji wa haki. Katika kulinda hadhi ya Serikali yetu katika utekelezaji wa Haki za Binadamu, mwaka jana nilihudhuria mikutano mbalimbali ukiwemo Mkutano wa Baraza la Haki za Binadamu uliofanyika huko Uswisi; Mkutano wa kuunganisha Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu uliofanyika huko Addis Ababa, Mikutano ya Tume ya Haki za Binadamu na Watu.

Katika mikutano hiyo tumekuwa tukitoa ufanuzi kuhusu mwenendo wa ulinzi na ukuzaji wa haki za Binadamu hapa nchini. Aidha, mwezi Mei mwaka huu nilihudhuria Mkutano wa 43 wa Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu ambapo taarifa yetu inayoeleza utekelezaji wa masuala mbalimbali ya kulinda na kukuza haki za binadamu kwa dhana ya demokrasia na utawala bora ilijadiliwa.

Aidha, zipo changamoto nyingi zinazotukabili kuhusu eneo hili likiwemo suala la kuwepo kwa adhabu ya kifo hapa nchini; kutoridhiwa kwa Mkataba wa Kuzuia Utesaji (*CAT*) na suala la kuwepo “*indigenous people*”.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kupitia Bunge lako Tukufu, kutoa taarifa kwamba, Tume kwa hivi sasa imetambuliwa katika ngazi ya Umoja wa Mataifa kuwa ni Tume iliyoundwa kwa kufuata misingi ya Paris (*Paris Principles*) kwa namna inavyofanya kazi, jinsi muundo wake ulivyo na namna inavyoteua Makamishna wake. Aidha, kwa kutambua mchango huo, Tume imepewa daraja la ’A’ kwenye Kamati ya Baraza la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa, ambalo heshima yake nikutambulika kwa nchi katika masuala ya Haki za Binadamu duniani kote.

Mheshimiwa Spika, shughuli za usajili wa matukio mbalimbali ya binadamu zilikuwa na mafanikio. Hadi ilipofika mwezi Juni, 2008, Wakala (*RITA*) ulikuwa umefanikiwa kusajili idadi ya vizazi 2,268,272; vifo 117,295; ndoa 12,295 na talaka 48 ikilinganishwa na idadi ya vizazi 829,384; vifo 118,538 na ndoa 46,320 kwa mwaka 2006/2007. Aidha, jumla ya watoto 27 wa kuasili waliandikishwa na kupatiwa vyeti vyaa kuasiliwa.

Katika shughuli za Mirathi na Udhamini, Wakala umesajili na kutoa vyeti vya usajili wa miunganisho ya wadhamini 318. Hata hivyo, eneo la uandikishaji wa matukio ya vifo, ndoa na talaka unahitaji kuimarishwa. Mirathi minane imepatiwa ufumbuzi na kufungwa. Katika eneo hili Wakala imeanzisha huduma ya utayarishaji na uhifadhi wa wosia kwa lengo la kupunguza migogoro katika masuala ya mirathi. Kuanzishwa kwa huduma hii mpya ni matokeo ya maboresho katika Sekta ya Umma ya kutoa huduma bora na kwa wakati. Huduma hii imeanza kutolewa katika Makao Makuu ya Wakala na itaendelea kwa mwaka huu wa fedha 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, Wakala umeimarisha mahusiano na wadau wanaofanya kazi za Wakala hususan shughuli za usajili na mirathi katika ngazi za Wilaya kwa kuwapatia mafunzo Makatibu Tawala wa Wilaya, Waganga Wakuu wa Wilaya, Wasaidizi Usajili, Watumishi katika Vituo vya Tiba, Maafisa Tarafa pamoja na Maafisa Watendaji wa Kata kwa Wilaya saba za Temeke, Bagamoyo, Kibaha, Hai, Makete, Mtware na Magu. Vilevile, Wakala imewapatia vitendea kazi watumishi wanaoshughulika na shughuli za usajili pamoja na kukarabati na kuweka samani katika baadhi ya Ofisi za Wilaya zikiwemo Temeke, Kinondoni, Morogoro, Musoma, Nyamagana, Dodoma, Shinyanga, Ilemela, Hanang na Musoma.

Mheshimiwa Spika, Wakala umeanza kuboresha mfumo wa mawasiliano (*Management of Information System*) ambao utawezesha ukusanyaji wa kumbukumbu zote za shughuli za Wakala kwa kuunganisha Wilaya zote za Tanzania Bara katika mtandao huu. Mfumo huu umeanza kutekelezwa Makao Makuu pamoja na Wilaya ya Temeke kwa majaribio. Mfumo huu utalinufaisha Taifa kwa kukusanya kumbukumbu kutokana na taarifa za usajili na kutoa takwimu zilizo sahihi kwa ajili ya mipango ya nchi. Aidha, mfumo huu wa mawasiliano utazinufaisha taasisi nyingine pia za uaandaaji wa Vitambulisho vya Utaifa, Vyuo Vikuu, Mabenki, Mifuko ya Pensheni, Daftari la wapiga kura na Idara ya Takwimu ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, katika kujenga uelewa mpana wa shughuli za Wakala kwa wananchi, Wakala umeeendelea kutoa elimu juu ya huduma zitolewazo kwa njia mbalimbali kwa kutumia vyombo vya habari. Vilevile, Wakala umeshiriki katika maonesho mbalimbali ya kitaifa yakiwemo yale ya Siku ya Mtoto wa Afrika, **TEKNOHAMA**, Wiki ya Utumishi wa Umma na kadhalika.

Napenda nilifahamishe Bunge lako Tukufu kuwa Wakala wetu ulishika nafasi ya kwanza kati ya Taasisi 115 zilizoshiriki Maonesho ya Utumishi wa Umma tarehe 16-23 Juni, 2008. Pia, ilishiriki katika maonesho ya 32 ya Biashara ya kimataifa yaliyofanyika katika viwanja vya Mwalimu Nyerere kuanzia tarehe 28 Juni, hadi 8 Julai, 2008. Kwa mwaka wa fedha 2008/2009, Wakala inatarajia kuanza kutoa elimu kwa umma kupitia vipindi vya luninga na redio ili kuwezesha wananchi walio wengi kupata elimu juu ya haki zao za msingi nakufahamu maboresho mbalimbali yanayoendelea katika Sekta ya Sheria. Aidha, huduma za usajili zitaendeleza katika wilaya za Ukerewe, Tanga, Hanang, Kibondo, Kasulu, Kigoma, Mpanda, Ngara na Siha.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Kazi za Mahakama Nchini. Katika kipindi cha mwaka 2007/2008, Serikali imewezesha Mahakama kutekeleza majukumu yake ya kutoa haki na utawala wa sheria. Kazi zilizofanyika ni pamoja na utekelezaji wa Programu ya Kuboresha Sekta ya Sheria ili kutoa huduma bora kwa jamii. Vilevile, imewezesha kuanzisha mchakato wa kutenganisha shughuli za upelelezi wa kesi za jinai na uendeshaji mashitaka. Serikali imejitahidi kuimarisha uwezo wa kuendesha kesi ili kupunguza mlundikano wa kesi mahakamani kwa kuteua Majaji na kuajiri Mahakimu wengi kwa wakati mmoja.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuchukua hatua mbalimbali katika kipindi cha mwaka 2007/2008 kwa lengo la kupunguza mlundikano wa kesi Mahakamani na kusikiliza migogoro ya mashauri katika Mahakama za Mwanzo, Wilaya na Mikoa. Mikakati iliyotumika ni pamoja na kutumia utaratibu wa Kamati za Kusukuma Kesi za Jinai, Mpango Maalum wa Kusukuma Kesi za Madai, kuteua Majaji zaidi, kuajiri Mahakimu wa Wilaya na Mikoa, Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo, Mawakili wa Serikali na Watumishi wa kada nyine.

Aidha, malalamiko na mashauri mbalimbali yanayohusu Haki za Binadamu, Migogoro ya Ardhi na Mashauri ya Biashara, Kazi na Ajira yameshughulikiwa. Pamoja na mambo mengine mikakati hiyo iliiwezesha Mahakama ya Rufani kuitisha vikao 16 vya kusikiliza mashauri kati ya 13 vilivyokuwa vimepangwa. Katika vikao hivyo, Mahakama ilisikiliza mashauri 1,189 kati ya 3,043 yaliyokuwepo. Ongezeko hilo la vikao lilitokana na uteuzi wa Waheshimiwa Majaji wanenye wa Mahakama ya Rufani walioeteuliwa hivi karibuni.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Mahakama Kuu ilifanikiwa kusikiliza mashauri 4,863 kati ya mashauri 14,152 yaliyokuwepo na kati ya hayo 1,874 yaliisha na yaliyobaki ni 2,986. Katika Mahakama za Mikoa na Wilaya, jumla ya mashauri 30,615 yalipangwa kusikilizwa na kati ya hayo mashauri 17,595 yalisikilizwa hadi kufikia mwezi Juni, 2008.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2008/2009, Mahakama ya Tanzania itaendelea kujizatiti katika kuimarisha uwezo wa kuendesha na kusukuma kesi ili kupunguza mlundikano wa kesi Mahakamani na mahabusu Magerezani kwa kufanya vikao 16 vya Mahakama ya Rufani. Pia, Mahakama Kuu imepanga kufanya vikao 208, vikao vya kila siku katika Mahakama 22 za Mahakimu Wakazi, Mahakama 88 za Wilaya na katika Mahakama 1,105 za Mwanzo vitaendelea kufanyika. Vikao vinne vya Kamati ya kusukuma mashauri vitafanyika kwenye kila kanda na kufanya vikao vinne vya Baraza la Elimu ya Sheria (*The Council of Legal Education*).

Aidha, Mahakama imepanga kununua pikipiki 100, ambazo siyo za mkopo, kwa ajili ya Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo ili kupunguza tatizo la usafiri na kuongeza ufanisi wa utendaji. Pikipiki hizo zitagawiwa kwa nchi nzima na ununuzi utaendelea kwa awamu kwa kadri bajeti itakavyoruhusu. Halikadhalika, nitoe wito kwa Mahakimu wote wa Mahakama zote nchini kuhakikisha kuwa kesi zote zinazohusu kuwapa mimba wanafunzi wa shule za msingi na sekondari mashauri yake yanamalizika haraka. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Spika, Divisheni ya Biashara ya Mahakama Kuu, inahusika na kusikiliza mashauri ya kibiashara na rufaa za mashauri hayo. Kwa mwaka 2007/2008 ilijiwekewa lengo la kumaliza asilimia 80 ya idadi ya kesi zinazofunguliwa. Hata hivyo, jumla ya mashauri ya 117 yalifunguliwa na mashauri 90 yalimalizwa kusikilizwa ikiwa ni asilimia 77 ya idadi ya kesi zilizofunguliwa.

Malengo yaliyokusudiwa kwa mwaka 2008/2009 ni kuendelea kushughulikia mashauri ya biashara kutoka mahakama za chini na kuyatolea maamuzi kwa wakati na kuhakikisha kuwa asilimia 90 ya idadi ya mashauri yaliyofunguliwa yatamalizika. Halikadhalika, ni kuhakikisha idadi ya kesi zinazofunguliwa ndani ya mwaka mmoja zinalingana na zile zinazomalizika ili kusiwe na mlundikano. Matarajio mengine ni kuendelea kusogeza huduma kwa wadau wengi zaidi. Aidha, inakusudiwa kuanza ujenzi wa jengo la masjala ndogo Dodoma, kukamilisha upembuzi yakinifu wa uanzishwaji wa masjala ndogo Mbeya na kukamilisha ujenzi wa jengo dogo la Ofisi ya Dar-es-Salaam.

Mheshimiwa Spika, Divisheni ya Kazi ya Mahakama Kuu inashughulikia migogoro ya kazi na ajira kwa kutoa haki za migogoro ajira na kazi ndani ya utaratibu wa Mahakama Kuu. Pia, inashughulikia rufaa kutoka Tume ya Upatanishi na Usuluhishi. Katika kipindi cha mwaka 2007/2008, ilipokea mashauri 941 na kumaliza mashauri 364 na yamebakia mashauri 577.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2008/2009 itaendelea na majukumu yake kwa mujibu wa sheria kutafsiri na kupokea maombi ya anuwai za kazi na ajira. Kusikiliza migogoro kati ya waajiri na wafanyakazi; kusikiliza rufaa, mapitio, marudio na marejeo kutoka vyombo vya kikazi na kupokea mashauri 600 na kumaliza 480 yaliyo sawa na asilimia 80. Pia, kusikiliza rufaa kutoka kwa Msajili wa Vyama vya Hiari vya Wafanyakazi na waajiri na kusikiliza mashauri yote yaliyoachwa na iliyokuwa Mahakama ya Kazi chini ya Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana. Vile vile, kuendelea na mchakato wa kukarabati jengo lake lililoko Kinondoni ambapo kwa sasa lipo katika hatua ya kusanifiwa.

Mheshimiwa Spika, katika kusogeza huduma karibu na wananchi, Ofisi za Kanda, huko Arusha na Mbeya zitafunguliwa. Kuwepo kwa Ofisi hizi kutawapunguzia wadau waliopo Mikoa ya karibu gharama za kufuata huduma hii Makao Makuu ya Divisheni yaliyopo Dar es Salaam. Aidha, tovuti na mtandao wa ndani wa Kompyuta (*Website & Local Area Network*) katika ofisi zake utaboreshw. Halikadhalika, Divisheni kwa kuititia vyombo mbalimbali vya Habari, itaendelea kutangaza shughuli zake ili zielewekwe kwa undani kwa wadau walio wengi zaidi.

Mheshimiwa Spika, Divisheni ya Ardhi ya Mahakama Kuu inashughulikia migogoro ya ardhi na nyumba na inasikiliza kesi za rufaa zinazotoka katika Mabaraza ya Nyumba ya Wilaya. Mwaka 2007/2008, hadi kufikia Juni 2008 ilipokea jumla ya mashauri 5,013, na kati hayo mashauri 736 yalisikilizwa na kumalizika ikilinganishwa na mashauri 612 ya mwaka 2006/07. Mashauri 4,277 yanaendelea kushughulikiwa.

Malengo ya mwaka 2008/2009 ni kuongeza ufanisi katika kushughulikia migogoro ya ardhi kwa kuhakikisha kwamba asilimia 80 ya migogoro mipy ya ardhi itakayofunguliwa inatatuliwa kwa wakati. Vile vile, itaimarisha usimamizi na ukaguzi wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya. Aidha, kufuatia uhaba wa Ofisi, Mahakama itakodisha majengo mawili kwa ajili ya Masjala ndogo zilizoko huko mkoani Arusha na Mwanza.

Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2007/2008, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali iliendelea kutekeleza majukumu ya kuiwakilisha Serikali katika kesi za madai dhidi yake na kuitetea mahakamani pale iliposhtakiwa au kushtaki. Vile vile, uendeshaji wa kesi za madai iliendelea kwa kutumia Mpango maalum wa kusukuma kesi, ambapo jumla ya kesi 189 zilisikilizwa na kumalizika kati ya kesi 251 zilizokuwepo na zimebaki kesi 62. Kwa upande wa kesi za madai katika Mahakama Kuu jumla ya mashauri 1,142 yamepokelewa na kati ya hayo mashauri 612 yametolewa uamuvi na mashauri 530 yanaendelea kusikilizwa. Katika Mahakama ya Rufaa jumla ya mashauri 34 yalipelekwa na kati ya hayo 11 yameshughulikiwa na mashauri 23 yanaendelea. Aidha, mashauri manne ya masuala ya upatanishi yanayoishusu Serikali yalipokelewa, mashauri mawili yameshughulikwa na mashauri mawili yanaendelea kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2007/2008 kulikuwa na kesi 36 za uchaguzi zilizofunguliwa, zote zimemalizika isipokuwa mbili za majimbo ya Uchaguzi la Mwibara na Tarime. Aidha, kwa kushirikiana na Idara ya Mashtaka, Mahakama ya Tanzania iliendesa vikao vya kamati ya kusukuma kesi na Bodi ya *Parole*. Halikadhalika, ilifanya vikao 28 vya kuendesa kesi katika kanda zote 13. Pia, Idara hii ilifanya vikao vinne vya Rufaa na ilisikiliza kesi 941 za rufaa na kuzitolea maamuvi. Usimamizi wa uendeshaji mashtaka ya jinai nchini iliendelea vizuri. Katika kushughulikia matatizo ya msongamano wa mahabusu na wafungwa Magerezani, Mawakili Wafawidhi kwa kushirikiana na Wakuu wa Upelelezi wa Mikoa, Majaji Wafawidhi na Mahakimu Wafawidhi walitembelea Magereza 20.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2008/2009, ukaguzi wa Magereza 60 na vituo vya Polisi 50 katika Wilaya 40 utafanywa na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. Tume pia itaendelea kutoa elimu ya haki za binadamu na misingi ya utawala bora katika Wilaya 70 na kutoa jumla ya vipeperushi 50,000 vya kuitangaza kwa lengo la kufahamu kazi zake. Aidha, Wizara itaendelea kusimamia jukumu lake la kuhakikisha kuwa, suala la demokrasia ya kweli na utawala bora kwa kuzingatia sheria zilizopo na zinazoendelea kutungwa linapewa kipaumbele na kutekelezwa katika ngazi zote za maamuvi.

Mheshimiwa Spika, jukumu lingine la Ofisi hii lilihusu kutoa ushauri wa kisheria kwa Serikali na Taasisi zake katika masuala ya Madai na Sheria za Kimataifa; mikataba ya Serikali na Mashirika yake; Uandishi, Uhuishaji na Tafsiri ya Sheria; Ushauri wa masuala ya Katiba na Haki za Binadamu na kushirikiana na Wizara nyingine katika uandaaji wa taarifa za mikataba ya kimataifa ya haki za binadamu na kuratibu shughuli za upelelezi wa makosa ya jinai.

Mheshimiwa Spika, majukumu ya Haki za Binadamu kwa mwaka 2007/2008 yaliendelea kutekelezwa. Mashauri 41 ya uvunjwaji wa Katiba yalishughulikiwa ambapo kati ya hayo 15 yalikuwa mapya na 26 yalikuwa ya zamani. Mashauri 12 yanaendelea kusikilizwa, matatu yaliondolewa Mahakamani, saba yametolewa uamuzi na matano yanashubiri uamuzi na 26 bado yanaendelea kusikilizwa. Aidha, chunguzi moja ya malalamiko ya uvunjwaji wa haki za binadamu bado inaendelea kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Utumishi wa Mahakama inatarajiwa kuwa taasisi inayo jitegemea baada ya muundo wake kuitishwa. Katika kipindi cha mwaka 2008/2009, Tume ya Utumishi wa Mahakama itashughulikia masuala ya ajira, uteuzi, kuthibitishwa kazini/cheo na masuala ya nidhamu ya Mahakimu na Maafisa wa Mahakama.

Pia, Tume ya Utumishi itaendesha semina ya kujitangaza Mikoani ili kuwaelimisha wananchi wazijue kazi zake na kuitumia. Mafunzo ya uandishi wa mihiutasari kwa makatibu wa kamati za maadili za Mahakama katika Mikoa na Wilaya yatatolewa. Tume kwa sasa iko katika jitihada za kutafuta jengo kwa ajili ya pango la Ofisi ili kuimarisha utekelezaji wa majukumu yake. Utekelezaji wa majukumu kwa taasisi hii utaendana na marekebisho ya Sheria ya Utumishi wa Mahakama (*The Judicial Service Act, Cap 237*) kukamilika mwezi Agosti, 2008 na kuwasilishwa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyowahi kutoa tamko katika mkutano wa kumi na moja wa kikao cha tano cha Bunge kilichofanyika tarehe 14 Aprili, 2008 wakati nikijibu swalii la Bunge na. 61 ambapo niliahidi kulifanyia kazi suala la Mahakama ya Tanzania kama mhimili mmojawapo wa Dola kuwa na mfuko wake wa fedha kama ulivyo Mfuko wa fedha wa Bunge. Naomba kuitia Bunge la Tukufu kutoa taarifa kwamba kimsingi Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amekubali kuanzishwa kwa Mfuko wa Fedha wa Mahakama (*Judiciary Fund*) katika kikao cha majadiliano na Majaji wote kilichofanyika tarehe 22 Mei, 2008 mijini Bagamoyo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka huu wa fedha 2008/2009, Wizara itaendelea kukamilisha uaandaji wa Waraka wa Serikali utakaowasilisha mapendekezo ya kufanya marekebisho katika Sheria ya Utumishi wa Mahakama na kuanzisha Mfuko wa fedha wa Mahakama (*Judiciary Fund*) katika kikao cha Majadiliano na Majaji wote kilichofanyika tarehe 22 Mei, 2008. Kwa sasa tunachoshughulikia ni taratibu za Kisheria na mara zitakapokamilika basi Mahakama itakuwa na Mfuko wake huru kama ilivyo kwa muhimili wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, katika kuleta ufanisi na tija katika utoaji wa haki na kuboresha utendaji wa kazi, Wizara imewapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi ya fani mbalimbali watumishi wa kada zote. Jumla ya wasimamizi 21 wa Programu ya Kuboresha Sekta ya Sheria kutoka Taasisi 15 zinazotekeliza Programu hii na Maafisa 40 wamepatiwa mafunzo ya uratibu na usimamizi wa Programu. Kwa upande wa Mahakama ya Tanzania, watumishi wa Mahakama wa ngazi mbalimbali walipatiwa mafunzo. Mahakimu Wakazi watano wamepata mafunzo ya uzamili, Mahakimu wa Mahakama za

Mwanzo 89 wamepata mafunzo ya stashahada ya sheria, 29 wamepata cheti cha Sheria na 40 Kiswahili kigumu.

Mheshimiwa Spika, katika kuinua viwango vya utendaji wa watumishi mwaka huu wa fedha 2008/2009, Mahakama imekusudia kusomesha Mahakimu 35 wa Mahakama za Mwanzo na makarani katika ngazi ya cheti na stashahada. Mafunzo ya uzamili yatatolewa kwa mahakimu wakazi 10 na watumishi wanne wa kada nyingine. Mafunzo ya muda mfupi yatatolewa kwa majaji watano, Mahakimu wakazi 40 na Mahakimu 100 wa Mahakama za Mwanzo. Aidha, watumishi 253, kati yao, Mahakimu wakazi 40, Mahakimu wa Mahakama za mwanzo 100 na 113 ni wa kada nyingine wataajiriwa kwa kipindi husika ili kukabili tatizo la upungufu uliopo wa watumishi katika Mahakama zetu.

Mheshimiwa Spika, katika Divisheni ya Biashara ya Mahakama Kuu, jumla ya watumishi 10 wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu na watumishi 36 wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi. Kwa mwaka 2008/2009, watumishi wa taaluma mbalimbali wataendelezwa. Aidha, semina mbili zenyne mada inayohusu kujikinga na UKIMWI na mapambano dhidi ya rushwa zitafanyika. Kila masjala ndogo itapatiwa Naibu Msajili kwa lengo la kuboresha mazingira ya kazi kwa kuendeleza usafi wa majengo na mazingira yake. Vifaa vyenye ubora katika Ofisi vitanunuliwa.

Mheshimiwa Spika, Divisheni ya Ardhi ya Mahakama Kuu imewapatia watumishi watano mafunzo ya muda mrefu na watumishi 30 wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi. Kwa upande wa Divisheni ya Kazi ya Mahakama Kuu watumishi 30 walipatiwa mafunzo ya muda mfupi ndani na nje ya nchi na watano kati ya hao wanahudhuria mafunzo ya muda mrefu ndani ya nchi.

Katika kuwaendeleza watumishi wake, Divisheni imepanga kuwapatia mafunzo ya muda mfupi ndani na nje ya nchi watumishi wa kada mbalimbali. Jumla ya watumishi 35 watapelekwa mafunzioni, kati ya hawa watumishi saba kwa mafunzo ya muda mrefu na waliobaki watahudhuria mafunzo ya muda mfupi ili kuongeza ujuzi kwa fani zao.

Pia, itaajiri watumishi wanne, kati yao ni Afisa Utumishi mmoja na Madereva watatu. Ili kutimiza azma yake ya kuboresha mawasiliano ya habari na kuitangaza Divisheni ya Mahakama ya Kazi, Katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali jumla ya watumishi 182 wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi na watumishi 22 mafunzo ya muda mrefu. Tume ya Kurekebisha Sheria iliwapatia mafunzo watumishi 18. Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora imewapatia mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi watumishi 14 wa kada mbalimbali. Mafunzo haya kwa kiasi kikubwa yameboresha utendaji kazi wa watumishi katika kila kitengo, hivyo kuongeza tija katika kutekeleza majukumu. Aidha, mafunzo yaliyotolewa kwa watumishi wote katika Wizara yamesaidia sana kupunguza malalamiko kutoka kwa wananchi na kuimarisha uendeshaji mashauri.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto, Wizara imeendelea kukitegemea sana Chuo hiki kwa kutoa mafunzo ya Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo na Makarani wa Mahakama. Katika mwaka 2007/2008, Chuo

hiki kimeongeza idadi ya wanafunzi kutoka 336 hadi 419 kwa kozi ya stashahada ya sheria na kutoka 80 hadi 90 kwa cheti cha sheria. Aidha, jumla ya wahitimu 116 walipata stashahada na 63 walipata cheti cha sheria. Mwaka huu wa fedha 2008/2009, Chuo kinatarajia kuendelea na ukarabati wa majengo ili kumudu ongezeko la idadi ya wanafunzi 500.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Utumishi wa Mahakama imeendelea kushughulikia masuala ya ajira, nidhamu na uteuzi wa Mahakimu na Maafisa wa Mahakama. Aidha, Tume imeendelea kumshauri Mheshimiwa Rais kuhusu mishahara, maslahi, maadili ya Majaji pamoja na suala la uteuzi wa Wasajili wa Mahakama ya Rufaa na Mahakama Kuu. Tume ilifanya vikao vitatu kati ya vinne vinavyotakiwa na kushughulikia ajira za kudumu na kubadilishwa cheo 121, kuthibitishwa kazini katika cheo 127, kupandishwa cheo 280 na nidhamu 15 kwa Mahakimu katika madaraja mbalimbali.

Sambamba na kuwapatia mafunzo watumishi, Wizara imeendelea kuajiri watumishi wa ngazi mbalimbali. Majaji wa Mahakama ya Rufani 4 na 11 wa Mahakama Kuu wameteuliwa na Mheshimiwa Rais. Uteuzi huu umeongeza idadi ya Waheshimiwa Majaji wa Mahakama ya Rufani kuwa 16 kutoka 12 na wa Mahakama Kuu kutoka 45 kuwa 56. Mahakama ya Tanzania imeajiri Mahakimu Wakazi 95 na Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo 128. Divisheni ya Kazi ya Mahakama Kuu imeajiri watumishi sita na wengine wawili waliletwa kuimarisha Kitengo cha Ugavi.

Mheshimiwa Spika, Makamishna sita, Makamishna Wasaidizi wawili na Katibu Mtendaji waliteuliwa na Mheshimiwa Rais kuiongoza Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. Halikadhalika, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ili ajiri watumishi 173 kati ya hao mawakili 157, wachumi wawili, wataalam wa mifumo ya kompyuta watatu na makatibu sheria saba.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kama ilivyokuwa kwa Wizara nyingine imekuwa msitari wa mbele katika kutekeleza Mkakati wa Kitaifa wa kupambana na rushwa. Kwa kushirikiana na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Wizara imekuwa ikisoma na kuchambua majalada ya kesi za rushwa na kuandaa hati za mashtaka kwa wahusika na kuendesha kesi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2007/2008 Wizara ilipokea majalada 103 toka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa. Majalada 39 yaliandaliwa hati za mashtaka, majalada 23 yalirejeshwa kwa upelelezi zaidi, majalada matatu yalifungwa baada ya kuona ushahidi uliopo hautoshi kuthibitisha kesi Mahakamani na majalada 38 yanaendelea kushughulikiwa.

Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Ofisi ya Maadili ya Watumishi wa Umma na Wakala wa Kusimamia Manunuzi ya Umma Tanzania (*PPRA*) ziko katika awamu ya kwanza ya utekelezaji wa Mradi wa Kupambana na Rushwa kubwa (*Grand Corruption*) unaohisaniwa na Serikali ya Uingereza kuitia Shirika lake la *DFID*. Katika kipindi cha 2007/2008, kiasi cha paundi za kiingereza 500,000 kilitolewa kwa ajili ya kuwajengea

uwezo Wakuu wa Ofisi za Kanda za Mwanasheria Mkoo wa Serikali katika kuendesha mashauri ya makosa ya rushwa kubwa. Aidha, mradi umekwisha fanikisha ununuzi wa vifaa na nyenzo mbalimbali muhimu kwa Idara ya Mkurugenzi wa Mashtaka vikiwemo vitabu, sheria mbalimbali, kompyuta na magari nane yatakayosaidia usafiri wa kwenda Mahakamani kwa Mawakili wa Serikali. Pia, kazi za mradi zitahusisha kuanzishwa kwa mfumo wa kuweka taarifa za kesi katika kompyuta (*computerized case docket management system*).

Mheshimiwa Spika, ushirikishaji wa jinsia zote katika utendaji kazi za Wizara unaendelea vizuri. Hivi sasa ushirikishwaji wa wanawake umeongezeka zaidi katika kazi za Mahakama Kuu na Rufani kwa kufikia asilimia 29 kama mlivyoona leo, kati ya lengo la asilimia 50. Aidha, ongezeko hili linachangiwa na uteuzi wa idadi ya Waheshimiwa Majaji waliopo sasa kwa kufikia 83. Kati yake Wanawake 28 na Wanaume 55. Sehemu ya uwiano huu upo pia katika Idara na taasisi nyingine za Wizara.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2007/2008 juhudini za kuhamasisha watumishi wa Wizara katika kujikinga na ugonjwa hatari wa Ukimwi ziliendelezwa. Jumla ya watumishi 479 walipima afya zao kwa hiari na watumishi wanne kati yao walijitangaza kuwa wameathirika. Aidha, watumishi 49 kati ya hao walipatiwa semina na ushauri nasaha. Wizara pia, imeshiriki katika kuandaa Muswada wa Sheria ya Ukimwi ambao umeshapitishwa na Bunge lako Tukufu kuwa Sheria. Aidha, rasimu ya Mpango wa Ukimwi mahali pa kazi kwa Ofisi ya Mwanasheria Mkoo wa Serikali imeandaliwa na kukamilika. Katika mwaka 2008/2009 Wizara inadhamiria kuendeleza programu mbalimbali za Ukimwi mahali pa kazi zilizoandaliwa ili juhudini hizi ziwe endelevu.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wizara ya Katiba na Sheria, napenda kuwashukuru kwa dhati wale wote walioshirikiana nasi katika kipindi cha mwaka 2007/2008 katika kutimiza malengo yetu. Shukrani zetu pia ziwaendee wadau wa maendeleo wanaoshirikiana nasi katika kutekeleza Programu na Mpango yetu ya Maboresho ya Sekta ya Sheria. Wahisani hao wanajumuisha Mashirika na Taasisi za kimataifa zinazochangia katika kuboresha utoaji haki sawa kwa wote na kwa wakati. Nchi na mashirika hayo ni pamoja na Serikali za Ujerumani, Ubelgiji, Denmark, Sweden, Finland, Canada, Uingereza (*DFID*), Benki ya Dunia (*WB*), *UNICEF* na Shirika la Umoja wa Mataifa (*UNDP*) na wengine wengi.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuwashukuru wananchi na wadau mbalimbali hasa sekta binafsi, wanahabari, vyuo vya elimu vinavyofundisha mambo ya sheria, vyama vya hiari vinavyohusika na mambo ya sheria kwa ushirikiano wao katika kutekeleza malengo ya sekta ya sheria. Shukrani za pekee ziwaendee waheshimiwa wabunge wenzangu kwa michango yao ambayo imechangia katika kuboresha huduma zitolewazo na Wizara. Naomba waendelee na ushirikiano huo ili tuweze kuendeleza sekta hii muhimu katika utoaji wa haki kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, shukrani zangu hazitakuwa zimekamilika bila kuwashukuru viongozi, watendaji wakuu na watumishi wote wa Wizara kwa ushirikiano ambao

wameendelea kunipatia katika kipindi cha uongozi wangu wa Wizara ya Katiba na Sheria.

Nikianza na Mheshimiwa Dr. Mary M. Nagu - Waziri aliyenitangulia; Mheshimiwa Jaji Mkuu - Augustino Ramadhani; Mwanasheria Mkuu wa Serikali - Mheshimiwa Johnson Paulo Mwanyika; Mheshimiwa Jaji Kiongozi, Salum Massati - Naibu Mwanasheria Mkuu na Katibu Mkuu Bwana Sazi Salula - Msajili wa Mahakama ya Rufaa Bwana Ferdinand Wambali, Msajili wa Mahakama Kuu Bi. Eliamani G. Mbise - Msajili wa Mahakama ya Biashara, Bwana John R. Kahyoza - Msajili wa Mahakama ya Kazi, Bwana Samuel G. Karua - Kaimu Msajili wa Mahakama ya Ardhi, Bi. Grace Mwakipesile - Katibu wa Tume ya Utumishi wa Mahakama; Bi. Celina Wambura, Kaimu Katibu Mtendaji wa Tume ya Kurekebisha Sheria; Bibi Angela Bahati - Kaimu Katibu Mtendaji wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Bibi Mary Massay, na Kaimu Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini, Bwana Philip Saliboko na watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano mzuri wanaonipa katika kutimiza majukumu niliyopewa. Kwa pamoja wamewezesha kutekeleza malengo tuliyojiwekea kwenye Wizara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ili Wizara iweze kutekeleza malengo yake yaliyoainishwa katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2008/2009, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya Sh. 89,853,123,600/= kwa ajili ya Matumizi ya Wizara kwa mwaka 2008/2009. Kati ya fedha hizi, Matumizi ya Kawaida ni Sh. 57,637,162,000/= ambapo Sh. 18,227,643,100/= ni Mishahara ya Watumishi wa Wizara (PE) na Sh. 39,409,518,900/= ni fedha za Matumizi Mengineyo (OC). Fedha za Miradi ya Maendeleo ni Sh. 32,215,961,600/= kati ya hizi, Sh. 6,356,843,000/= ni fedha zetu za ndani na Sh. 25,859,118,600/= ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, naliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe Makadirio hayo ya Fedha za Maendeleo na Matumizi ya Kawaida kwa Mafungu tisa kama ifuatavyo:-

MATUMIZI:

Fungu 12: Tume ya Utumishi wa Mahakama

Matumizi ya Kawaida	703,031,000
Matumizi ya Maendeleo (Ndani)	-
Matumizi ya Maendeleo (Nje)	-
Jumla Sh.	703,031,000

Fungu 16: Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali

Matumizi ya Kawaida	9,150,351,000
Matumizi ya Maendeleo (Ndani)	0
Matumizi ya Maendeleo (Nje)	1,637,250,000
Jumla Sh.	10,787,601,000

Fungu 40: Mahakama		
Matumizi ya Kawaida	33,411,097,000	
Matumizi ya Maendeleo (Ndani)	5,137,374,000	
Matumizi ya Maendeleo (Nje)	5,531,000,000	
Jumla Sh.	44,079,471,000	

Fungu 41: Wizara ya Katiba na Sheria		
Matumizi ya Kawaida	6,850,129,000	
Matumizi ya Maendeleo (Ndani)	1,079,893,000	
Matumizi ya Maendeleo.(Nje)	16,442,433,600	
Jumla Sh.	24,372,455,600	

Fungu 55: Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora.		
Matumizi ya Kawaida	2,873,868,000	
Matumizi ya Maendeleo (Ndani)	-	
Matumizi ya Maendeleo (Nje)	1,351,000,000	
Jumla Sh.	4,224,868,000	

Fungu 59: Tume ya Kurekebisha Sheria.		
Matumizi ya Kawaida	1,256,234,000	
Matumizi ya Maendeleo (Ndani)	-	
Matumizi ya Maendeleo (Nje)	572,636,000	
Jumla Sh.	1,828,870,000	

Fungu 60: Mahakama ya Kazi.		
Matumizi ya Kawaida	1,116,651,000	
Matumizi ya Maendeleo (Ndani).	-	
Matumizi ya Maendeleo (Nje)	-	
Jumla Sh.	1,116,651,000	

Fungu 64: Mahakama ya Biashara.		
Matumizi ya Kawaida	1,137,512,000	
Matumizi ya Maendeleo (Ndani)	139,576,000	

Matumizi ya Maendeleo (Nje)	228,799,000
Jumla Sh.	1,505,887,000

Fungu 90: Mahakama ya Ardhi.

Matumizi ya Kawaida	1,138,289,000
Matumizi ya maendeleo (ndani)	-
Matumizi ya Maendeleo (nje)	96,000,000
Jumla Sh.	1,234,289,000

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2007/2008 hadi kufikia mwezi Juni, 2008 Wizara ilikuwa imekusanya jumla ya Sh. 2,517,289,207/= ikilinganishwa na Sh. 2,638,783,605/= zilizokusanywa mwaka 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2008/2009, Wizara yangu inatarajia kukusanya kiasi cha Sh. 2,623,442,000/= kama Maduhuli ya Serikali. Mchanganuo wa makusanyo kwa kila Fungu husika ni kama ifuatavyo:

Fungu 40	-	Sh.	858,433,000
Fungu 41	-	Sh.	1,118,861,000
Fungu 55	-	Sh.	1,144,000
Fungu 64	-	Sh.	580,001,000
Fungu 90	-	Sh.	<u>65,003,000</u>
Jumla	-	Sh.	<u>2,623,442,000</u>

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

SPIKA: Ahsante sana Waziri wa Katiba na Sheria.

Waheshimiwa Wabunge, nilipokuwa natambua uwepo wa wageni kwenye *gallery* bahati mbaya sikupewa jina la Mheshimiwa Jaji Mfawidhi Ernest Mwipopo wa Mahakama Kuu Kitengo cha Kazi, ningombaa asimame. Ahsante sana, Mheshimiwa, samahani sana!

Basi, tunaendelea. Namwita sasa Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria kwa niaba yake, Mheshimiwa Maneno.

MHE. RAMADHANI A. MANENO (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala na kwa mujibu wa Kanuni ya 99(7), Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge

ya Katiba, Sheria na Utawala, kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha wa 2007/2008 na Makadario ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuipatia Kamati yangu kazi ya kujadili Makadirio ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009, Kamati ilikutana na Wizara ya Katiba na Sheria, tarehe 5 Juni, 2008, katika Ofisi Ndogo ya Bunge, Dar es Salaam, kushughulikia Makadirio ya Wizara hiyo. Aidha, Kamati ilipokea na kujadili taarifa ya Wizara kuhusu utekelezaji wa majukumu yaliyofanywa kwa Mwaka wa Fedha uliopita na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2008/2009, iliyowasilishwa na Mheshimiwa Mathias M. Chikawe, Waziri wa Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Katiba na Sheria inahusisha Mafungu yafuatayo: Fungu 41 - Wizara ya Katiba na Sheria; Fungu - 59 Tume ya Kurekebisha Sheria; Fungu 55 - Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora; Fungu 40 – Mahakama; Fungu 16 - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali; Fungu 12 - Tume ya Utumishi wa Mahakama; Fungu 60 - Mahakama ya Kazi; Fungu 64 - Mahakama ya Biashara; na Fungu 90 - Mahakama ya Ardhi.

Katika Mwaka wa Fedha wa 2007/2008, Wizara ya Katiba na Sheria ilitekeleza shughuli mbalimbali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kipindi kilichopita Kamati ilipokea taarifa kuwa Wizara iliandaa mikakati mbalimbali ya kupunguza mlundikano wa kesi Mahakamani. Miiongoni mwa mikakati hiyo ni kuandaa taratibu mbalimbali za kusukuma kesi za jinai na kesi za madai, kuongeza idadi ya watumishi katika sekta ya sheria kwa kuajiri mawakili, mahakimu na watumishi wa kada nyingine na kuteua majaji.

Katika kutekeleza azma hii Bunge lako tukufu litakumbuka kuwa tangu Serikali ya Awamu ya Nne iingie madarakani, imefanya juhudu kubwa kuwateua Majaji wa Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufaa. Hivi karibuni Serikali ili wateua Majaji, wengi wao wakiwa wanawake. Hii ni katika kukabiliana na upungufu wa watumishi hao katika Mahakama hususan katika kanda au mikoa ambako upungufu huo umekuwa ukisababisha ucheleweshaji wa kesi. Kamati inaipongeza Serikali kwa jitihada hizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika ziara ya Kamati iliyofanyika tarehe 18 – 25 Januari, 2007, kukagua miradi ya maendeleo katika Mikoa ya Iringa na Ruvuma, ikiwemo Miradi ya Mahakama, Kamati ilijionea hali halisi ya upungufu wa watumishi uliopo Mahakama za Mwanzo, Wilaya na Mahakama Kuu zilizopo katika mikoa hiyo. Hii ni pamoja na matatizo ya usafiri na vitendea kazi na uchakavu wa majengo, hususan Mahakama za Mwanzo. Kamati inaanini kuwa, picha ambayo imeipata katika mikoa hiyo, inafanana na mikoa mingei nchini.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mikakati mizuri iliyowekwa na Serikali katika mwaka huu wa fedha kuwapatia usafiri mahakimu, inaonekana kuwa zoezi hilo linakwenda polepole, ikilinganishwa na Idara na Taasisi nyingine za Serikali. Kwa

sababu hiyo, Kamati inashauri kuwa, Wizara iharakishe utaratibu mzima wa kuwapatia usafiri mahakimu ili waweze kutoa huduma kwa wananchi kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha na kuboresha uendeshaji wa mashitaka, katika kipindi cha mwaka 2007/2008, Serikali ilianzisha mchakato wa kutenganisha shughuli za upelelezi na uendeshaji mashitaka na kuwasilisha Bungeni Muswada wa Sheria ya Kusimamia Mfumo wa Mashitaka Nchini uliopitishwa na Bunge tarehe 30 Januari, 2008. Baada ya kuridhiwa na Rais, Muswada huo umekuwa Sheria na Sheria hiyo (*The National Prosecution Act No.27 2008*), imeanza kutumika tarehe 9 Juni, 2008.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kuwa tarehe 23 Juni, 2006, Serikali ilizindua rasmi Wakala wa Serikali wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (*RITA*), kutokana na iliyokuwa Idara ya Kabidhi Wasii Mkuu. Wakala huo umeundwa chini ya Sheria ya Wakala wa Serikali Na. 30 ya Mwaka 1997 na uliundwa kutokana na nia ya muda mrefu ya kubadili muundo wa iliyokuwa Ofisi ya Kabidhi Wasii Mkuu kuwa taasisi inayojitegemea kwa lengo la kuboresha majukumu yake.

Aidha, katika kipindi kilichopita, Wizara kwa kupitia Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini iliendelea na kuimarisha shughuli za usajili wa vizazi na vifo, ndoa na talaka, kusimamia mirathi na ufilisi, kusajili miunganisho ya wadhamini na kusajili watoto wa kuasili (*adopted children*). (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu yake, wakala imeweka mikakati ya kupitia na kurekebisha vipengele vya sheria zinazoongoza kazi za Wakala zilizokuwa zinakwamisha na kuchelewesa huduma kwa wananchi. Mikakati hiyo ni pamoja na kufanya mapitio ya taratibu zinazokwamisha huduma, hususan fomu za maombi ya cheti cha kuzaliwa kwa waliochelewa kuandikishwa ili kupunguza gharama na kuwaondolea kero wananchi, kutoa huduma za papo kwa papo katika makao makuu ya Wakala na kuwezesha kupatikana kwa cheti katika muda wa siku moja hadi tatu.

Kamati inapenda kuchukua fursa hii kuupongeza Wakala kwa kuweka mikakati hiyo mizuri inayolenga kuondoa urasimu na kuleta ufanisi. Pamoja na hayo, Kamati inashauri kuwa zoezi la kusajili vizazi lifanywe kwa uangalifu sana kwa kufuatilia kwa makini kumbukumbu zote za watu waliochelewa kuandikishwa watakaoomba hati za kuzaliwa ili kuepuka udanganyifu unaoweza kujitokeza. Vinginevyo, Taifa linawezekujikuta linawapa hati za kuzaliwa watu ambao si raia wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, jukumu kuu la Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ni kuhakikisha kwamba, haki za binadamu na misingi ya Utawala Bora inakuzwa, inalindwa, inazingatiwa, inatekelezwa na inahifadhiwa kwa lengo la kujenga jamii inayozingatia haki na misingi ya Utawala Bora.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi kilichopita, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ilishughulikia malalamiko kadhaa ya haki za binadamu kutoka Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar. Aidha, Tume ilitoa elimu kwa wananchi, wafanyakazi wa

taasisi na vyombo mbalimbali nchini kwa ajili ya kuwapa elimu kuhusu masuala ya haki za binadamu na Utawala Bora.

Pamoja na jitihada zilizofanyika, Kamati inashauri kuwa, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ipanue wigo wake wa kuwatembalea wadau wengi iwezekanavyo wakiwemo wananchi vijijini, kwa ajili ya kuwaelimisha, kusikiliza malalamiko yao na kutoa ushauri kuhusu masuala ya haki za binadamu na Utawala Bora. Hayati Mwalimu Julius Nyerere, aliwahi kutamka kuwa, ili tuendelee tunahitaji vitu vinne; watu, ardhi, siasa safi na uongozi bora.

Kamati inaamini kuwa, hivyo vyote vitaweza kufikiwa iwapo wananchi wetu, wakiwemo viongozi katika halmashauri zetu, watapewa elimu ya kutosha kuhusu Utawala Bora unaozingatia misingi ya demokrasia.

Mbali na hayo, Tume ilifanya utafiti kuhusu masuala yanayohusu haki za binadamu na Utawala Bora. Aidha, Wizara imeshiriki katika mikutano ya Kimataifa ya Haki za Binadamu na kutoa taarifa kuhusu jinsi Tanzania inavyotekeleza mikataba inayohusika katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu yake, Tume imekabiliwa na matatizo kadhaa ambayo yamesababisha isitekeleze majukumu yake kikamilifu. Kwa mfano, kutohana na shughuli zake, Tume husafiri sehemu mbalimbali. Zoezi hilo siyo tu linahitaji fedha nyingi, lakini pia linahitaji magari imara. Kamati inashauri kuwa jitihada za haraka zifanyike ili kuipatia Tume magari mapya yatakayoiwezesha kusafiri masafa marefu badala ya kutegemea magari yaliyopo ambayo yanapoharibika matengenezo yake huigharimu Serikali kiasi kikubwa cha fedha.

Mheshimiwa Spika, tatizo jingine ni kwamba, baadhi ya Ofisi za Tume zipo katika majengo yaliyochakaa na ya kukodi; Dar es Salaam, Pemba na Unguja. Kamati inashauri kuwa, majengo hayo yafanyiwe ukarabati haraka kupusha hatari inayoweza kutokea na kwa upande wa Zanzibar, Serikali inunue jengo jipya litakalokidhi mahitaji ya shughuli za Tume.

Mheshimiwa Spika, kama nililivyotaja hapo mwanzo, jukumu mojawapo la Tume hii ni kufanya utafiti kuhusu masuala mbalimbali yanayohusiana na Utawala Bora na haki za binadamu kwa jumla. Lengo la utafiti huo ni kuiwezesha Serikali kupata majibu sahihi ya kukabiliana na matatizo yaliyopo.

Miongoni mwa matatizo ambayo yamekuwa yakiisumbua Serikali na Wananchi kwa jumla ni kukithiri kwa mauaji ya maalbino. Kwa kutambua tatizo hilo, Tume inahitaji kufanya utafiti wa kina juu ya mauaji hayo katika Mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Mara na Mbeya. Kamati inatoa wito kwa wananchi wote kuipa Tume ushirikiano itakapotekeleza jukumu hilo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilijulishwa kuwa, muundo wa Ofisi ya Mwanasheria wa Serikali umerejewa na kufanya Ofisi hiyo kuwa Taasisi inayojitegemea kama zilivyo taasisi nyingine. Katika utaratibu huo, nafasi ya Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika Wizara imetenganishwa na ile ya Katibu Mkuu. Lengo ni kumwezesha Naibu Mwanasheria Mkuu, kumsaidia Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kuboresha utendaji kazi wa Taasisi hiyo.

Mheshimiwa Spika, jukumu mojawapo la msingi la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni kutoa ushauri kwa Serikali na Taasisi zake. Katika kipindi cha mwaka 2007/2008, Ofisi hiyo ilitoa ushauri kwa Serikali na taasisi zake kuhusu mambo yanayohusu madai, Sheria za Kimataifa, Mikataba ya Biashara, Katiba na Haki za Binadamu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, jukumu hili linaweza kutekelezwa vyema endapo Taasisi hiyo itakuwa na wafanyakazi wa kutosha, wenyewe uwezo na watakaopewa vivutio vitakavyowafanya wavutike na mazingira ya kazi na hivyo kutoshawishika na rushwa.

Aidha, Kamati inashauri kuwa, Mawakili wa Serikali wapewe mafunzo ya mara kwa mara, yatakayowajengea uwezo mzuri wa kuiwakilisha na kuishauri Serikali na taasisi zake katika maeneo mbalimbali ikiwemo mikataba.

Mheshimiwa Spika, uandishi na utafiti wa Sheria ni moja kati ya eneo ambalo limekuwa likishughulikiwa na Wizara ya Katiba na Sheria. Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi wa jinsi Miswada ya Sheria inavyoandalialiwa na Serikali kuititia kwa Mwandishi Mkuu wa Sheria na kuwasilishwa Bungeni kwa hatua mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, ili kuboresha mfumo wa huduma za kisheria, Wizara ya Katiba na Sheria, imefanya utafiti kuhuisha Sheria zilizopitwa na wakati na kuandaa Miswada na kutafsiri sheria kwa Lugha ya Kiswahili. Aidha, Tume ya Kurekebisha Sheria, imefanya utafiti wa baadhi ya sheria ambazo zipo katika hatua za rasimu za mwisho. Kamati inatumaini kuwa, wakati utakapowadia, Miswada ya sheria hizo itawasilishwa Bungeni kwa hatua muhimu.

Kamati inaipongeza Wizara na Tume kwa jitihada hizo. Aidha, inaipongeza Wizara kwa kuona umuhimu wa kufanya utafiti juu ya uwezekano wa kutafsiri sheria kwa Lugha ya Kiswahili. Pengine ni kutokana na sababu za kihistoria, taasisi zetu za sheria nchini zimekuwa zikitumia Lugha ya Kingereza na hivyo kuwanyima Watanzania walio wengi, fursa ya kuzielewa sheria kwa lugha wanayoilewa vyema. Hata hivyo, Kamati inashauri kuwa, zoezi la utafiti wa matumizi ya Kiswahili katika sheria za nchi, lihusishe wadau mbambali wakiwemo Waheshimiwa Wabunge, asasi za kiraia, wanasheria, wataalamu wa Kiswahili na wananchi kwa ujumla ili waweze kutoa ushauri mzuri wa jinsi ya kuboresha Miswada yetu na sheria zetu kwa ujumla. Aidha, Kamati inasisitiza kuwa, sheria zinazohitaji marekebisheso kama Sheria ya Ndoa, Sheria ya Mirathi, Sheria ya Mtoto na kadhalika, zishughulikiwe mapema na marekebisheso yake yawasilishwe Bungeni. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, katika kipindi kilichopita, shughuli nyingine zilizofanyika ni pamoja na kuwaendelea watumishi katika taaluma mbalimbali na kuongeza idadi ya watumishi kwa kuwaajiri watumishi wapya; kuanzisha Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa vitendo iliyoanzishwa chini ya Sheria Na.18 ya Mwaka 2007 na kuanza kutumika mwezi Mei, 2007; uboreshaji wa mazingira ya kazi kwa kujenga majengo mapya, kukarabati majengo ya zamani ya Mahakama na Ofisi za Kanda za Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, pamoja na ununuvi wa vitendea kazi na vyombo vya usafiri; kuratibu Programu ya Maboresho ya Sekta ya Sheria ambayo inatekelezwa na Taasisi 15 zikiwemo Wizara saba, Idara na Taasisi za Serikali na zisizo za Kiserikali na kushughulikia masuala mtambuka, ikiwemo Mikakati ya Kitaifa ya Kupambana na Rushwa na Ukimwi katika Wizara.

Mheshimiwa Spika, kama alivyosema Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Mathias B. Chikawe, wakati akitoa majumuisho ya Makadirio ya Wizara yake kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009, kwenye kikao cha Kamati; Wizara ya Katiba na Sheria imepanuka sana na ina majukumu mazito ambayo yanagusa nyanja zote za kiuchumi, kijamii, kisiasa na kiutamaduni. Kwa kuzingatia unyeti huo, Serikali imekuwa ikiipa Wizara hiyo umuhimu wa pekee wa kutengewa rasilimali kufuatana na uwezo uliopo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kusikia kilio cha mara kwa mara kilichokuwa kikitolewa na Kamati kupigania Bajeti ya Wizara. Hata hivyo, kama nilivyoeleza hapo awali, yapo baadhi ya matatizo ambayo bado hayajatafutiwa ufumbuzi wa kutosha hadi hivi sasa kutohana na ufinyu wa bajeti. Kamati inasisitiza na kuishauri Serikali kwamba, jitihada zaidi zifanyike ili Wizara iongezewe bajeti yake kushughulikia maeneo yenye matatizo zaidi.

Mheshimiwa Spika, shughuli zilizopangwa kutekelezwa kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009, Wizara imejiwekea malengo ya kutekeleza majukumu yake ya kusimamia utoaji haki kwa wananchi. Aidha, itashughulikia shughuli mbalimbali zilizoainishwa kwenye majukumu ya msingi ya Wizara na Taasisi zake, ikiwa ni pamoja na kuendeleza shughuli zilizoanza kutekelezwa katika kipindi kilichopita. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009, Wizara ya Katiba na Sheria imeomba iipitishiwe jumla ya shilingi 89,853,123,600 kwa ajili ya Mafungu yake yote. Kati ya fedha hizo, shilingi 57,637,162,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi 32,215,961,600 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kamati iliyapokea maombi hayo na kuyapitisha Fungu kwa Fungu ili yawasilishwe Bungeni kwa hatua zinazofuatia.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii muhimu ya kuwasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009.

Aidha, namshukuru Mheshimiwa Mathias B. Chikawe, Waziri wa Katiba na Sheria, Waheshimiwa Wenyeviti wa Tume, Makamishna wa Tume, Waheshimiwa Majaji, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Katibu Mkuu, Wakuu wa Idara, Taasisi

na Vitengo na Maafisa wote wa Wizara, kwa kushirikiana vyema na Kamati wakati wote ilipojadili Makadirio ya Wizara.

Kipekee, naomba niwashukuru Wajumbe wa Kamati hii, kwa kufanya uchambuzi wa kina wakati wa Makadirio ya Wizara hii. Naomba niwatambue kama ifuatavyo: Mheshimiwa Geroge Malima Lubeleje, Mwenyekiti, Mheshimiwa Ramadhani A. Maneno, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Yusuf R. Makamba, Mheshimiwa Kingunge Ngombale-Mwiru, Mheshimiwa Stephen J. Galinoma, Mheshimiwa Fatma Mussa Maghimbiri, Mheshimiwa Pindi H. Chana, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mheshimiwa Nimrod E. Mkono, Mheshimiwa Rajab Hamad Juma, Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakary, Mheshimiwa John P. Lwanji, Mheshimiwa Salim Yussuf Mohamed, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa Abass Z. Mtemvu na Mheshimiwa Benedict N. Ole-Nangaro

Aidha, napenda kutumia fursa hii kumshukuru Kaimu Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas D. Kashililah, Wakuu wote wa Idara na Vitengo na Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge, kwa kufanikisha shughuli za Kamati.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, nawashukuru Makatibu wa Kamati hii, kwa kuratibu na kushiriki kikamilifu katika maandalizi ya vikao vya Kamati. Naomba niwataje kama ifuatavyo; Ndugu Charles Mloka, Ndugu Ramadhani Abdallah na Ndugu Elihaika Mtui.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu, liipokee taarifa hii na likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria na Mafungu yake yote, kwa Mwaka wa Fedha wa 2008/2009. Jumla ya shilingi 89,853,123,600 zinaombwa na kati ya fedha hizo; shilingi 57,637,162,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi 32,215,961,600 kwa ajili ya Mpango wa Maendeleo kama alivyowasilisha Mto Hoja.

Mheshimiwa Spika, naiunga mkono hoja hii na naomba kuwasilisha. (*Makofii*)

MHE. FATMA MUSSA MAGHIMBI - MSEMADI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, napenda kutoa maoni kuhusu Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2008/2009, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 99 (7), Toleo la mwaka 2007.

Kwanza, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwenye wingi wa rehema, kwa kunipa afya njema na kuweza kusimama mbele yenu ili niweze kutoa maoni kwa niaba ya Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara hii ya Katiba, Sheria na Utawala. Napenda pia kuendeleza shukrani zangu kwa Wananchi wa Jimbo la Chake Chake, kwa imani yao kwangu na mimi nawaahidi nitaendelea kuwatumikia kwa uadilifu mkubwa. Kwa umuhimu mkubwa sana, napenda kumshukuru mume wangu, Bwana Mussa Maghimbiri, kwa uvumilivu mkubwa alionao, wakati ninapokuwa katika shughuli za siasa.

Mheshimiwa Spika, pili, napenda kuishukuru Kambi ya Upinzani kwa utendaji wake bora na ushirikiano unaoifanya kila leo ionekane kuwa imara na muhimu katika kupelekeea utendaji bora wa serikali. Pia nahisi nitakuwa mwizi wa fadhila, kama sitatoa shukrani zangu za dhati kwa chama changu cha *CUF*, kwa uongozi wake makini chini ya Mwenyekiti wake Prof. Ibrahim Lipumba na Katibu Mkuu wake Maalim Seif Shariff Hamad na nia zao za kuwatetea Watanzania, ustawi na maendeleo ya taifa letu.

Naahidi kukilinda chama changu, kukitetea na kupigania utekelezaji wa sera zake makini ili kuhakikisha haki sawa inapatikana kwa Watanzania wote popote walipo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba sasa nitoe maoni ya Kambi ya Upinzani katika Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka 2008/2009 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hoja ya Katiba mpya ya Tanzania: Moja ya kazi ya Kambi ya Upinzani ni kutoa maoni hasa ya kupendekeza marekebisho ya mambo ya msingi katika Serikali yetu na Taifa kwa jumla. Inapofikia mapendekezo ya kurekebisha jambo kubwa kama Katiba, Wizara ya Katiba na Sheria isipuuze kile tunachopendekeza. Katika hotuba yetu ya bajeti ya mwaka 2007/2008, nilipendekeza kuitia vipengele 12, lakini hadi leo hii hakuna dalili ya mabadiliko yoyote. Naomba nikumbushe kwamba, hoja ya kuwa na Katiba mpya si ya kambi ya Upinzani tu bali ni kilio cha Watanzania wote.

Hii ni kwa sababu marekebisho 14 yaliyofanywa katika Katiba, hayatoshelezi kuleta maendeleo na wala mustakabali wa kitaifa. Katiba imempa Rais Madaraka makubwa kuitia kiasi. Kuna sehemu imebana utendaji kama ilivyojitokeza wakati tunapitisha Sheria ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za za Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inashauri kuwa, suala la kuwa na Katiba mpya ya Tanzania ni la msingi, haliepukiki kwa sasa na lisifumbiwe macho. Hivyo basi, Katiba mpya itungwe kwa kuwashirikisha wananchi wote, kwa utaratibu utakaoandaliwa na pia kuitia vikundi mbalimbali vya kijamii, vyama vya siasa na viongozi wa kidini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hoja ya mgombea binafsi wa Urais; nchi yoyote inayopenda utulivu ni lazima iheshimu sheria, demokrasia ya kweli na Haki za Binadamu ikijumuisha kutoa haki za msingi za Raia. Tanzania inaonekana inayumba katika kuheshimu mambo hayo matatu. Suala la kuwa na mgombea binafsi ni la msingi na kilio cha muda mrefu. Kwa hiyo, hatuwezi kulipuza kwa sababu linaungwa mkono na Watanzania walio wengi. Mgombea binafsi inapaswa aruhusiwe katika ngazi zote za uchaguzi, yaani katika nafasi ya Urais, nafasi ya Ubunge na Chaguzi za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, hii ni kutokana na sababu zifuatazo:-

Haki ya kupiga kura au kupigiwa kura ni haki ya msingi kikatiba kwa kila Mtanzania. Hivyo, kuwalazimisha watu kujunga na vyama vya siasa ili wawe na haki ya kuchaguliwa itakuwa sawa na kuwanyima haki yao hiyo ya msingi.

Ni Watanzania wachache ambao ni wanachama wa vyama vyaa siasa. Hivyo basi, kuwalazimisha Watanzania kijiungu na vyama vyaa siasa, inainyima Tanzania kupata viongozi wazuri ambao hawapendi kuwa katika vyama vyaa siasa.

Nchi nyingi duniani na hata za kiafrika, kwa sasa zinaruhusu mgombea binafsi, kwa mfano, Ghana, Namibia na Rwanda. Kwa msingi huu, haitakuwa suala jipya iwapo Tanzania nayo itaruhusu mgombea binafsi katika nafasi mbalimbali za uchaguzi.

Nikirejea ripoti iitwayo “*Report of Short term Consultancy on Electoral Law and Procedure of Tanzania*” ya mwaka 1995, iliyotolewa na Tume Maalum iliyoongozwa na Profesa Mgongo Fimbo, (Mhadhiri Mwandumizi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam), uliyoiteua mwenyewe Mheshimiwa Spika, ukiwa Waziri wa Katiba na Sheria wakati huo, ililiangalia suala hili na kutoa mapendekezo yanayofaa na ya msingi kabisa kama yatafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa 12 wa Ripoti hiyo ilipendekezwa yafuatayo:-

Mabadiliko yanayofaa ya Katiba yafanywe ili kuruhusu mgombea binafsi katika nafasi ya Urais, Ubunge na uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

Mgombea binafsi asiwe mwanachama wa chama chochote kilichosajiliwa au kisichosajiliwa mwaka mmoja kabla ya uchaguzi.

Mgombea binafsi katika nafasi ya Ubunge lazima aungwe mkono kwa kupata sahihi (*signatures*) za angalau asilimia tano ya wapiga kura katika jimbo; nusu wakiwa wanawake na nusu wakiwa wanaume. (*Makofi*)

Mgombea binafsi katika nafasi ya Urais lazima aungwe mkono wa angalu asilimia 5 ya wapiga kura kutoka angalau mikoa kumi ya Tanzania Bara na mikoa miwili ya Zanzibar. Je, mapendekezo haya yalifanyiwa kazi kwa kiasi gani? Ili kuhakikisha haki ya msingi ya kuchagua na kuchaguliwa, hatuna budi kuruhusu mgombea binafsi. (*Makofi*)

Katiba ya Ghana ya 1992, ibara ya 28(4) na Sheria ya Uchaguzi, 1993 vifungu vyaa 178 na 184 vinaruhusu kuwepo mgombea binafsi.

Vile vile Katiba ya Namibia, ibara ya 28(4) na Sheria ya Uchaguzi 1992, kifungu cha 34, zinaruhusu suala la kuwa na mgombea binafsi.

Mahakama zetu pia zimeonyesha ukomavu wa hali ya juu kwa kutengua kipengele cha 39(1)(c) cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano, kinachomlazimisha mtu kushiriki katika chaguzi mbalimbali kwa kuititia dhamana ya chama. Inasikitisha kuona kwamba, serikali badala ya kutekeleza hatua hii muhimu ya upanuzi wa demokrasia katika nchi yetu, imeamua kukata rufaa.

Kambi ya Upinzani inaamini kwamba, rufaa hii ni mkakati wa dhahiri wa kuchelewesha mabadiliko haya muhimu ya kikatiba.

Mheshimiwa Spika, zipo sekta mbalimbali za umma nchini, ambazo kwa makusudi serikali imekuwa ikizifanyia maboresho ili ziweze kutoa huduma bora kwa jamii. Miiongoni mwao ni Sekta ya Afya, Kilimo, Maji na hata Sekta ya Sheria. Masikitiko yangu yapo katika Maboresho ya Sekta ya Sheria. Maboresho haya yamekuwa yakifanywa kwa kasi ndogo na hayaendelei. Mpango wa Maboresho ya Sekta ya Sheria ni muhimu sana katika kuhakikisha Utawala Bora, utoaji na upatikanaji wa haki kwa wakati, hifadhi ya haki za binadamu na mfumo bora wa uchumi, kwani sekta ya sheria kimsingi ni sekta kiongozi katika taifa lolote lile, kwa kuwa ni sekta mtambuka na utendaji kazi wa sekta zote unategemea sheria nzuri na mfumo mzima wa utoaji haki. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, katika utafiti wangu, nimegundua kuwa, maboresho ya sekta hii yanakabiliwa na matatizo mengi ikiwemo sera yake kutozingatiwa ipasavyo, kutokuwepo utaratibu maalum wa kufadhili maboresho, lakini hasa tatizo ni matumizi ya *World Bank Procurement Regulations and Procedures*. *Procedures* hizi hupelekea kuwepo mlolongo mrefu na ukosefu wa uwazi.

Mheshimiwa Spika, kuna mkanganyiko juu ya taratibu sahihi za kufuatwa baina ya zile za Benki ya Dunia, kama ilivyoelezwa hapo juu na zile za *Public Procurement Act, 2004*.

Hili pia linapelekeea utekelezaji wa Mpango huu kutokuwa na ufanisi, kwani ni wazi kuwa, *faster procurement leads to faster programme implementation*. Hali hii inaonyesha kuwepo utegemezi uliokithiri wa taratibu za Benki ya Dunia, jambo ambalo sio muhimu kwani hata hizo *World Bank Procurement Guidelines* zinaonyesha ni manunuvi gani yanatakiwa yafuate taratibu hizo na yepi yasifuate. Mfano, kwa mujibu wa Sheria ya Manunuvi ya Umma 2004, chini ya kifungu cha 4(1)(a) na (b); Serikali inatakiwa kuzingatia matakwa ya mkataba au makubaliano kati yake na taasisi za fedha, nchi wahisani au washirika wa maendeleo iwapo Sheria ya Manunuvi ya Umma ya Tanzania inakinzana na mkataba husika. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kifungu hiki pamoja na 4(1)(b), vinaeleza kuwa, kwa hali yoyote manunuvi yatafanywa au yataendeshwa kwa kuzingatia Sheria hii ya Tanzania ingawa hakikuonyesha kuhusiana na mikopo na *credit agreements* ya aina hii, ambayo Tanzania imeingia na *World Bank* katika kuendeleza sekta hii.

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine la msingi ni kutokuwepo uwazi juu ya nafasi ya vyombo vyta manunuvi vyta serikali. Hili linapelekeea mkanganyiko, ucheleweshaji wa manunuvi na kuhusisha mamlaka mbalimbali ikiwemo bodi za zabuni za Wizara. Mfano, inatokea wakati fulani nyaraka za manunuvi ambazo zinatangaza zabuni, zinakubalika na Bodi ya Zabuni ya Serikali lakini zinakataliwa na Benki ya Dunia. Je, hii ina maana kwamba Bodi hizi za Zabuni ni kwa ajili ya ku-rubber stamp maamuzi ya manunuvi tu?

Hii inaonyesha kuwa, *Ministerial Tender Boards* hazina nafasi yoyote katika hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka serikali ichukue hatua za makusudi na haraka, kuhakikisha kwamba, Mpango huu unakuwa na ufanisi na lengo la kuasiwi kwake linafikiwa. Kama tatizo linatokana na Sheria yetu ya Manunuzi ya Umma; ni muhimu irekebishwe ili mipango na miradi yetu isishindwe kuendelea kwa sababu ya kuingiliwa kati na taratibu za taasisi za fedha, nchi wahisani au washirika wa kimaendeleo, kutokana na kutupatia kwao mikopo na ruzuku. Kweli sisi ni maskini, lakini umaskini wetu usiwe sababu ya kupangiwa kila kitu na kushindwa kutekeleza sera na mipango yetu ipasavyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Suala la uanzishaji wa Mahakama ya Kadhi ni jambo la msingi na lisiloepukika kwa sasa. Ilani ya Chama cha Mapinduzi iliona umuhimu wa Mahakama hiyo. Hii ni kwa sababu, kutokuwepo kwa Mahakama hiyo ni kikwazo katika utatuvi wa masuala ya msingi yanayowahusu Waislam. Utetezi wa Mahakama hii ni kutokana na msingi kwamba, kuna uthibitisho wa wazi kwamba, yapo mambo maalum yanayohitaji kuwepo na kushughulikiwa na Mahakama Maalum; mfano, kwa sasa kuna Mahakama za Biashara, Mahakama za Ardhi, Mahakama za Kazi, hivyo Mahakama ya Kadhi itakuwa ni sawa na kuwa na Mahakama Maalum kama hizo nilizozitaja.

Mheshimiwa Spika, msingi mwingine pia ni kuwa Mahakama ya Kadhi kwa Tanzania sio suala la kuianzisha bali itakuwa ni suala la kurudisha tu baada ya kuondolewa kwa muda, kwani ilikuwepo hata kipindi cha ukoloni. Kuna hoja mbalimbali zinazotolewa kupinga kuwepo kwa Mahakama ya Kadhi mionganoni mwa Watanzania. Baadhi ya hoja hizo ni kuwa:-

Kuanzishwa kwa Mahakama ya Kadhi kwa kutumia Sheria ya Bunge itakuwa ni kuvunja au kwenda kinyume na Katiba ya nchi. Hoja hii hutetewa kwa maelezo kuwa, Serikali ya Tanzania haina dini, hivyo kuwepo mahakama hiyo itakuwa inakwenda kinyume na vifungu 107(a), 3, 9(a), (f) na (h), 13 na 19 vya Katiba ya Jamhuri ya Muungano, ambavyo vinapinga na vinazuia kuanzishwa kwa chombo chochote cha Sheria chenye misingi ya kibaguzi. Tafsiri ya vifungu hivi inayotolewa kutetea hoja hii si sahihi kwa sababu ni kweli Serikali haina dini, lakini raia au wananchi wana dini zao na wanaruhusiwa kuabudu na kufanya mambo yao kwa mujibu wa misingi ya dini zao.

Hoja hii ni dhaifu, kwa msingi kwamba, nchi nyingine jirani na za Kiafrika zina Mahakama ya Kadhi kwa muda mrefu sasa na mahakama hizo hazijaleta udini mfano, Kenya, Rwanda na Uganda. Hata Tanzania ilipokuwepo Mahakama hiyo, hapakuwa na Ubaguzi wowote. Kwa mfano, Sheria ya Ndoa ya Tanzania ya Mwaka 1971, inaeleza wazi kwamba, ndoa zifungwe kwa kutumia au kufuata misingi na taratibu za sheria za Kiislam, Kikristo, Kimila au Kiserikali. Vile vile talaka zinatolewa au zinathibitishwa na Mahakama nchini, lakini baada ya kuitia BAKWATA au Mabaraza ya Makanisa.

Kimsingi, Mahakama ya Kadhi haitakuwa inavunja Katiba kwa sababu Mahakama hiyo itaanzishwa kwa kufuata Sheria; itatumia Sheria za nchi zikiwemo

Sheria za Kiislamu ambazo zinaruhusiwa kutumika kama inavyosema *Judicature and Application of Laws Act, Cap. 358 2002, Section 2 (JALA)* na chini ya Sheria ya Mwenendo wa Madai ya Mahakama za Mwanzo. Mfano halisi ni mfumo wa mahakama hizo uliopo Zanzibar chini ya *Kadhi's Court Act, 1985* katika kifungu cha sita kinatoa wazi mamlaka ya Mahakama hizo, ambayo ni mambo yanayohusu ndoa, talaka, mirathi na matunzo ya watoto katika kesi ambazo wahusika wote ni Waislam na walioowana kwa mila na desturi za Kiislam.

Mheshimiwa Spika, wakati wa kuwa na Mahakama hiyo umefika na hoja zote za kuipinga hazina msingi; hivyo hatua za haraka zichukuliwe ili kuhakikisha Mahakama hiyo inaanzishwa haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kwamba, CCM ilizunguka nchi nzima katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2005 ikiomba kura, kwa ahadi kwamba, itairudisha Mahakama ya Kadhi. Kura wamepata; ni jukumu lao sasa kutekeleza kile walichokiahidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Chaguzi za Serikali za Mitaa kuendeshwa na kusimamiwa na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa badala ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi ni kukejeli demokrasia na mifano hai tumekwishaitoa mara kadhaa; mathalan barua ya Mkurugenzi wa Manispaa ya Singida Bernadeta Kinabo kwa Watendaji na *WEOs* wote ya 2005, akiwaonya Watendaji wasishirikiane kwa namna yoyote ile na Kambi ya Upinzani; vinginevyo, watachukuliwa hatua za kinidhamu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Katiba yetu inatuongoza katika misingi ya demokrasia na Utawala wa Sheria, lakini chaguzi hizo kwa hivi sasa haziko huru na haki haitendeki. Tukiangalia Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa (*The Local Government Election Act, Cap 292*), ambayo inaweka mazingira ya uchaguzi kuendeshwa na kusimamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu ni sawa kabisa kuiruhusu Serikali kuwa Mchezaji na Muamuzi (refarii), kwa wakati mmoja katika uwanja wa mapambano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali itoe majibu kwa nini Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa isifutwe na chaguzi hizo zisiendeshwe na Tume ya Taifa ya Uchaguzi katika mazingira hayo? Wakurugenzi wanajipa mamlaka ya kufuta matokeo ya uchaguzi pasipokuwa na mamlaka. Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, inajulishwa haichukui hatua; ni chaguzi gani hizi zinazofuata matakwa ya mtu mmoja mmoja? Je, kwa mtindo huu Tanzania itajiita kweli ni nchi inayofuata Utawala wa Sheria? Japokuwa suala hili lipo chini ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, lakini kinachovunjwa ni Sheria ya Nchi.

Mheshimiwa Spika, msingi mkuu wa demokrasia na Utawala Bora duniani ni kuwa na Serikali inayowajibika kwa wananchi na viongozi wanaowatumikia wananchi kwa uadilifu katika kuwapatia maendeleo na maisha bora. Hii ni kwa sababu uongozi ni dhamana na madaraka yanapaswa kutumiwa kwa manufaa ya wananchi wote na si kwa maslahi ya watu binafsi au kikundi fulani cha watu.

Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu litakubaliana nami kwamba, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma ni chombo muhimu sana katika kuhakikisha Utawala Bora. Hii ni kwa sababu chombo hiki kina mamlaka ya kisheria chini ya ibara ya 132 ya Katiba na kazi yake ni kuchunguza tabia na mwenendo wa kiongozi yeoyote wa umma ili kuhakikisha maadili ya viongozi wa umma hayakuukwi, ikiwemo kuепusha kiongozi kuweka maslahi binafsi mbele.

Pia chini ya kifungu cha 18 cha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma (*The Public Leadership Code of Ethics Act, Cap 398*), sekretarieti hii imepewa mamlaka ya kuanzisha na kuendesha uchunguzi juu ya ukiukwaji wa maadili ya viongozi, lakini kama kawaida, Tanzania huwa inaanzisha kitu kizuri lakini hakiwezeshwi wala hakipewi nafasi kufanya kazi kwa ufanisi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kutokana na malalamiko na matukio ya ufisadi dhidi ya viongozi wakubwa hapa nchini, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali itueleze kama Sekretarieti hii ipo hai au imekufa na je, Kiongozi anapokiuka maadili, inatosha kwa kiongozi huyo kujiuzulu kutoka nafasi moja na kubaki katika nafasi nyingine? Je, Sekretarieti hii inasimamiaje utekelezaji wa sheria hii?

Kambi ya Upinzani inaomba ijue idadi ya viongozi waliokwishatiwa hatiani na Sheria hii au tokea Sekretarieti hii iundwe; hakuna kiongozi aliyekosa Maadili? Je, sote hapa Bungeni tupo safi? (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, moja ya masharti ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma ni viongozi hao kutoa au kuwasilisha tamko rasmi la maandishi, linaloorodhesha mali na rasilimali zake; je, ni kwa kiasi gani viongozi wanatekeleza hili? Kwa mujibu wa Gazeti la *THIS DAY*, toleo la tarehe 3 Julai, 2008, inaelezwa kuwa, hata hapa Bungeni baadhi ya Wabunge na Mawaziri hawajazi fomu zao au hawazijazi fomu hizo kwa wakati. Kambi ya Upinzani inaomba kujua kuna ukweli gani kuhusu taarifa hiyo na kama ni kweli Waheshimiwa hao wapo juu ya sheria (*above law*)? (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo yote, Sekretarieti hii inafanya kazi katika mazingira magumu sana. Serikali imeipuuza na kuifanya isiweze kufanya kazi ipasavyo. Hivi sasa ina upungufu mkubwa wa wafanyakazi ambapo kwa mwaka 2005/2006, ilikuwa na wafanyakazi 55 na mwaka 2007/2008, wanao wafanyakazi 115 ambaa ni wastani wa wafanyakazi kumi kila Kanda (Kanda maana yake ni mikoa mitatu). Idadi hii haiwezi kupelekea chombo hiki kufanya kazi ya kuridhisha. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, tunashuhudia idadi ya viongozi inavyoongezeka nchi nzima. Hivyo, ofisi hii bila kuwezeshwa ili iweze kuwafuata viongozi nchi nzima, ufanisi utakuwa mdogo sana. Hivi sasa Sekretarieti imeanza kufanya *Random Check* kwa baadhi ya viongozi nchi nzima, hata mimi nilipata barua kuwa watakuja lakini mpaka leo sijawaona.

Mheshimiwa Spika, ukaguzi wa aina hii utasaidia sana kwa viongozi kuogopa kukiuka maadili na fomu zitajazwa kwa ukweli. Rais Kikwete katika hotuba yake ya

kuzindua Bunge Desemba, 2005, aliiomba Sekretarieti hii iieleze jamii kuhusu matamko ya viongozi na yahakikishwe kwamba matamko hayo ni ya kweli, lakini hadi hii leo hilo halijafanyika. Kambi ya Upinzani inaomba kuja kwa nini hilo halijafanyika?

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inashauri kuwa, sekretarieti hii ifanye majukumu yake ipasavyo na isisite kuchukua hatua zinazofaa kwa wale wote wanaokiuka Maadili ya Viongozi wa Umma kama Rais Kikwete alivyoagiza.

Mheshimiwa Spika, *Registration, Insolvency and Trusteeship Agency (RITA)*, Wakala huu kwa sasa umeshakuwa na mtandao mzuri katika kusajili na kutoa vyeti nya vizazi na vifo nchini. Kwa mantiki hii, inaonekana kuwa ni chombo pekee kinachowezza kutoa takwimu bora na sahihi zaidi za Watanzania. Kwa msingi huo basi, wakala huu unaweza kupewa uwezo ili uhusike moja kwa moja katika utoaji wa vitambulisho nya uraia (*National Identities*), hati za kusafiria (*Passport*) na kuboresha daftari la wapiga kura (*Register of Voters*).

Inasikitisha kuona hati za kusafiria zinatolewa na Idara ya Uhamiaji, Daftari la Wapiga Kura linatolewa na Idara Ofisi ya Waziri Mkuu, Vitambulisho nya Uraia vinatolewa na wakala mpya na vyeti nya kuzaliwa na vifo tu ndio vinatolewa na RITA, wakati habari zote za kupata *Passport*, kurekebisha Daftari la Wapiga Kura zinapatikana Ofisi ya RITA. Kwa nini Tanzania tusiwe na utaratibu mzuri wa kuhuishaji mambo, hata pale uhuishaji huo unapokuwa na manufaa makubwa kwa Taifa?

Mheshimiwa Spika, hali hii inaashiria matumizi mabaya ya rasilimali za taifa na inapelekea mlolongo mrefu na usumbufu usio wa lazima. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuangalia upya maamuzi yake yasiyo na tija kwa Taifa na sasa kuifanya RITA kuwa ndio wakala pekee kupewa majukumu yaliyoainishwa hapo juu, jambo litakalo leta tija katika nyanja zote za matumizi ya rasillimali za walipa kodi.

Meshimiwa Spika, *Sheria ya Adoption (The Adoption of Children Act, Cap 335 RE 2002)* ni sheria muhimu sana katika kuhakikisha maendeleo na ustawi wa mtoto, lakini utaratibu uliowekwa na Sheria hii ni kikwazo katika kuhakikisha mtoto anapata wazazi kwa haraka. Hii ni kwa sababu inaweka mlolongo mrefu wa kupatikana amri ya *adoption*, kwani ni Mahakama Kuu pekee ndio imepewa mamlaka ya kusikiliza mashauri ya *adoption* na kutoa maamuzi. Urasimu huo unatisha, tunasikia eti sababu ni kwamba, Serikali inaogopa *Human Trafficking*, lakini mtu mpaka akienda Mahakamani kuomba *adoption* ya mtoto, basi huyo hana nia mbaya.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inapendekeza kuwa, Mahakama za chini kama vile za Wilaya na za Hakimu Mkazi, zipewe mamlaka ya kusikiliza na kutoa maamuzi ya *adoption* ili kurahisisha mtoto kupata wazazi haraka. Mfumo huu pia ndio unaotumika katika nchi nyingi kwa sasa, hata majirani zetu Kenya na Uganda wameteremsha *adoption* kusikilizwa na Mahakama za Chini ili kurahisisha mtoto apate wazazi. Inasikitisha kwa Tanzania kuona shauri la *adoption* linachukua miaka miwili hadi mitatu kabla halijamalizika na kutolewa maamuzi. Tuwaonee huruma watoto.

Mheshimiwa Spika, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, imeweka Mahakama Maalum ya Katiba (*Constitutional Court*), katika mfumo wa mahakama nchini. Kambi ya Upinzani inataka kufahamu Mahakama hii imekwisha kufanya Vikao mara ngapi na kuamua mambo mangapi tangu ilipoanzishwa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano na ni mambo gani yameshughulikiwa hadi leo au ndiyo kusema hapajawahi kutokea jambo lililohitaji Tafsiri ya Mahakama hii tangu Muungano ulipoanza? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vile vile inashangaza kuona Katiba yetu ina mamlaka finyu sana kwa mahakama hii kwa kule kuipa uwezo wa kushughulikia migogoro ya kikatiba kwa jambo ambalo litabishaniwa baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tu. Nchi nyingi duniani, zina Mahakama za Katiba ambazo mara nyingi huwa ndizo za juu kabisa hasa katika mambo yote ya kikatiba. Mfano, Afrika ya Kusini, chini ya kifungu cha 166 na 167(3) vya Katiba ya nchi hiyo, inaweza Mahakama ya Katiba kuwa ndiyo ya juu katika matatizo yote ya Katiba. Ni mahakama ya kudumu na ina majaji wa kudumu.

Vile vile mahakama hii ipo nchini Ghana, Zambia, Kenya na sio katika mfumo kama huu wa Tanzania. Je, jinsi kila kukicha kunapotokea mambo yanayohitaji ufanuzi na au tofauti za tafsiri hadi watu wanataka kuandamana, si jambo jema iwapo Mahakama hii ikawa sasa ya kudumu na ikashughulikia migogoro hii kabla haijawa mikubwa?

Mheshimiwa Spika, bahati nzuri siku ya Alhamisi ya tarehe 3 Julai, 2008, Waziri Mkuu alitamka ndani ya Bunge hili kwamba, Zanzibar sio nchi. Tarehe 9 Julai, 2008, Mheshimiwa Iddi Pandu Hassan, Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, alisema katika Baraza la Wawakilishi la Zanzibar kwamba, Zanzibar ni nchi. Je, huu sio mgogoro wa kutosha wa kuonyesha haja ya kuwepo Mahakama ya Katiba?

Hili sio jambo la kusema litatatuliwa na tafsiri ambayo itatolewa kwa mashirikiano ya Wanasheria Wakuu wawili, yaani yule wa Zanzibar na wa Jamhuri ya Muungano, kwa sababu ni mgogoro wa kikatiba ambapo Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaelekeza litatuliwe na Mahakama ya Katiba ya Tanzania. Vile vile jambo hili sio suala la kujadiliwa na CCM kama alivyotamka Mheshimiwa Waziri Mkuu katika Bunge lako Tukufu, ikizingatiwa kuwa Tanzania siyo mali ya CCM wala ya wana-CCM pekee. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaona kwamba, kuna haja ya kuboresha Mahakama hii ili iwe ya juu katika mfumo wetu wa mahakama nchini ili ishughulikie na kutafsiri mambo ya msingi ya kikatiba, yanayohusu Taifa la Tanzania. Hivi sasa kuna mambo ya msingi yanayohitaji Mahakama ya Katiba. Kwa mfano:-

- (a) Tafsiri ya Mambo ya Muungano, yaani kama Zanzibar ni nchi au sio nchi.
- (b) Suala la Mahakama ya Kadhi.

(c) Suala la Zanzibar kujeungu na *OIC*, ambalo lilipata kusikilizwa na kuamuliwa na Mahakama Kuu ya Tanzania katika kesi ya Mwalimu John Paul Muhozya V/S Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaomba kujua hatua aliyochukuliwa yule Mgambu wa Jimbo la Solwa, Shinyanga Vijijini, aliyemuweka Mama Mjamzito katika Selo, pamoja na wanaume na akajifungua ndani ya Selo hiyo eti kwa sababu mumewe hajalipa mchango wa kujenga shule. Kashfa hiyo ilitajwa hapa Bungeni na Mheshimiwa Ania Chaurembo tarehe 24 Juni, 2008.

Mheshimiwa Spika, nawaomba wanawake wenzangu ambao ni wanaharakati wa kutetea haki za wanawake, walifuatilie suala hilo kwa kushirikiana na Tume ya Haki za Binadamu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, pia naamini kwamba, Waziri Mkuu ambaye ni Mwanasheria; Mwanasheria Mkuu; Waziri wa Katiba na Sheria; pamoja na wewe Mheshimiwa Spika, tukishirikiana na Wanasheria wenzetu waliomo humu Bungeni na waliko nje ya Bunge hili, tusilifumbie macho suala hili. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Mwaka jana Waziri wa Katiba na Sheria alikiri upungufu wa Wanasheria nchini. Tukategemea kuanzishwa kwa *Law School* kutaongeza wanasheria lakini sheria inayoanzisha *Law School of Tanzania* ya mwaka 2007 inazidi kuchochlea kuendelea kwa upungufu huo ingawa ilisemwa kuwa lengo la kuanzishwa kwake ni kuboresha sekta ya sheria kwa kuwapatia wanasheria wa hapa nchini mafunzo bora ya vitendo yanayoendana na mazingira ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, hii ni kwa sababu sheria hii inapiga marufuku kwa wahitimu wa shahada ya kwanza ya sheria kutoka Vyuo Vikuu mbalimbali nchini, kutoajiriwa katika taasisi za umma kabla hawajapata mafunzo ya mwaka mmoja kutoka *Law School*. Lengo la kupata Wanasheria wengi halitafikiwa, endapo sharti la kupata ajira ni lazima kupita *Law School* kwa sababu zifuatazo:-

(a) Hivi sasa hakuna *Law School* inayoweza kuchukua wahitimu wa shahada ya sheria kutoka vitivo kumi vya sheria vilivyopo Tanzania na kupata mafunzo hayo kwa wakati mmoja.

(b) Bodi ya Mikopo inaondoa uwezekano wa wanafunzi hao kupewa mikopo kutokana na *nature* ya mafunzo hayo.

(c) *Law School* yenyewe mpaka sasa haina majengo yake, inatumia majengo ya UDSM ambapo haiwezi kuchukua idadi kubwa ya wanafunzi wanaozidi mia tano.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaona hili ni tatizo katika taasisi hii muhimu nchini na inapendekeza yafuatayo yafanyike:-

(a) Mfumo wa *Law School* uliopo sasa ubadilishwe na kila Chuo Kikuu kinachotoa shahada ya sheria, kiendeshe mafunzo haya na baadae kuwe na mtihani wa pamoja wa *Law School* kwa wanafunzi wote.

(b) Mafunzo ya *Law School* yawe ni sehemu ya mafunzo ya shahada ya kwanza na gharama zake zitolewe kama sehemu ya gharama za shahada ya kwanza na ziwe chini ya Bajeti ya Wizara ya Sheria na Katiba.

(c) Serikali iboreshe miundombinu ya Chuo cha Mahakimu cha Lushoto na kitumike kama sehemu ya kuendeshea mafunzo hayo.

(d) Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ifanyiwe marekebisho ili kuruhusu wanafunzi wa Taasisi hiyo wapate mikopo.

Mheshimiwa Spika, suala la kuwepo na utekelezaji wa hukumu ya kifo lina upinzani mkubwa duniani na nchi nyingi zimefuta adhabu hiyo, bado Tanzania inabaki katika mfumo wa adhabu ya kifo kwa kunyonga. Kambi ya Upinzani inapendekeza sheria hii ifutwe, kwa sababu adhabu ya kifo si adhabu ya kibinadamu. Hakuna uthibitisho kuwa adhabu hiyo inasaidia kupunguza makosa ya jinai katika jamii, kwani inaonekana pamoa na kuwepo na adhabu hiyo ya kifo, idadi ya mauaji haijapungua.

Watalaam wanasema, adhabu ya kifo siyo nzuri kwa sababu mtu anayetoa hukumu ya kifo na yule anayetekeleza hukumu hyio, wote hao wanakuwa wameingia katika kosa la mauaji na mkosaji hatakuwa amejifunza chochote kwani atakuwa amekufa.

Mheshimiwa Spika, Kuendelea kubaki na adhabu ya kifo karibu tutabaki kama Kisiwa na nchi zipatazo 133 zimeshafuta hukumu ya kifo. Hivi sasa bado nchi 64 tu ambazo hazijafuta adhabu hiyo, Tanzania ikiwa mojawapo ya nchi hizo.

Mheshimiwa Spika, Tanzania kwa miaka 13 iliyopita, hakujatekeleza hukumu ya kifo na zaidi ya watu 400 walikaa wakisubiri adhabu hiyo. Katika Utawala wa Mheshimiwa Rais Mkapa, hakusaini utekelezaji wa hukumu yoyote ya kifo. Mwaka 2002 alibadilisha hukumu za watu 100 ambao walihukumiwa kifo, akawapunguzia adhabu hiyo ili wapate vifungo vya maisha na kufanya idadi ya hukumu za kifo 500 zilizobadilishwa kuwa vifungo vya maisha katika kipindi cha utawala wake. Inaelezwa hata katika utawala wa Rais Ali Hassan Mwinyi, alisaini utekelezwaji wa hukumu ya kifo kwa watu/wafungwa 21 tu, ambao walinyongwa mwaka 1994. (*Source: Sunday News 15 July, 2008, Ukurasa wa 8*).

Mheshimiwa Spika, hata Marais wamegundua kuwa, hukumu ya kifo imepitwa na wakati. Sasa hebu tuwapunguzie Marais kazi ambayo kimsingi sio ya kwao, yaani kutengua hukumu na kuweka kifungo cha maisha. Waziri alitueleza kwamba, yapo majadiliano ya kina yanayoendelea ya kufuta hukumu ya kifo, lakini huenda yakachukua hata miaka 20.

Mheshimiwa Spika, naomba nilikumbushe Bunge lako Tukufu kwamba, adhabu ya Kifo ambayo imo katika Kanuni ya Adhabu na pia imo chini ya Sheria ya Usalama wa Taifa ni kati ya zile sheria 40 ambazo Tume ya Nyalali (Mungu amlaze pema),

ilipendekeza zifutwe ni adhabu ambayo haimsaidii aliyeua, aliyeuliwa wala haiisaidii Serikali kuondoa makosa kama hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwaka 2006 ulifanywa utafiti kuhusu adhabu ya kifo, asilimia 68 ya waliohojiwa waliipinga hukumu hiyo. Pia Mahakama za Tanzania katika kesi mbalimbali ilishaamua kuwa, hukumu ya kifo ni mbaya.

Mheshimiwa Spika, katika nchi nyingi duniani, teknologia ya *ICT* hutumika hata katika kuendesha mashauri ikiwemo kutafuta na kupokea ushahidi, lakini kwa Tanzania hili linaonekana ni gumu. Jaji Mkuu wa Tanzania, Mheshimiwa Agustino Ramadhan, alinukuliwa katika makala moja inayoitwa *Technological Advancement to Streamline the Judiciary* akisema matumizi ya *ICT* katika utoaji haki (*administration of justice*), bado yapo katika hatua za chini kabisa na inapaswa kuangaliwa kwa makini.

Mheshimiwa Spika, naomba ninukuu maneno ya Adish Aggrawal (*The President of International Council of Jurists and Chairman of all India Bar Associations*) alisema: “*Judicial system need to be well equipped with new technological know how to deliver better services to the public. These new technologies offer opportunities for judicial System to render justice more accessible, transparent and effective.*” (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani ina kiu ya kuona Mahakama zetu zinafanya mabadiliko ya haraka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni muda mrefu sasa vyombo vya habari vimekuwa vikiripoti juu ya taarifa za kuuwawa kwa makundi fulani ya wanajamii kama vile Maalbino na Vikongwe. Siku ya tarehe 3 Julai, 2008, Mheshimiwa Mbunge wa Tandahimba alieleza wakati akiuliza swali kwa Waziri Mkuu kuwa, kumetokea aina nyingine ya mauaji ya wanawake kwa kukatwa makoromeo. Hii inaonyesha jinsi watu wasivyoreshimu Sheria za Tanzania na kutothamini maisha ya watu wengine. Sina hakika kuwa, Wizara ya Katiba na Sheria kuititia taasisi zake, imeifuatilia kadhaa hii. Kambi ya Upinzani inaomba kupata Takwimu kamili ya watu waliopoteza maisha yao.

Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze Waziri Mkuu, pale aliposema atalichukulia suala hili kwa uzito unaostahili. Pia Kambi ya Upinzani inaiomba Wizara ya Katiba na Sheria, iwachukulie hatua za hasira (*Drastic Measures*) wale wanaohusika na mauaji hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wabunge wote na wale walioko nje wanaonisikiliza na naomba kuwasilisha. Ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Maghimbi, kwa hotuba yako hiyo.

Waheshimiwa Wabunge, ninao wachangiaji 28 na kama ilivyo utaratibu wetu, tutaanza na wale ambao wamechangia mara chache zaidi kuliko wenzao. Kwa hiyo, wafuataa wataanza: Mheshimiwa Dr. Omari Nibuka Mzeru, huyu hajachangia kabisa

inaonyesha, halafu Mheshimiwa Florence E. Kyendesya, Mheshimiwa Ruth Msafiri na Mheshimiwa Harrison Mwakyembe, ameomba achangie kesho. Kwa hiyo, watatu wa kwanza ni Mheshimiwa Dr. Mzeru, Mheshimiwa Kyendesya na Mheshimiwa Ruth Msafiri. Kabla ya kumaliza au kusitisha shughuli, basi nitatangaza wale wengine watakaoendelea hapo saa 11.00. Nianze na Mheshimiwa Mbunge wa Morogoro Mjini, Mheshimiwa Dr. Mzeru.

MHE. DR. OMARI M. NIBUKA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii na mimi niweze kuchangia katika Wizara hii muhimu ya Sheria na Katiba. Kama ulivyosema, kwa kipindi hiki cha Bunge ni mara yangu ya kwanza kuchangia kwa kauli. Kwa hiyo, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, ningependa nimshukuru sana Mwenyezi Mungu, kwa kunipa afya njema mpaka siku hii ya leo nikasimama hapa kuweza kuchangia. Nakushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia, lakini pia nakupongeza kwa nafasi uliyoipata ya kuwa *President* wa CPA na ninaamini kabisa kama ulivyosema wewe mwenyewe kwamba, heshima hii siyo ya kwako wewe ni heshima ya Watanzania wote na hasa Wabunge wa Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, napenda pia niwashukuru sana Wananchi wa Jimbo langu la Morogoro Mjini, kwa imani walijonipa, lakini pia kwa jinsi wanavyoniunga mkono hadi wakati huu kwa kipindi hiki nilichopo sasa hivi. Nami nawahakikishia kwamba, nitawatumikia kwa nguvu zangu zote bila ya ajizi. *Inshallah*, Mungu atajaalia.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, nataka nizungumzie masuala ya sheria. Sheria maana yake ni utaratibu au makubaliano ya pamoja katika kulinda haki za wanadamu. Kinyume cha hivyo, maana yake ni kuvunja sheria na kwa hiyo ni kosa ambalo halina budi lichukuliwe adhabu inapotokea. Cha kushangaza ni kwamba, Bunge lako Tukufu au huko nyuma ni kwamba, sheria mbalimbali zilikuwa zikitungwa, lakini sheria hizi mara nyingi zilikuwa wakati mwingine hazitekelezwi vizuri au kwa utaratibu mzuri na wakati mwingine zilikuwa zinavunjwa bila utaratibu na wale wanaovunja sheria hizo hawakuchukuliwa hatua zozote, kitu ambacho kusema kweli kinashangaza sana.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu inaendesha utawala wake chini ya mihimili mitatu kwa maana ya Bunge ambalo linatunga sheria, Mahakama inatafsiri sheria pamoja na kuziweka vizuri ziweze kutumika, lakini pia Serikali ambayo inatekeleza sheria hizo. Sasa utakuta watendaji au baadhi ya viongozi wengi katika nchi yetu, wanavunja sheria hizi kwa makusudi kabisa, kitu ambacho ni kosa, lakini bila kuchukuliwa hatua zozote.

Mheshimiwa Spika, ningombaa nitoe sheria angalau moja kwa kuokoa muda. Zipo sheria nyingi, lakini naomba nitoe mmoja tu hasa Sheria ya Ardhi ya Mwaka 1999, Sheria Na. 4 na Sheria Na. 5 ya Mjini na Vijijini, ambayo inazungumzia masuala ya ardhi. Utakuta katika Sheria hii imejieleza wazi kwamba, endapo wananchi wanatakiwa kuondolewa mahali fulani kwa faida ya nchi au kwa faida ya Serikali au kwa faida ya kijiji ni kwamba, wananchi wale ni lazima watekelezewa kama inavyozungumza sheria kwa maana ya kwanza, walipwe ardhi yao, lakini pia walipwe mazao yao kama

yapo, lakini pia majengo yao kama zipo nyumba na vilevile walipwe usumbufu (*Disturbance Allowance*) na mwisho walipwe pango la miaka mitatu.

Mheshimiwa Spika, sasa utakuta wakati wa utekelezaji wa sheria hii, wananchi hawa wanaondolewa utafikiri mifugo ya ng'ombe. Hawajalipwa fidia wala chochote, wanaambiwa ondoka na ninavyojua mimi ni kwamba, fidia itangulie, halafu kuhama kufuate kwa sababu fidia hiyo itawasaidia wao kule wanakokwenda kuanza maisha mapya. Sasa nashangaa, unamwambia mtu aondoke wakati fidia hujampa na fidia hiyo utakapokuja kumpa utakuta mtu yule pengine anapewa 100,000 au 200,000 ambazo hazimsaidii. Kwa hiyo, utakuta ni unyanyasaji kwa wananchi wetu, kitu ambacho hakikubaliki kabisa na hii ni dhambi.

Mheshimiwa Spika, hapa Bungeni, Wabunge wengi sana wamekuwa wakichangia au kulalamika kwamba, katika majimbo yao; wananchi wao ni kwamba aidha hawajalipwa fidia au wamelipwa fidia kiduchu kabisa. Sasa sisi kama tunazungumzia utawala wa sheria ni vizuri tukafuata sheria zetu ili tusijigonge sisi wenyewe.

Mheshimiwa Spika, mimi namshukuru sana Mheshimiwa John Pombe Magufuli, nakumbuka aidha kwenye Kikao cha Bajeti cha mwaka jana au wakati akijibu swalii, alisisitiza sana kuhusu sheria hii ya fidia ya ardhi. Alituambia kwamba ni vizuri Wabunge tukachukua nafasi hii kwenda kuwaelimisha wananchi wetu ili waweze kuzielewa hizo sheria. Mimi kule kwangu nilitoa *photocopies* nyingi, nikawagawia wananchi hasa waliopo kando kando ya Mji ambao kufahamu sheria kwao imekuwa ni vigumu ili angalau akitokea mtu yejote wa kuweza kuwababaisha wajue sheria hiyo ya ardhi inasema nini.

Mheshimiwa Spika, jambo la kuwaondoa wananchi ili ijengwe taasisi au hospitali au chochote, kwanza sio kitu cha dharura ni kitu cha mpango wa kawaida tu. Kwa hiyo, huna haja ya kuwaondoa wananchi kwa haraka haraka katika mazingira ambayo ioneckane kama zimamoto ni kosa.

Mheshimiwa Spika, lakini pia kama Serikali inakuwa haijajipanga vizuri, kwa maana ya kuwalipa fidia wale wananchi, basi isubiri mpaka Serikali itakapokuwa imejipanga ili kusitokee bugudha ya hapa na pale kwa wananchi hao.

Mheshimiwa Spika, zipo sheria nyingi ambazo hazitekelezwi vizuri, lakini hii nimeona niitolee kama mfano katika kuokoa muda wa kuchangia hoja hii.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu inazungumzia sana suala la utawala bora na mimi nashangaa kama Utawala Bora maana yake ni kuvunja sheria za nchi au namna gani. Kwa sababu mimi ninavyojua, Utawala Bora maana yake ni kwanza kuamua kwa kufuata sheria, lakini pia kuwapa haki wale wananchi ambao ndiyo wanaotawaliwa katika nchi ile. Nashangaa sasa kama litakuwa hilo halifuatwi, maana yake sioni hata umuhimu wa hili suala la Utawala Bora.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine nataka nizungumzie kuhusu majengo ya Wizara hii ya Katiba na Sheria hasa idara ya mahakama; inasikitisha sana katika

mahakama zetu utakuta majengo yanatia huruma kabisa; yamechakaa, utakuta *sealing board* zimeoza, makabati hayafungiki mpaka watu wanafunga na makaratsasi, meza na viti vimevunjika na utakuta wakati mwingine viti vingine misumari imechomoza, kitu ambacho pia ni hatari kwa maisha ya wale watumishi na inaweza ikatokea mtumishi akachomwa; huwezi kujua anaweza akapa tetenasi na akafa kwa kitu kidogo tu.

Mheshimiwa Spika, mimi nashindwa kuelewa kwa nini mpaka wakati huu tuliofikia, hatuwezi kuwasaidia watumishi wetu? Kwanza, wanafanya kazi katika mazingira magumu, mishahara midogo, hawana marupurupu lakini hata vitendea kazi bado hatujawajali ni namna gani ya kuwasaidia.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, pale kwangu Morogoro, kwa kweli kuna tatizo kubwa licha ya uchakavu wa majengo, ubovu wa thamani, lakini pia majengo hayatoshi na vyumba havitoshi. Utakuta mahakimu wakati mwingine wanafanya kusubiriana, yaani wanapokezana kwamba mwenzangu endesha kesi kama mbili ukimaliza unipishe nami niingie kwa sababu chumba ni kimoja, mahakimu wapo wawili au watatu; hivi kweli katika utaratibu wa kuzungumza kwamba tuondoe kero za kesi kurundikana mahakamani; tutafanikiwa kweli kwa mtindo huu?

Mheshimiwa Spika, ninachoomba hapa Mheshimiwa Waziri, kwa sababu katika mpango ule wa kuongeza maofisi na kugawa mawakili katika sehemu mbalimbali za nchi sikutikia kuitaja Morogoro; kwa hiyo, naomba hapa anieleze kwa makini sana kwamba; je, Morogoro watatusaidiaje katika hili, kwa sababu ninavyofahamu, Morogoro ni kioo ukiondoa Dar es Salaam inafuata Morogoro? Morogoro ni njia panda lakini pia wanakuja wageni mbalimbali kutoka nchi za nje, sasa ni mahali ambapo panatakiwa paangaliwe tofauti na mikoa mingine ambayo pengine kwenye ramani ukisema unaweza ukahisi labda pengine huu mji uko Zaire au wapi, Morogoro ni kioo cha nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba sana Mheshimiwa Waziri wakati wa kujumuisha, aniambie atatusaidiaje Morogoro katika kutupatia majengo au vyumba vya kutosha kwa ajili ya Mahakamu? Hilo kaka yangu naomba atanisamehe sana wakati wa vifungu.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ni kero kwa wafanyakazi hawa wa mahakama ni suala la masomo, wafanyakazi wa mahakama wengi wanafanya kazi kwa muda mrefu wengine hawapatiwi kabisa nafasi ya kwenda chuoni kuongeza elimu zao, hasa elimu ndani ya kazi kwa maana *inservice course*. Matatizo haya yanakuja kwa sababu mbili; kwanza kabisa, utakuta gharama ya kwenda kusoma wanapopata nafasi ni kubwa; mtu anaambiwa pengine atoe shilingi milioni moja kwa mwaka, mtumishi huyu mshahara wake ni mdogo; shilingi milioni moja kwa mwaka ataipata wapi?

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba angalau wakopeshwe walipe kidogo kidogo au mahakama iangalie jinsi ya kuwapunguzia hii gharama ili angalau waweze kupata elimu, kwa sababu nao ni haki yao vile vile. Jambo la pili, watumishi hawa walioko kazini mara nydingi kabla hawajapata nafasi ya kwenda kusoma, kwa kawaida huwa wanadahiliwa kwa maana ya kufanya mitihani, lakini mitihani hiyo wakati mwingine wanawachanganya na wale wanafunzi au wafanyakazi waliotoka *fresh from school*.

Hawa waliotoka shuleni moja kwa moja, wana nafasi kubwa zaidi ya kupasi ile mitihani na kwenda chuoni na wengine wa zamani wanabaki pale pale.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilichokuwa naomba, kwa vile viongozi wa mahakama wapo hapa ni vizuri wakalirekebisha jambo hili ili hawa wafanyakazi waliopo muda mrefu, wafanyiwe utaratibu mzuri wa kuweza kwenda kusoma kwa sababu nao ni haki yao. Haitakuwa haki kuona wale walioanza kazi juzi wanapanda vyeo siku hadi siku, wakati wao wanabaki pale pale. Kwa kweli hatuwatendei haki, naomba sana wahusika walitilie maanani suala hili.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo naona ni kero ni kuhusu malipo ya wazee wa baraza. Nashukuru hivi karibuni angalau Serikali imejali Baraza la Wazee, hata kama si wote waliopata mafao yao, lakini sasa isiwe kwamba mafao haya katika kupewa iwe kwa zima moto, iwe ni utaratibu ambaao ni endelevu. Kwa sababu hawa wazee hawana kazi nyingine, kila siku wanashinda mahakamani, wanaenda saa moja na nusu asubuhi wanarudi jioni, hawawezi kufanya kazi nyingine yoyote ya kuendesha maisha yao. Sasa kama hawawezi kupata hizi fedha zao, maana pia inawaletea hata kuwa na msukumo wa kuweza kupokea rushwa, kwa sababu sisi binadamu wakati mwingine mtu anafanya dhambi kwa sababu ya shida, ingawa binadamu wengine wanafanya makosa kwa sababu ya mazoea. Binadamu walio wengi wanafanya makosa kutokana na shida walizonazo.

Meshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba wazee hawa wa baraza waendelee kupewa mafao yao ili yaweze kuwasaidia waweze kupata chakula cha kuwalisha wao pamoja na familia zao.

Mahakama ni chombo kinachoendeshwa kwa kutumia sheria na nilivyoona ni kwamba, wazee wengi wanaochaguliwa kuwasaidia mahakimu katika mabaraza, wanachaguliwa kwa umaarufu wao siyo kwa elimu zao, ninachoomba ni kwamba; ni vizuri mahakama ikapanga utaratibu wa kuwaendeleza.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana.

MHE. FLORENCE E. KYENDESYA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii mchana huu ili nami niweze kuchangia hotuba nzuri ya Wizara ya Katiba na Sheria iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, aidha, nampongeza sana Waziri wa Katiba na Sheria, kwa kuandaa hotuba hii nzuri ambayo kama utekelezaji wake utakuwa kama ilivyo kwenye kitabu hiki, nadhani inaweza ikaleta maendeleo mazuri na kutenda haki kwa Watanzania wote, pia nawapongeza watendaji wote alioshirikiana nao.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo na baada ya maeleo hayo, mimi ninayo yangu machache ambayo napenda kujikita hasa kwenye Sheria ya Ubakaji; wanaume wanaowabaka watoto wadogo, wanaume ambaao wanawabaka wanawake na kuwalawiti watoto wa kiume.

Mheshimiwa Spika, nasikia wanasema hata wanawake; wanawake hawawabaki wanawake wenzao ni wanaume ndiyo wanabaka.

Mheshimiwa Spika, napenda kuelezea suala hili hasa kuhusu wabakaji kwamba, sheria ni nzuri lakini pale ambapo mimi napata tatizo kubwa sana ni pale ambapo wabakaji wanapokamatwa wanapewa dhamana na mahakama. Wakati huo mwathirika ameatheririka, wakati mwininge bado yupo hospitali, lakini yule aliyebaka utakuta amepewa dhamana; hii sheria maana yake nini?

Mheshimiwa Spika, inasikitisha sana hawa wanaume utakuta baba mzima au mwanaume miaka 30 – 45, anakwenda kumbaka mtoto wa miaka mitano au mitatu; huu ni unyama na ukatili usiokuwa na huruma yoyote, halafu anapewa dhamana; maana yake nini; sheria ndivyo inavyosema kweli awekewe dhamana?

Mheshimiwa Spika, hata huruma hawana ni unyama wa hali ya juu, mimi naomba hili lifanyiwe marekebisho, waangalie wafanye marekebisho kwamba, hawa watu wanaobaka watoto wadogo na wanawake wasiwekewe dhamana hadi hapo kesi yao itakapomalizika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni juzi mfano halisi hapa hapa Dodoma, Siku ya Jumamosi nilikuwa naangalia kwenye luninga nikamwona Mheshimiwa Magreth Sitta, Waziri wa Maendeleo Jamii, Jinsia na Watoto, akiwa Hospitali akimliwaza mtoto mdogo wa kike wa miaka 12 amebakwa na amelazwa hapo. Baadhi ya akina mama aliofuatana nao wakaanza kulia. Nikafuatana pia na Mama Hewa kwenda kumwona yule mtoto, maana yake sisi kama akina mama tulipata uchungu; yule mtoto amebakwa baada ya kubakwa alipomtaja yule aliyembaka, ndugu zake wakachukua kisu wakaweka kwenye moto wakaanza kumchoma na kisu kwenye mikono na miguu.

Mheshimiwa Spika, hawa wamewekewa dhamana na polisi, kuna haki za binadamu gani? Yule mwathirika ambaye mpaka sasa yupo hospitali; hakuna haki za binadamu? Naomba sheria hii jamani iangaliwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mbaya zaidi ambalo mimi linanipa tatizo kubwa ni hii sheria chini ya Bodi ya *Parole*. Sheria hii ni nzuri sana na ninashukuru hapa umewatangaza Majaji na Jaji Mkuu yupo, naomba anisikilize. Hii sheria ni nzuri sana, lakini ingekuwa inaangalia ni mfungwa wa makosa gani anufaika na Bodi hii ya *Parole*.

Tabia ya kuwaachia hata waliobaka, mimi kwa kweli naona hii haifai kabisa. Ninao mfano halisi, naweza nikakaa na Waziri wa Katiba na Sheria, tena nampenda sana, lakini katika hili naona nitakuwa tofauti naye, pamoja na kumpenda kote. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa jihadhari, mke wake yupo hapa hapa anakusikiliza. (*Kicheko*)

MHE. FLORENCE E. KYENDESYA: Ahsante. Nimemwona tena ni Profesa nimemwona, tunampenda wote lakini katika hili mimi hapana. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, mimi naona ingefaa sana hii sheria iangalie ni makosa yapi ambayo hawa wafungwa wanufaikie chini ya Sheria ya Bodi ya *Parole*. Nazungumza hili ambalo ni kweli limetendeka na mimi nikiwa Mjumbe wa Bodi ya Parole, kuna mfungwa mmoja aliachiwa huru, lakini baada ya kufuata taratibu zote za kisheria halafu wanaachiwa huru.

Mheshimiwa Spika, kuna mfungwa alimbaka mtoto wa miaka mitatu, libaba la miaka 45; akafungwa miaka 15 akatumikia jela miaka mitatu, akaachiwa huru baada ya kufuata taratibu zote za Bodi ya *Parole* kama nilivyosema akaachiwa huru. Sasa hii maana yake nini? Libaba lizima la miaka 45, sijui anamshikaje huyo mtoto wa miaka mitatu anavyombaka na *kumtatandura* kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naona hilo la ubakaji limeeleweka, naomba lifanyiwe marekebisho, hiyo sheria iangaliwe upya.

Mheshimiwa Spika, nimefarijika wakati anasoma hotuba yake Mheshimiwa Waziri amesema, Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 inafanyiwa marekebisho na italetwa hapa Bungeni ili iweze kupidishwa. Nashukuru sana kwa sababu mwaka 1971 ni Bunge hili hili lililopitisha hiyo sheria, lakini tukumbuke kwamba, wakati huo wanawake walikuwemo kama watano tu ndani ya Bunge na walipitisha ni wanaume ambao ndiyo wakandamizaji wakubwa kwa wanawake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwaka 1971 nakumbuka alikuwemo Mheshimiwa Jully Maalim na wengine sijui walikuwa watano, pamoja na wale wa kuteuliwa. Sasa tutategemea kwamba, kweli wakati huo wanaume wangeiangalia vizuri hiyo sheria. Wanawake kwa kweli wanakandamizwa sana na wananyanyaswa sana hasa walioko vijijini, ambao hawailewi vizuri sheria.

Mheshimiwa Spika, ilivyo ni kwamba, mara nyingi wanandoa wanapopeana talaka, wanaume wa vijijini wanashahau chombo pekee, chenye uwezo na mamlaka ya kutoa talaka ni mahakama. Wao hawalielewi hilo.

Sisi wanawake mara nyingi hatupendi sana talaka, kwa sababu wanandoa wanapopeana talaka, wanaoathirika ni watoto wasiokuwa na hatia, matokeo yake ni ongezeko kubwa la watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi mitaani na inaleta mzigo mkuwa kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, wanawake wanapoachwa huko vijijini wanaachwa hivi hivi bila kupewa haki zao; kama wamejenga nyumba, wana mashamba, wanaume ni wajanja sana, wana akili wanasema hii nyumba ni mali ya watoto wakati watoto hawakujenga hiyo nyumba aliyejenga ni mama na baba.

Mheshimiwa Spika, naomba sheria hii iangaliwe upya ili wanawake nao waweze kupata haki yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimefarijika pia na hili la ndoa, mfano mwanaume anapotaka kumwacha mke wake hasemi ondoka, anampa kipigo. Ningekuja na hilo gazeti hapa, lakini lisingeonekana kwenye *Hansard*. Tukisoma Gazeti la Mwananchi la tarehe 27 Julai, nawapongeza sana Waandishi wa Habari kulionyesha hilo tendo. Kuna mwanaume mmoja Dar es Salaam, alimpiga mke wake na nondo kichwani, akaanguka chini, akachukua maji ya moto akamuunguza kuanzia kichwani mpaka *Mbeya*. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, maana yake nini? Inaonyesha kabisa kwenye picha, uso umeungua, matiti yameungua, tumbo limeungua mpaka *Mbeya*. Sasa huyu mama akitaka talaka aondoke atamwacha hivi hivi bila kumpa kitu chochote, naomba hili kwa kweli liangaliwe sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu marekebisho ya mirathi amesema atalifanyia marekebisho.

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee kidogo kuhusu Mahakama ya Kadhi. Suala la Mahakama ya Kadhi, naona litatuletea kidogo matatizo.

Mimi kwa maoni yangu, ningeshauri tu kwamba, ni vyema masuala yanayohusu itikadi za kidini yangebaki kwenye taasisi za madhehebu hayo ya kidini huko huko.

Mheshimiwa Spika, nchi hii ina makabila 120; Mkoa wa Mbeya peke yake una madhehebu si chini ya 140, mikoa mingine sielewi. Sasa kama kila dhehebu likihitaji mahakama yake, mimi naona kwa kweli itakuwa vurugu tu hapa nchini. Ningombaa na ningeshauri kwamba, kila dhehebu liendelee na taratibu zake ili Serikali ishughulikie masuala ya ustawi wa jamii tu, kwani kukiwa na Mahakama nyingi kila dhehebu litahitaji mahakama yake, itakuwa ni vurugu.

Tubaki na Katiba tuliyonayo na nchi nyingi zinaheshimu sana Taifa letu kwa utulivu na amani. Nasema hili kwa nia njema tu ndugu zangu kwamba, tungeacha kila dhehebu liendelee na taratibu zake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja asilimia mia kwa mia, lakini Mheshimiwa Waziri angalia hiyo Sheria ya Ubakaji hapo ndiyo sintanyang'anya mshahara wako. Ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, isingekuwa vyema nikaruhusu mchangaji anayefuata kwa sababu haitawezekana kumpa haki yake ya dakika 15 kwa mujibu wa Kanuni. Vilevile si vyema kusema achangie kwa dakika tisa halafu tumpe dakika sita haitapendeza.

Kwa hiyo, kutokana na tatizo hilo la kiufundi na muda wa kusitisha shughuli ulikuwa bado, lakini kwa sababu hiyo ya kiufundi, nasitisha shughuli hizi hadi hapo saa kumi na moja jioni.

Waheshimiwa Wabunge, niseme tu tutaendelea na wafuatao; baada ya Mheshimiwa Ruth Msafiri, atafuatia Mheshimiwa Mpendazoe, Mheshimiwa Steven Galinoma, Mheshimiwa Mohamed Missanga na Mheshimiwa Athuman Janguo na wengine watatajwa baadaye.

(*Saa 06.56 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni*)

(*Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia*)

Mwenyekiti (Mhe. Zubeir Ali Maulid) Alikalia Kiti

MWENYEKITI: Ahsante sana na sasa namwita mchangiaji wetu wa mwanzo kwa jioni ya leo, Mheshimiwa Ruth Msafiri, atafuatiwa na Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe, sawa naambiwa kwamba Mheshimiwa Dr. Mwakyembe atachangia kesho, kwa hiyo atafuatiwa na Mheshimiwa Fred Mpendazoe na Mheshimiwa Stephen Galinoma, ajiandae.

MHE. RUTH B. MSAFIRI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi ya kwanza kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii nikiwa wa kwanza katika mchana wa leo siku ya kwanza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiunga mkono hoja. Nachukua nafasi hii kumpongeza mtoa hoja kwa kuiwasilisha vizuri, nikitambua kwamba kazi hii imefanyika pamoja na wenzake alioshirikiana nao, nawapongeza sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe pongezi zangu za kwanza kabisa za kiuongozi nizipeleke kwa Mheshimiwa Rais wetu kwa jinsi anavyotutetea sisi wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapoyasema haya nitayasema kwa mfano, nitaihusisha hii ni pamoja na uteuzi wa Baraza lake za Mawaziri, ni Baraza ambalo lina wanawake wengi Mawaziri na Naibu wao. Ni suala ambalo kwa kweli linatutia moyo, linatuonyesha kwamba kweli Mheshimiwa Rais anatutetea.

Mhesimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile uteuzi wa Majaji, Mheshimiwa Rais amevunja rekodi kwa kuteua Majaji wengi sana wanawake katika kipindi chake. Hii ni wazi kabisa kwamba amedhamiria kwamba katika vyombo vyaa maamuzi awaweke pia wanawake ambao sisi wote ni mashahidi na ukweli ulio wazi kwamba katika kipindi kirefu na cha miaka mingi vyombo vyaa maamuzi vimekuwa na wanaume, wababa walikuwa wakiamua kwa ajili ya sisi wanawake. Kumbe masuala mengine sivyo ambavyo mwanamke angeamua kwa mazingira yake. Kwa hiyo, nampongeza sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza pia kwa vita kubwa anayoipiga dhidi ya mimba mashulenii. Hakuna namna unavyoweza kumkomboa mwanamke kama hujawenza kumpa elimu. Lakini huwezi ukaacha mtu anayemkatisha huyu mtoto masomo asiweze kupata elimu yake akaendelea kufanya mchezo huo mwaka hadi mwaka mwisho ikawa ni mazoea, halafu ukasema utamkomboa mwanamke. Mimi naunga mkono vita hii na kuiomba Serikali na kuomba kila mmoja katika nafasi yake aliyokuwa nayo, baba, mama, mlezi, mzazi, mwangalizi, kiongozi wa namna yoyote kwa namna yoyote kuhakikisha kwamba anaunga mkono vita hii ya kuhakikisha kwamba tunapambana na mimba za watoto wa kike shuleni ili kuwapa nafasi za kuweza kusoma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, napenda niseme kwamba Watanzania hawajui sheria, wakati ambapo Taifa letu sasa na sisi tunahesabika na tumekwishapiga hatua kwamba utawala wetu ni utawala bora na tunafuata utawala wa kisheria. Lakini ukweli wenye Watanzania hawajui sheria. Nilipota mchango wa maandishi kuchangia kwenye Wizara ya Ardhi, niliwapa mifano kwamba kwa mfano Serikali, Bunge imetunga sheria nyingi tu ambazo tumezipeleka mpaka kwenye Vijiji na Kata. Lakini sheria zile zinatakiwa zitafsiriwe na zitumike na wanasheria. Hakuna mafunzo yoyote yametolewa, lakini unategemea huyu mtu wa kijijini awe Baraza la Kijiji, awe Baraza la Kata eti asimamie haki, kwa kujifunza kwa wapi? Kafundishwa na nani? Kwa vyovvye vile hawezi kutenda vizuri.

Mheshimiwa Waziri alipokuwa ana-*wind up* akatuambia kwamba katika ngazi ya Wilaya, ndipo walipowapata wanasheria amba ni Mahakimu na wengi walikimbilia kazi hizo na hata wakaacha kazi walizokuwa nazoo. Kwa hiyo, inaonyesha kwa kiwango gani ambavyo kweli Watanzania hawajui sheria, Watanzania haki zao zinaporwa na watu wajanja wajanja na hali imekuwa inadhoofisha mambo mbalimbali ambayo yangeweza yakasonga mbele.

Kwa hiyo, haki za Watanzania zimekuwa kwa kweli hazifikiwi. Sasa katika ukurasa wa 48, Ibara ya 81, hapa kwenye Tume ya Binadamu wanasema katika mwaka ujao pamoja na mambo mengine Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora itaendelea kutoa elimu ya Haki za Binadamu na misingi ya utawala bora katika Wilaya 70 na kutoa vipeperushi 50,000 vya kuitangaza kwa lengo la kufahamu kazi zake. Kwa kuitangaza sawa ili ifahamike haki zake. Lakini mimi naona lengo hili liko chini sana, viperurushi hivyo ni vichache sana. Kwenye nchi ya watu milioni 34 unasema utatoa vipeperushi 50,000 ufahamike, haiwezekani. Haiwezekani vitaishia kwenye ofisi chache, havitafika mahali popote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa naomba kwamba pengine tubadilike, tuangalie namna zingine ambazo hazina gharama kubwa. Lakini watu wengi wanazisikiliza, wanazitii na zinawezekana zikafahamisha jambo hili kwa Watanzania wengi. Kwa mfano, kwenye elimu ya msingi, tumewapelekea watoto wa elimu ya msingi, elimu ya UKIMWI. Kwa nini, kwa sababu tuliona kwamba watoto katika umri wa kuanzia darasa la tatu, wanaanza kuathirika na kuhusishwa katika vitendo vya ngono na hata wengine kupata mimba katika umri mdogo. Tumekubali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, imekwenda sekondari na kadhalika. Sasa suala hili ambalo ni la msingi ni kwa nini lisiingizwe katika mitaala yetu ya shule za msingi, katika shule za sekondari na elimu yetu ya watu wazima ikarejeshwa ili kila Mtanzania akawenza kufahamu haki zake za msingi ni zipi tangu anapoanza kuchipukia akiwa mdogo mpaka anapokua ili kuondoa hao wajanja wajanja wanaitwa *ma-bush lawyers* hawa wakati wakiwa wanadanganya watu na kusababisha watu wapoteze haki zao bila kuwa wameweza kuzipata na kumbe ni haki zao, vyombo vya habari vimetusaidia sana. Kwa nini tusiviombe vyombo vya habari, luninga, redio, tukaomba magazeti? Kwa nini wasitusaidie wakatuwekea *ki-page* kwenye magazeti, kiukurasa cha kuwa wanaelimisha kila siku kaeneo kadogo tu, nini maana ya haki za binadamu na ni mambo gani ambayo unatakiwa wewe kuyasimamia na kuyafahamu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile kwa nini tusijipe utaratibu kwa sisi viongozi. Mimi nataka nitoe mfano, kwenye Kanisa langu ninaloabudu mimi kuna Muongozo wa Sala tangu tarehe 1 mpaka tarehe 31 ya Desemba. Kwa hiyo, kwa kila siku nchi nzima mnaofuata muongozo huo mnakuwa mnasoma hilo neno na mimi nasema hivi sisi viongozi Serikali ituwekee muongozo kwamba kwa mwezi, mwezi wa kwanza, mpaka wa tatu, ili tunapokuwa kwenye mikutano yetu, mikutano ya hadhara, mikutano midogo tunayoweza kuchanganya uongozi, tuelimishane maana ya haki hizi ili Watanzania wazijue kwa wakati mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mwaka mmoja tunaweza kufanikiwa kwa kiwango fulani, ili Watanzania waweze kuzifahamu haki zao, lakini wawe na nguvu ya kuzidai, kufahamu peke yake haitoshi. Unaидai haki yako wapi? Watanzania hawajui. Nilikuwa naomba sana kwamba suala hili tulismamie, tulizingatie, kwa nguvu ya kipekee kwa sababu ni vizuri Watanzania wafahamu haki zao na pia wafahamu namna ya kudai haki zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia nizungumzie habari ya upungufu wa Mahakimu. Upungufu wa Mahakimu hata Kamati inayohusika imelieleza, ni kubwa sana katika Tanzania. Tangu nimekuwa Mbunge katika Bunge hili kwa bahati nzuri kipindi changu cha kwanza nilikuwa Mjumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria, tatizo la Mahakimu ni kubwa hata leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nimejaribu kusoma kwa haraka haraka pengine sikulisoma hilo eneo. Lakini kwa mara ya mwisho kulikuwa na upungufu, kulikuwa na Mahakama zaidi ya 1,200 na upungufu ulikuwa ni zaidi ya Mahakimu 600. Sasa ninapoangalia hii, hii kasi ya maandalizi ya kuongeza Mahakimu ni ndogo sana. Chuo cha Lushoto kilikusudiwa pengine kwa ajili ya kuongeza Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sasa naona kimepewa majukumu mengi. Hiki chuo hakitaweza, lakini katika Mahakama ya Mwanzo na katika Mahakama ya Wilaya ni maeneo ya msingi kabisa ambapo hayatakiwi yakose hakimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, inashangaza kuona sasa nitatoa mifano iliyo hai. Hakimu mmoja ana Mahakama mbili, tatu, tano na hata sita, Hakimu huyu mmoja. Ni kitu ambacho hakiwezekani. Hapa hakuna haki na *at least* tunavyofahamu kwamba kwa mwananchi katika ngazi ya Mahakama za Mwanzo ndipo ambapo kuna matatizo mengi sana ambayo yangeweza yakamalizwa na yakaweza yakamalizika. Lakini huku hakuna watu wa kutenda kazi hii. Kwa mfano, nitatoa mfano, kwenye Jimbo la Muleba Kaskazini, tuna Tarafa mbili, Tarafa ya tatu tuna-share na Jimbo la Kusini. Lakini tuna jumla ya Mahakama tatu.

Katika Mahakama zote tatu, sisi tuna hakimu mmoja tu, sijui sasa kwa Muleba Kusini kuna Mahakama ngapi? Lakini ninachofahamu ambacho najua kwenye ngazi ya Wilaya ya Muleba, sisi hatuna Hakimu wa Wilaya. Tunaoletewa ni Mahakimu wanaosoma, akija miezi miwili, yuko pale kazini, miezi sita amekwenda masomoni. Wakifunga anakuja pale anakaa zile wiki tatu, nne za likizo. Sasa mimi nashindwa kuelewa kwenye Mahakama za Mwanzo hatuna Mahakimu. Kwenye ngazi ya Wilaya hatuna Hakimu, hivi hapa kuna haki kweli Muleba inayotendeka? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipowahi kuuliza swalii hili hapa Bungeni niliambiwa kwamba Hakimu huyu atapelekwa, lakini kwa taarifa niliyokuwa nayo jambo hili halijafanyika. Naomba Mheshimiwa Waziri, Serikali iangalie iweze kutupatia Mahakimu. Kwa sasa hivi anayesimamia Mahakama ya Muleba ya Kamachumu na Muhutwe anatoka Mahakama ya Mwanzo ya Muhutwe. Lakini ile Mahakama ya Rushwa, Rushwa ya Kihaya anatoka Nshamba zaidi ya kilomita 10 anatembea kwenda hiyo Mahakama. Mimi nadhani hata usafiri tunaowapangia wa pikipiki kwa kweli hautatosheleza kazi kubwa waliokuwa nayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tungeangalia namna nyingine ya kuboresha. Pikipiki tuliziomba wenyewe, lakini ni pikipiki iwepo kwa Hakimu mmoja na Mahakama moja. Kama ni Hakimu mmoja kwa Mahakama mbili, tatu, nne haiwezekani kwa pikipiki, lakini ukienda pia katika Wilaya ya Misenyi ambayo ilikuwa ni jimbo, ina jumla ya Mahakama sita ambazo ni Mahakama za Gera, Kayanga, Kanyigo, Buyango, Kyaka na Minziro. Tarafa mbili wana Hakimu mmoja, hapa kazi haiwezi kufanyika, haki haiwezi kutendeka. Nilikuwa naomba Serikali iangalie na sasa hivi Wilaya ya Misenyi inahitaji pia kupata Hakimu wa Mahakama ya Wilaya. Maana yake Mahakama ya Mwanzo iweje Mahakama ya Wilaya? Naomba masuala haya yaangaliwe ili kuweza kuona kwamba tunapata watu wenyewe kusimamia sheria tangu ngazi ya mwanzo kabisa. (*Makofi*)

La pili linaloendana na habari ya Mahakama za Mwanzo ni ubovu wa majengo. Tulipo-break hapa nikapata nafasi ya kuzungumza na Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo Muhutwe, akasema Mheshimiwa jua linapiga juu ya mafaili na hivi mvua zikinyesha mimi inabidi nahirishe kusikiliza kesi. Tafadhalii Mheshimiwa Waziri, naomba unapomaliza hapa, nilikuomba sana uiangalie Muhutwe, lakini katika mahesabu yako ulivyoweka hakuna hesabu yoyote ya Muhutwe. Muhutwe jua linapiga kwenye mafaili, mvua ikinyesha hawaendeshi session. (*Makofi*)

Mheshimiwa Dr. Mary Nagu alipokuwa kwenye nafasi hii alitembelea, alijionea. Huko mavi ya popo ndiyo perfume ya Hakimu na wenzake. Hapa hapakaliki, kazi

hazifanyiki. Naomba tafadhali sana Mahakama ya Muhutwe iingizwe kwenye ukarabati wa haraka ili kusudi kazi iweze kufanyika. Mengine ambayo yanahusu zaidi usalama wa raia, mambo ya ndani ya nchi, ni masuala yanayohusu *lock up* mbovu. Mahakama za kwetu zinaanza na *lock up*. *Lock up* mbovu, milango mibovu, watuhumiwa hawakai humo na watu wamekamatwa, ni suala ambalo linaleta matatizo. Ninaomba liangaliwe vizuri ili kuweza kuondoa matatizo. Watu wanakwenda kutafuta haki zao, pawe ni mahali pia panaweza pakaonekana kwamba panajali haki za binadamu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie kabisa, mwisho kabisa hili linalohusu Mahakama ya Kadhi. Mahakama ya Kadhi ni kitu kizuri sana, lakini uzuri wa Mahakama hii ya Kadhi, ni chombo ambacho kimetokea chini ya Taasisi ya Dini. Mimi sifahamu ni kwa nini Mahakama hii ilizuiwa miaka iliyopita, halafu wakati ule watu walikuwa ni wachache, lakini wakaona kwamba Mahakama ya Kadhi ni chombo ambacho zaidi kipo chini na ya Taasisi ya Dini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa nini leo kisiendelee kubaki chini ya Taasisi ya Dini? Kinataka kiingizwe katika utaratibu mzima wa Kiserikali, hii kitu hakiwezekani, hakiwezekani. Watanzania tuna dini mbalimbali, tuna imani mbalimbali, tuna makabila mbalimbali, tuna koo mbalimbali, tuna upenzi na ushabiki wa aina mbalimbali, haya mambo yamalizwe ndani ya dini zenyewe. Dini zote zinaruhusiwa kufunga ndoa, zinaruhusiwa kubatiza na wengine wanaruhusiwa kusoma, wanaita kusoma hakika kwa maana ya kwamba waweze kuthibitisha kuzaliwa kwa mtoto, dini zote zinaruhusiwa kufungisha ndoa, zinaruhusiwa kuzika. Sasa na mambo yanayohusu hawa watu katika jamii wayamalize, atakayeona haridhiki aende kwenye Mahakama iliyopo ya Serikali, hakuna mahali mimi nasema kuna matatizo kama kwenye dini ya Kikristo. Mwanamume yule wa Kikristo haruhusiwi kuongeza mke wa pili, lakini hawawaoi? Mwanamke wa Kikristo haruhusiwi kuolewa mpaka mume wake amekufa, lakini akiachwa haolewi? Mbona hawajadai kuanza Mahakama yao? (*Makofi*)

Mimi nilikuwa naomba haya wawe wanamalizana huko huko na yaendelee huko huko. Mtu adai haki zake mahali anapoona haki zitakuwa, lakini kwa utaratibu wa Kiserikali ambao sisi wote tutaungana pale, haya mengine naomba turudi kwenye dini zetu. Ukiamini dini yako naomba utii kweli kweli na mambo yake uyatii kweli kweli. Lakini usiitake Serikali sasa ikuwekee kiongozi wa Kitaifa mpaka imlipe na mshahara, ikiingia ndani ya Serikali hapa tutavurugana, hatutafika mbali. Hii ni nchi yenye amani na utulivu, tusimame tulivyo, tutaweza kufanikiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo, mimi napenda kusema kwamba narudia kuunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante, sasa namwita Mheshimiwa Fred Mpandazoe, atafuatiwa na Mheshimiwa Stephen Galinoma na Mheshimiwa Mohamed Missanga ajiandae. (*Makofi*)

MHE. FRED M. TUNGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nishukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hoja iliyoko mbele yetu. Kwanza kabisa naomba kusema kwamba naunga mkono hoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitakuwa na mambo mawili tu ya kuchangia, la kwanza kabisa ni suala hili ambalo tumekuwa nalo kwa muda mrefu. Tatizo ambalo tumekuwa nalo muda mrefu katika nchi yetu, lakini kwa sasa ndiyo inaonekana, tatizo la ufisadi usio na kifani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, uporwaji wa uchumi wetu unaofanywa na kikundi cha watu wachache unatakiwa kudhibitiwa Kikatiba kama tunataka nchi yetu isalimike. Katika kitabu cha uongozi wetu na hatima ya Tanzania, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere anasema hivi, naomba kunukuu, “Utajiri katika Tanzania unaweza kupatikana kutokana na rushwa kwa watumishi wa umma au kutokana na wafanyabiashara ambao wanawania nafasi za kisiasa ili wawe wadeni wa Rais aliyeko madarakani.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafsiri ya maneno haya ni kwamba Rais aliyeko madarakani, itabidi alipe fadhila kwa matajiri waliokifadhili chama chake au waliyemfadhlili ye ye mwenyewe wakati wa uchaguzi. Miaka 14 iliyopita Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere aliyona hayo na sasa ni dhahiri kuna dalili kwamba yatatokea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais na Waziri Mkuu, Mheshimiwa Joseph Sinde Warioba alisema hivi katika vyombo vya habari mwaka 2000 Aprili, naomba kunukuu; “Kuna mwenendo usiopendeza wa kuongezeka kwa kasi kwa pengo kati ya matajiri na maskini, siasa inatekwa na matajiri, ufisadi na rushwa ni vitu muhimu kwenye uchaguzi. Ufisadi unaigawa nchi vipande.” (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, aliyosema Mheshimiwa Jaji Joseph Warioba miaka minane iliyopita sasa ni dhahiri, wapo wananchi matajiri sana na wapo wananchi maskini sana kwenye nchi hii yenye utajiri mkubwa. Pia ni kweli kwamba si kila tajiri ni fisadi. Wapo wananchi waliopata utajiri kwa haki, japokuwa pia ni rahisi ngamia kupita kwenye tundu la sindano kuliko tajiri kuurithi ufalme wa Mungu. Lakini pia kwamba si kila tajiri ana uwezo wa kuongoza, kuwa tajiri pekee siyo sifa ya kukufanya uwe kiongozi wa wananchi kwa lengo la kuwawakilisha vizuri na kuwatumikia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuiuliza Serikali, je, haupo umuhimu sasa wa kuiangalia Katiba yetu ili tuone kama inajitosheleza kukabiliana na changamoto hizi. Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete alipokuwa analizindua Bunge, tarehe 30 Desemba, alisema hivi naomba kunukuu; “Mheshimiwa Spika yameanza mawazo kuwa uongozi unaweza kununuliwa kwa fedha. Tusipokuwa waangalifu nchi yetu inaweza kuwekwa rehani kwa watu wenye fedha za kununua uongozi au wanaoweza kupata fedha za kufanya hivyo. Maana unaweza ukafadhiliwa na mtu ili anunue uongozi. Ni vyema sasa tulizungumze hili na tulishughulikie suala hili.” Mwisho wa kunukuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi kuwekwa rehani kwa matajiri ni jambo la hatari sana. Maana yake Serikali itaongozwa na matajiri. Hivyo haitawajibika kwa wananchi bali italinda maslahi ya matajiri. Maana yake matajiri watanunua kila haki ya mwananchi,

ina maana demokrasia itakoma, udikteta utaanza na wananchi watapata shida kubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna mwenendo ambao ulionekana kwenye uchaguzi wa mwaka 2005. Fedha nyingi sana zilitumika kwa vyama vyaa siasa na wagombea wengine. Ipo haja sasa ya kuweka utaratibu wa kuweka wazi kiasi cha fedha zitakazotumika kwenye uchaguzi kwa vyama vyaa siasa na wagombea wenye. Tusipofanya hivyo ni rahisi sana nchi yetu, majimbo yetu, kata zetu, tutaziweka rehani kwa matajiri. Watapatikana viongozi wasio na nia ya kuwatumikia wananchi na wasio na uwezo wa kuongoza. Kwa sababu si kila tajiri ana uwezo wa kuongoza na nchi itaporomoka kiuchumi na kimaadili. Je, Wizara imechukua hatua gani mpaka sasa kuhusiana na mtazamo wa Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete tangu alipozindua Bunge miaka mitatu iliyopita?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 8 kifungu 1(a) na kifungu cha 1(c) cha Katiba yetu inasema, wananchi ndiyo msingi wa mamlaka yote na Serikali itapata madaraka na mamlaka kutoka kwa wananchi na Serikali itawajibika kwa wananchi. Serikali inayopata madaraka kutoka kwa wananchi na Serikali inayowajibika kwa wananchi ni Serikali ya kidemokrasia. Maana yake Serikali inachaguliwa na watu, ni Serikali inayoongozwa na watu, ni Serikali inayowajibika kwa watu, lakini kutokana na mwenendo uliopo na unaoendelea sasa, hakika kama hatutachukua hatua madhubuti, Serikali haitachaguliwa na watu, itachaguliwa na matajiri. Serikali haitawajibika kwa wananchi, itawajibika kwa matajiri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wataalam wa sayansi wanasema, kutokana na uporaji wa uchumi unaofanywa na kikundi cha watu wachache, kwa njia mbalimbali za ufisadi, ipo hatari ya kuibuka matabaka mbalimbali katika jamii, tabaka la kwanza ni la matajiri hawa wachache wanaomiliki uchumi katika nchi yetu. Tabaka hili kwa Kigiriki linaitwa oligaki. Tabaka hili la oligaki litakuwa na watu wake wateule wanaojiona bora katika jamii. Watu ambao wameingizwa na oligaki kwenye sehemu muhimu za nchi kama mabenki na kwenye makampuni yaliyowekeza hapa nchini. Kikundi hiki cha watu wachache wanajiona ni bora katika jamii wanaitwa *aristocracy*. (*Makofi*)

Vile vile kuna tabaka lingine, kutokana na *aristocracy* kuna tabaka lingine litaibuka la watu ambao wana tamaa ya madaraka, wana tamaa ya makuu. Kikundi hiki kinaitwa *timocracy*, *timocracy* ni kikundi cha watu ambao hawana msimamo wowote kwa sababu ya tama, wapo tayari kuunga mkono hoja zote za oligaki na *aristocracy*. Kwa hiyo, ni watu ambao ni hatari sana, lakini kundi la mwisho ni la watu maskini. Wananchi maskini ambao wanaishi kwa matumaini ya kupata maisha bora na inawezekana wasiyapate. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanasyansi wa jamii wanasema matabaka haya yameanza kutokea, ina maana Serikali haitachaguliwa na watu na Serikali haitaongozwa na watu na Serikali haitawajika kwa watu. Hivyo demokrasia itakoma na udikiteta utashamiri. Nakubaliana na mtaalam wa mahesabu na mwanafalsafa anaitwa Albert Ensiten aliyesema kwamba ulimwenguni pamekuwa mahali pa hatari sana kuishi. Hali hii

haitokani na uovu unaotendeka lakini unatokana na watu wanaoangalia uovu ukitendeka na hawachukui hatua. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hivyo nakubaliana kwamba au unaweza kusema kwamba kulingana na Ensiten, yawezekana Tanzania pakawa mahali pa hatari sana kuishi, lakini haitatokana na ujisadi unaofanyika. Lakini utatokana na Serikali kuchelewa kuchukua hatua au kutochukua hatua kabisa dhidi ya ujisadi unaotokea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuishauri Serikali ichukue hatua mapema na madhubuti dhidi ya ujisadi wote uliotokea nchini, ujisadi wa *EPA*, ujisadi wa MEREMETA unaotajwa na ujisadi mbalimbali ambao tumeusikia. Hatua zisipochukuliwa na za madhubuti kama alivyosema Ensten, Tanzania patakuwa mahali pa hatari sana kuishi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mwisho lakini si kwa muhimu, tena la muhimu sana. Wilaya yetu ya Kishapu ina upungufu mkubwa sana wa Mahakimu kama alivyoeleza dada yangu Mheshimiwa Ruth Msafiri. Vile vile Kishapu kuna matatizo makubwa ya upungufu wa Mahakimu na majengo mengi ya Mahakama ni mabovu, yamechakaa.

Naiomba Wizara iangalie uwezakano wa kukarabati majengo hayo ya Mahakama na kutuwezesha kupata Mahakimu wa kutosha. Vile vile kuna Mahakimu wamekaa muda mrefu sana katika sehemu moja. Utendaji wao wa kazi umekuwa hafifu, naiomba Serikali iliangalie tatizo hilo, uhamisho ni jambo lililo muhimu. Umuhimu wake ni kwamba unapelekwa mahali panya hasa kwa Mahakimu ambako watu hawakufahamu na hawataweza kukujaribu kukufanyia chochote cha kukupa rushwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba Mheshimiwa Waziri anipe maelezo kwa nini? Baadhi ya Mahakimu wa Wilaya yetu ya Kishapu, wanaendelea kupokea na kusikiliza kesi zinazohusu migogoro ya mipaka au migogoro ya ardhi wakati Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji yapo. Mabaraza ya Ardhi ya Kata yapo na Baraza la Wilaya lipo, sasa Mahakimu wanaendelea kupokea na wanaendelea kusikiliza badala ya kuwaelekeza wananchi waende kwenye Mabaraza hayo. Sasa kuna nini, naomba sana Waziri anipe maelezo ya kutosha kuhusu hali hii ambayo inaleta usumbufu mkubwa katika Wilaya yetu ya Kishapu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo kama nilivyosema naunga mkono hoja, lakini naomba sana maoni niliyotoa nipate maelezo ya kutosha kesho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Fred Mpandazoe, sasa namwita Mheshimiwa Stephen Galinoma na atafuatiwa na Mheshimiwa Athuman Janguo na Mheshimiwa Maria Hewa, ajiandae.

MHE. STEPHEN J. GALINOMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. Pili, napenda nimpongeze Waziri wa Sheria na Katiba kwa mambo mawili.

Kwanza kwa hotuba yake nzuri, yenyе kina na yenyе matumaini, lakini pili, napenda nimpongeze maalum na mahususi kabisa kwa kazi ambayo Wizara yake inafanya Jimboni kwangu kwa kujenga Mahakama ya Makao Makuu ya Jimboni kwangu Kalenga. Kazi inayofanyika inakwenda haraka sana na sasa hivi wamefikia hatua ya kupaua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa nitoe mchango mfupi tu, sitakuwa na maneno mengi, lakini la kwanza ni kuhusu upungufu wa Mahakimu. Asubuhi akijibu swalı, Mheshimiwa Waziri ameeleza vizuri sana, mkakati wa kuziba mapengo mengi yaliyopo na mimi hapo sina la kusema, isipokuwa ningemuomba atupe msimamo wa uhakika juu ya wajibu wa kusafirisha na kulisha mahabusu katika Mahakama zetu. Sasa hivi jinsi ilivyo ni kwamba jukumu hili anachukua au anaambiwa atekelze yule anayemshitaki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, yule anayepelea malalamiko ndiye anaambiwa msafirishé mtuhumiwa, ndiye anayeambiwa amlishe, hii si haki na ningependa kumsikia Mheshimiwa Waziri anaweka msimamo gani. Najua siku za nyuma tumeambiwa kwamba ni jukumu la polisi au kitu kama hicho, lakini haitekelezwi. Kwa hiyo, ni vizuri tukawa na msimamo ambao unatekelezeka. Kwa sababu haki inachelewa kutekelezwa na vile vile wakati mwingine haki haitolewi kabisa kwa sababu wakati mwingine mtu anakwenda hamkuti hakimu, anakata tamaa na pengine kesi yenyewe ni ndogo labda ya kuiba kuku tu. Kwa hiyo, inatusumbua sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, naomba hao Mahakimu wachache waliopo naomba kama walivyosema wenzangu wawezeshwe, wapate vyombo vy ya usafiri kwa sababu kama walivyosema wengine mahakimu hawa wana kazi kubwa ya kutembelea na kufanya kazi katika mahakama nne, tano kwa muda mfupi. Sasa bila kuwa na usafiri wa uhakika jambo hili si rahisi kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nigusie suala la Mahakama ya Ardhi, siyo ya Kadhi, Mahakama ya Ardhi. Mahakama hizi zimeanzishwa sehemu nyingi katika mtindo wa Kanda kiasi kwamba unakuta hakimu mmoja anahudumia Wilaya sita, saba wakati mmoja. Wakati mwingine anatakiwa kwenda mkoaa mwingine. Kwa hiyo, kunakuwa na ucheleweshaji mkubwa sana wa kesi hizi. Naomba katika suala hili mfumo huo ufikiriwe upya, sioni kwa nini kwa mfano mahakimu wote wa ngazi ile wasipewe *jurisdiction* kusikiliza mashauri hayo badala ya kuweka mahakama tofauti tofauti na kusababisha ucheleweshaji. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ningependa niende katika suala ambalo ni nyeti lakini tunapaswa kuzungumza na sitakwenda kwa undani, nitazungumza kwa ufupi sana. Mwaka 1983, Bunge hili hili lilitunga sheria ya kudhibiti uhujumu wa uchumi (*Act No.*

09 of 1983), hii ilitungwa ili kukabili vitendo vya kuhujumu uchumi vilivyokuwa vimejitokeza wakati huo yaani *economic sabotage*. Wale tuliokuwepo wakati ule tutakumbuka kwamba kweli kulikuwa na vitendo fulani fulani vya hujuma hapa na pale lakini sio kwa kiwango kikubwa hiki tunachoshuhudia leo. Hujuma za sasa ni nyingi, kubwa, zinafilisi Taifa na sasa hivi zimebadilika zinaitwa ujisadi, lakini bado ni zile zile kuhujumu Taifa.

Sasa mimi ningependa, japo sipendi kuingia kwa undani, niulize Serikali kama sheria hii haijafutwa, inakuwaje tuhuma zote ambazo zimekuwa zikisikika kila wakati kushoto, kulia na katikati, hazichukuliwi hatua? Ni nini kinachotuzuia? Kwa nini hatuitumii sheria hiyo ili kusafisha jina na sifa nzuri ya Taifa letu? Madai kwamba fisadi au mhujumu hawezi kushughulikiwa mpaka kuwe na ushahidi wa kuthibitisha *beyond reasonable doubt* mimi naona ni kisingizio tu. Nakumbuka wakati sheria hii inatengenezwa mimi nilikuwa ni Naibu Katibu Mkuu wa Waziri Mkuu, wakati huo Hayati Edward Sokoine, tulisema na nadhani ilikuweko katika sheria, iliwekwa katika sheria kwamba si lazima kuwe na *proof* hiyo ya *beyond reasonable doubt*. Tulisema mazingira ya rushwa, mazingira sasa hivi ya ujisadi yangetosha kabisa kumtia mtu hatiani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipengele hicho nadhani bado kipo na kama ninavyosema sioni ni kwa nini sheria nzima hiyo imewekwa kando. Hujuma, ujisadi, umeenea kila kona, lakini hatutaki kuitumia hiyo sheria, tunaogopa vivuli vyetu wenywewe hadi Taifa litakapoangamia na mimi nasema historia itatuhukumu. Ni vizuri tujitazame upya tuone kwamba vitendo hivi vinaharibu sifa na jina la nchi yetu, tutambue kwamba nchi nyingi zimeangushwa huko nyuma kwa sababu ya mambo haya ya rushwa na ujisadi. Hivi kweli tunapenda tufike hatua hiyo?

Mimi nafikiri kila anayependa Taifa hili, anayependa nchi yake, atakataa na kwa sababu hiyo mimi nashauri kama alivyosema mjumbe mmoja aliyeppita sasa hivi kwamba ni vizuri tukajiimarisha tukawa *bold*, tukachukua hatua za makusudi kabisa kusafisha suala hili zima. Tukumbuke kwamba hata sisi Wabunge, tunawekwa katika hali ngumu kwa sababu hatuwezi kutetea baadhi ya haya mambo, kama hatujui ukweli hatujui undani. (*Makofi*)

Kwa hiyo, ni vizuri kukawa na maelezo, kukawa na kama muongozo hivi kwamba haya ndio yaliyotokea na kwa hiyo, sisi tutakuwa mstari wa mbele kusaidia kusafisha jina la Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema awali kwamba mimi sio mtu wa maneno mengi na sipendi kupoteza muda mwangi sana. Napenda niishie hapo, naunga mkono hoja ya Waziri wa Katiba na Sheria kwa nguvu zangu zote na hasa nikikumbuka kwamba fedha walijotengewa ni kidogo sana ukilinganisha na majukumu walijokabidhiwa. Kwa hiyo, naunga mkono moja kwa moja. (*Makofi*)

MHE. ATHUMANI S. JANGUO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii adhimu ya kuweza kuchangia kwenye hoja hii muhimu sana kwa Watanzania. (*Makofi*)

Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuniwezesha kusimama hapa ili niweze kutoa mchango wangu. Napenda vile vile kuwashukuru wapiga kura wangu wa Kisarawe kwa imani wanayonipa na kuniunga mkono na kunipa ushauri kila wakati ninapotimiza majukumu haya na ninawaahidi kwamba nitaendelea kupigania maslahi yao kwa nguvu zangu zote na uwezo wangu wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo napenda kwa kweli nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu na wasaidizi wao wote kwa mambo mawili, moja kwa hotuba nzuri sana ambayo imegusa maeneo mbalimbali na pili, kwa kazi nzuri ambayo Wizara inaifanya katika mazingira magumu sana, hususan mahakimu kule katika ngazi za Wilaya na Mahakama za Mwanzo ambapo kama walivyosema wenzangu waliotangulia vitendea kazi ni finyu, hakuna usafiri, majengo ya mahakama ni mabovu na ukiangalia hata marupurupu wanayoyapata kwa kweli hayalingani na kazi ngumu wanayoifanya. Kwa ufupi tu, kielelezo cha matatizo haya ni katika wilaya yangu ambacho kinatosha kuonekana kwamba wilaya nyingine zote zina hali kama hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Kisarawe, mahakama ya wilaya haina hata ofisi na mahakama moja ya mwanzo haina ofisi. Wao pamoja na polisi wanahifadhiwa katika jengo la Mkuu wa Wilaya, namshauri Mheshimiwa Waziri, aangalie uwezekano wa kuhakikisha kwamba hili linatatuliwa upesi. Katika mahakama zilizobaki mahakimu hawapo, pale Kisarawe kwenyewe Hakimu Kiongozi hayupo, aliyekuwapo amestaafu na hakuna tena mwingine isipokuwa kuna hakimu msaidizi mmoja tu mbali na kwamba wanahitajika kutembelea mahakama katika Tarafa nne ambako mahala pengine hakuna hata makarani wa mahakama. Kwa hiyo, basi nifupishe katika hili, nashukuru kwamba kwenye hotuba hii Mheshimiwa Waziri, ametoa ahadi ya kuweza kutatua matatizo hayo na ningemuomba aangalie matatizo ya Kisarawe kwanza kwa kuwa nayaona ni magumu zaidi kuliko hata mahala pengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya pili, ningependa kuzungumzia hoja ya Mahakama ya Kadhi. Kwanza nimpe pole Mheshimiwa Waziri na Serikali. Unapokuwa na jamii ambayo watu waliokuwa wengi, lukuki, wanataka jambo hili halafu wanakuwepo wachache wanaoinga maamuzi yake ni magumu, tena wanaokataa wala hayawahuusu. Kwa hiyo basi, wana kazi ngumu sana lakini kwa hotuba ya leo nimepata matumaini kwamba Serikali angalau baada ya miaka 50 tangu mwaka 1958 suala hili lilipoletwa Bungeni, mpaka sasa hivi bado halijaamuliwa sasa inakishughulikia. Unapowaweka watu katika *suspense* kwa muda mrefu namna hiyo unaweza kukosa hata ule uvumilivu wao, ninaamini kabisa kwamba kwa kuwa Serikali imesema suala hili sasa limemalizwa katika ngazi ya Tume ya Kurekebisha Sheria, ninaamini Serikali itatoa uamuzi wa haraka ili kuondoa kukereketwa kwa watu ambao wanakuwa wanaona kwamba hawatendewi vizuri. Muda hauniruhusu kuelezea *argument* za kwa nini hasa Waislamu wanataka sana kuwe na Mahakama ya Kadhi. Lakini kwa ufupi tu, maamuzi ambayo wanatakiwa wayafanye ni katika maeneo ambayo ni *matrimonial*. Ndoa, utunzaji

wa watoto, talaka na migongano misikitini. Haya yanataka yaamuliwe na watu ambao wanajua *Islamic Law*, bila ya hivyo maamuzi yake yatakwenda kinyume na maamuzi ambayo *Quran* inaelekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa unaposema kwamba hutaki hilo maana yake unawafanya hawa wafuate maamuzi ambayo yanakwenda kinyume na maelekezo ya Mwenyezi Mungu kwa imani yao na kwa kufanya hivyo ni kwamba wanavunja ibada zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, historia imeelezwa ndani mle, tatizo limetokea toka mwaka 1963 na mwaka 1971 wakati imepitishwa Sheria ya Ndoa ambayo imekubali tu sehemu chache za *Islamic Law* na ikaacha yale mengine. Waislamu kutoka wakati huo wameanza kunung'unika mpaka hii leo. Kwa hiyo basi kilichofanywa na Wabunge waliopita akiwemo Mheshimiwa Augustino Mrema, Mheshimiwa Baruti na Mheshimiwa Thomas Ngawaiya kati ya mwaka 1995 na 2000, na kuleta hoja ambayo ilikuwa inafuatilia manung'uniko ya watu. Kwa hiyo basi, mimi ni mategemeo yangu Mheshimiwa Waziri na Serikali, watazingatia yafuatayo; kwanza, Waislamu bado wanانung'unika kwa kulazimishwa kufuata maamuzi ya watu ambao hawajui maelekezo ya Mwenyezi Mungu kwa utaratibu wa dini yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili limekaa muda mrefu sana kwa hiyo, lisiposhughulikiwa ni kwamba inawezekana tukafika mahala tukakosa uvumilivu wao. (*Makofi*)

Pia Serikali imetumia fedha nyingi sana kwa suala hili na hapa ningependa nimpongeze Spika Mstaafu, Mheshimiwa Pius Msekwa, kwa kufuata maelekezo ya ya Chama cha Mapinduzi katika Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2005, aliunda Kamati tatu mfululizo kuanzia mwaka 1998 mpaka 2000 ambazo zimetumia fedha za Serikali kwa kukutana na waumini wa Kiislamu, waumini wa dini nyingine, kufanya misafara kwenda Zanzibar, Kenya, Uganda, Mozambique na *South Africa* ili kupata maoni na kuona ni namna gani Mahakama hizi zinafanya kazi katika nchi hizo hususan Kenya na Zanzibar, ambako tayari kuna Machifu Kadhi lakini hakuna migogoro. Sasa leo mtu akija akiniambia kwamba tutavurugana, kwa nini hatukuvurugana kabla ya mwaka 1963? Kwa nini hawavurugani Kenya? Kwa nini hawavurugani Zanzibar? Mimi nafikiri wanaosema hivi ni watu wasiojua undani wa hili ambalo Waislamu wanataka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, pana haja ya kuwaelimisha na pengine isingekuwa vibaya tukawa na semina halafu wakaelimishwa wenzangu kusudi wawewe kujua ni nini hawa watu wanadai. Katika Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2005 Ibara ya 99, kwa ruhusa yako naomba niinukuu inasema; "Katika kuzidi kuimarisha misingi ya demokrasia na utawala bora katika kipindi cha mwaka 2005 hadi 2010, CCM itahakikisha utekelezaji wa mambo yafuatayo:-" (a), (b), (c), (d), lakini ukifika (g) inasema; "Kuweka na kusimamia utaratibu mzuri zaidi wa kupokea kero za wananchi na kuhakikisha kuwa zinapatiwa ufumbuzi wa haraka," hii ni kero.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Ibara ya 108 inazungumzia sekta ya sheria inasema; “CCM itazitaka Serikali ziendelee na hatua zilizoanza kuchukuliwa ili kuiboresha sekta ya sheria kusudi nayo itoe huduma bora zaidi kwa jamii. Yatakayozingatiwa katika kipindi hiki ni pamoja na yafuatayo:-” (a) naacha lakini (b), “Kulipatia ufumbuzi suala la kuanzishwa kwa Mahakama ya Kadhi Tanzania Bara,” kidumu Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Sasa kwa kutokutimiza hili si tu kwamba tumedharau pesa zilizotumika, si tu kwamba kuna watu wanalamika lakini vile vile bado hatujatekeleza agizo la Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa mujibu wa Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2005. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema kwamba hii ni ibada na labda hapa nimnukuu Jaji Mkuu Mheshimiwa Agustino Ramadhani, akimnukuu Profesa Noel J. Coulson wa *Chicago University* katika mada yake ya mwaka 1969, anasema katika *The problems and solutions of administration of justice in plural systems of the common law; “Islamic Law is the divinely ordained system of God’s commands which determines ultimate values and purposes of human life of the Muslims since Islam is...”* maneno yanayofuata sasa, nataka tu kuya-underline, *“Islam is the total submission and surrender to Allah.”* Sasa unapobagua sheria zake zingine hujakuwa na *total surrender*. Tafsiri yake ni kwamba Uislamu ni kukubali na kujisalimisha moja kwa moja kwa Mwenyezi Mungu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuikumbusha Serikali kuwa suala hili limeigharimu Serikali fedha nydingi, kama nilivyosema na kwa hiyo, mimi nina amini kabisa ni kwamba ni muhimu kulifatilia. Lakini mwisho, mwaka jana, aliyekuwa Waziri wa Sheria, Mheshimiwa Dr. Mary Nagu na Naibu wake ambaye sasa hivi ndiye Waziri, Mheshimiwa Mathias Chikawe, walikuwa na kikao na baadhi ya Waislamu kutaka kupata maoni yao juu ya malalamiko ya Waislamu ni nini na tufanye nini kusudi kuweza kutatua tatizo hili. Pakaahidiwa kwamba suala hili limepelekwa kwenye Tume ya Kuchunguza Sheria na tunaamini kwamba matokeo yatapatikana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafurahi kusikia kwamba ingawa baada ya mwaka mmoja, sasa hivi Serikali imeshapata ile taarifa basi himizeni mtoe uamuzi, uwe mzuri au mbaya Waislamu ama wameze ama wateme. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho katika hotuba hii tunaambiwa kuwa Serikali inachukua tahadhari ili tusiligawe Taifa, sawa. Lakini kwa kuacha *section fulani* ya *society* inanung’unika, unaligawa Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nimalizie kwa kumnuuu tena Jaji Mkuu, anasema; *“Again there is a feeling that Nationalism is forged better by acknowledging ethnic or tribal origins rather than suppressing them. The same can be said about religions, the more conscious we are of varying faiths and willing to respect or even incur some expenses to enable observances the more harmonious we are going to be.”* Maneno haya Waingereza wanasema *they speak loud and clear. Expense* nimesikia hapa ikitsemwa kwamba kwa nini tuingie gharama. Demokrasia ina gharama. Ili uweze kutimiza demokrasia ni lazima ukubali kwamba utaingia gharama. Kwa hiyo basi,

nimalizie tu kwa kusema kwa mategemeo kwamba Serikali sasa itachukua hatua, mimi naiunga mkono hoja hii na ninategemea kwamba watafanya lile ambalo linastahili kufanyika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru ahsante sana na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. MARIA I. HEWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii jioni ya leo ili na mimi niweze kushiriki katika kutoa mawazo yangu kuhusu hotuba ya Waziri wa Katiba na Sheria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda cha kwanza kabisa ambacho ninataka nianze kuzungumzia ni suala zima la jinsi gani hotuba hii au Wizara hii imeweza kufikiria juu ya upunguzaji wa kesi mahakamani. Labda nianze tu moja kwa moja kwa kumpongeza Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa suala zima la uteuzi wa Waheshimiwa Majaji akiwa amezingatia kuweka akinamama wengi kuliko wanaume. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende tu kusema hivyo kwa sababu inawezekana katika ngazi hii walio wengi wangeweza kufikiria kuweka wanaume zaidi kuliko wanawake kwa umuhimu wa kusikia neno Jaji. Lakini kumbe ni wakati muafaka sasa, tunapozungumzia masuala ya jinsia Jaji, hata kama kuna ngazi nyingine zaidi ya Jaji, wanawake tunatosha. Sasa katika hili mimi ninaamini suala zima la kesi mahakamani zitapungua kwa sababu wanawake ni wajibikaji wakubwa, tumeumbwa hivyo kwamba tunajua kujituma, tunajua kutii na mara nyingi tunakuwa tupo wakati tunapohitajika na katika hili matatizo mengi hata sheria hizi ambazo tunapiga kelele humu Bungeni zibadilishwe au zirekebishwe au zina upungufu fulani zinamgusa mwanamke na nadhani ni wakati muafaka sasa wanawake hawa wakatumbo wanawake wenzao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili, hasa hasa Kamati hii ya Katiba, Sheria na Utawala wameongelea pia suala la usafiri wakiwagusa mahakimu tu. Mimi naomba pamoa na mahakimu kupewa usafiri, mahakimu humo humo wamo wanawake pia na kwenye Majaji hawa ndio wengi 11 na wenyewe waendelee kufikiriwa kupewa usafiri wa uhakika kwa sababu mwanamke ni mwanamke kama nilivyosema mambo ni mengi. Ni pamoa na kuhudumia familia ikibidi akihitaji kuhudumia familia awe na nyenzo hizi zisije zikampa shida. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda sasa niende kwa suala la pili la haki za binadamu na utawala bora. Wakati Kamati inasoma taarifa yake walizungumzia suala la mauaji ya albino na ikatajwa Mwanza. Nakubali kweli kwamba haya mambo yametendeka kwa sababu wanayatenda na watu wanayaona na yana ushahidi ndani. Lakini niseme hivi kinachosibu ni ukosefu wa elimu ya kujua kwamba albino naye ni binadamu kama binadamu tulivyo sisi. Ukimpa shughuli zozote zile anaziweza lakini elimu inayohitajika ni ile ya kumthamini tu, ya kujua kwamba naye ni binadamu kama kawaida halafu pili wajue tu kwamba huko waliko wanakowazia suala zima la kumuandama albino ni suala la ushirikina tu wala sio suala lingine. (*Makofi*)

Sasa elimu ambayo naitaka mimi ni ile ambayo inatakiwa iende mpaka huko wanakofanya hayo madhambi. Elimu tunabaki kuelimishana sisi tu, sisi hapa tukiulizana hapa tumepitisha semina ngapi za kumuelewa albino ni nani, ni nyingi mpaka hata wakati mwingine unawenza ukasema leo siendi kuhudhuria. Lakini huyu anayeyafanya haya inawezekana hajui kabisa afanye nini, ili mradi ye ye kaambiwa tu kwamba ukimpata albino basi ndio unatajirika, ukimfuatilia hata utajiri hana si afadhalii apate elimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niombe katika hili, Mheshimiwa mmoja amesema suala la makongamano, warsha, semina, sijui nini hebu tuyapunguzwe basi na wenyewe nao wayapate haya makongamano wapate semina, wapate hotuba mbalimbali ili kusudi tuweze kudhibiti uhalifu huu na kesi mahakamani zitapungua. (*Makofi*)

Naomba hili tuliwekee maanani kabisa kama ni kufikiria juu ya Bajeti, Bajeti hizi kama zinaongezwa basi ziongezwe kwa maana ya kuwajali na hawa watu wa chini waweze kuelimika, waweze kuacha kutenda maovu ili kesi mahakamani zipungue. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu ambalo nataka niliongelee ni suala la utafiti na uandishi wa sheria. Niliposoma hotuba hii kwa kweli nilijisikia vizuri kwa sababu tunapoongelea kubadilisha suala la maandishi yanayogusa sheria kutoka Kiingereza kwenda Kiswahili tunajua tunamuongelea mtu ambaye ni mtu wa kati na mimi nazidi kuzungumzia hasa hasa hizi sheria zinazowagusa akinamama, akinamama wengi huko nyuma walikuwa wala hawafikiriwi kwa kupewa kipaumbele kupelekwa shulenii. Walikuwa wakipelekwa hata shulenii wanakuwa na muda, *I mean* na kiwango chao cha kupata elimu. Wanaambiwa kuishia darasa la nane, wanaambiwa mwisho wao darasa la 10, wanaambiwa mwisho wao darasa la 12, mimi hata mama yangu mzazi wakati anasoma aliambiwa mwisho darasa la sita, kumbe alikuwa na nia ya kuendelea. Sasa katika *group* hilo ukianzia mama yangu na wengine na wengine mpaka hata wengine tu wa kutukaribia umri wetu na wenyewe hawakwenda shule, lakini ndio wenye matatizo ya kujua sheria. (*Makofi*)

Sasa katika kuibadilisha kutoka Kiingereza kuipeleka katika Kiswahili na huyu mama naye atashiriki ataaelewa, ataisoma hata hukumu yake inasema nini. Kwa hiyo, mimi nashukuru sana sana tu, ili wengi tujue kufuatilia na kuelewa sheria inasema nini na hukumu mahakamani zinapotolewa zinazungumza nini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi katika hili kwa kweli ninaunga mkono kabisa ili kusudi mbele ya safari ukiniuliza au nikimueleza mwanamama kwamba wewe chukua hii hukumu yako, hebu kaisome vizuri, katika *level* aliyoelimishwa Tanzania hii anawenza akaielewa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho napenda kuongelea adhabu zinazotolewa na Mahakimu Mahakamani. Mahakimu sijui huwa wana-refer vipi, mimi mpaka leo huwa nashindwa kuelewa. Anatoa hukumu kwa kuweka kumbukumbu ya Sheria ya Amerika, Urusi na kadhalika kwamba ukisoma sheria ya mahali fulani inasema hivi basi na

Tanzania anahukumu mtu kulingana na hiyo sheria. Mimi wala hata sielewi kwa kweli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika hili hebu tufike basi mahali hivi sisi hatuwezi tukajitegemea na maamuzi? Tuendelee tu ku-*refer* huko nyuma mpaka lini? Mimi naomba maana yake wakati mwingine hukumu zinatoka mtu kaiba kuku anahukumiwa miaka sita, sheria ya Amerika ilisema hivi hivi kwamba aliyeiba kuku anahukumiwa miaka sita. Anakuja mwingine ameiba ng'ombe 20 anaambiwa mwaka mmoja, sheria ya Urusi ilisema alipofanya hivi akafanya hivi na kadhalika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwamba hebu tufike mahali na sisi wenyewe tujitegemee basi katika sheria. Kuku miaka sita, ng'ombe mwaka moja tuki-*refer*, hapana! Tujue kwamba tunapotoa adhabu za namna ile mtu kaiba kuku hebu mfikirie na gharama za kumlaza kule, kumlipia vitu vingine badala yake angekuja akajenga Taifa, unamuhukumu miaka sita kaiba kuku, hebu tujaribu kuona na hasara ambazo tunazipata katika nchi yetu katika kuwarundika mahabusu au kuwapa hukumu ambazo ni kali wakati mwingine zinawaathiri hata akinamama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi nilikuwa nasoma gazeti moja, wake za wafungwa wanataka nao kuandamana, sasa na hivi maandamano yamenoga nchi hii, nao wanataka kuandamana. Lakini unaweza ukawauliza hivi mama unataka kuandamana mume wako amefungwa kwa kitu gani? Atakujibu kwamba ameiba kuku, ukimuliza amefungwa miaka mingapi anakuambia sita, anaona kwa kweli tunakuwa na maamuzi yasiyokuwa na msimamo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu katika hili hebu tuone kwa nini mtu huyu mwenye kufanya makosa ambayo ni madogo madogo bila ku-*refer* hukumu za wenzetu tuwatoe mapema ili waweze kuja kufanya shughuli za maendeleo nchini mwetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo yangu hayo naunga mkono hoja na ninashukuru sana. Ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mama Hewa na sasa namuita Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, atafuatiwa na Mheshimiwa Hassan Kigwalilo na Mheshimiwa Bernadeta Mushashu ajiandae. (*Makofi*)

MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia juu ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria. Kabla ya yote kwanza nimpongeze kwa hotuba yake na mimi niseme naunga mkono hoja hii mia kwa mia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwa leo nitajikita katika suala zima la Mahakama ya Kadhi. Kwa misingi ya kisheria kuna aina kuu za kesi, kesi za jinai na kesi za madai. Lakini kesi za jinai ni kesi za Serikali, kama kuna mtu ameua hapo hakuna suala la ndugu kuingilia isipokuwa ni Serikali itaingilia kati na kusimamia kesi hiyo mpaka imalizike. Lakini kuna kesi ya madai. Kesi ya madai Serikali kazi kubwa inayofanya ni kuleta

suluhisho ili upatikane muafaka na hiyo kesi waridhike pande zote mbili na kama kuna mtu anatakiwa alipe gharama au kurudisha gharama basi Mahakama kazi yake kubwa ni kufanya kazi hiyo ya usuluhishi ili haki ipatikane. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kesi za madai zipo mahususi zinazoitwa *Personal Law* yaani Sheria Binafsi, jinsi mtu atakavyoendesha familia yake katika mambo yote kama ndoa, mazishi, mirathi na kadhalika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini labda ninukuu Katiba Ibara ya 19 ambayo inatuambia kwamba; “Kila mtu anastahili kuwa na uhuru wa mawazo, imani na uchaguzi katika mambo ya dini pamoja na uhuru wa mtu kubadilisha dini au imani yake.” Mwisho wa kunukuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mahakama ya Kadhi ni kuhusu *Personal Law*, Mahakama ya Kadhi ni Mahakama ya Kiislam inayoendesha na Hakimu Muislam, inayowahukumu Waislamu tu katika matatizo yanayowahusu Waislamu tu katika ndoa, talaka, mirathi, wakfu, wasia, migogoro ya ibada misikitini, malezi ya watoto na kadhalika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nikienda mbali zaidi masomo ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, katika *Islamic Law* angalia kitabu cha *University of Dar es Salaam Prospectus* cha mwaka 1997/1998 ukurasa wa 152 mpaka 156. Katika maneno yote yaliyotajwa *Islamic Law* yanaonyesha kwamba kitendo cha kukubaliwa hizo *Islamic Law* na zikafundishwa katika Chuo Kikuu chetu ndiyo ishara wazi kumkubali msimamizi wa sheria hizo ambaye ni Kadhi. Kama anavyotajwa katika Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 ukurasa wa 7 nanukuu; “Kwa mujibu wa Sheria ya Ndoa, Padri, Mchungaji, Kadhi, Shehe ni wasajili wa ndoa kwa hiyo, wao wanao uwezo wa kufungisha ndoa za waumini wao.” Mwisho wa kunukuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa shehe sasa hivi anafungisha ndoa, lakini Kadhi yumo katika sheria lakini yeze mwenyewe hatakiwi. Sasa hakuna maelezo yanayotolewa kwenye Sheria Kadhi anatajwa lakini *practically* yeze mwenyewe hayupo, sasa sijui ni kwa mantiki ipi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama hapa sitaki nikosee maneno yangu nataka niyazungumze vizuri tu, ni kwamba Mahakama ya Kadhi ilikuwepo katika nchi yetu ya Tanganyika, kabla na baada ya Uhuru ikaondolewa, lakini sababu za kuondolewa hazikuelezw. Kuondolewa au kukosekana kwa Mahakama hii kunawaletea Waislam wa Tanzania Bara madhila na matatizo mengi sana na nitayataja machache kwa ruhusa yako. (*Makofi*)

La kwanza, ndoa ya kiislam iliyofungwa Msikitini na shehe yakitokea matatizo inapelekwa Mahakama ya kawaida, mwisho wa yote inavunjwa na Hakimu anatoa hukumu ile kwa Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 na wakati mwingine mvunjaji ni Hakimu Mwanamke. Sasa mwanamke anampa talaka mwanamke mwenzake, hili ni tatizo! Kwa sheria zetu sisi za kiislamu hairuhusu. Sasa mtuelewe tu kwa sababu

tunapozungumzia Kadhi ni mambo ambayo kwetu sisi waislamu sheria za ndoa hizi zote zimetajwa katika Msahafu nayo ni ibada na kwa muislamu yoyote anayekiuka haya yaliyokuwemo katika Msahafu ni dhambi kwa Mungu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ikitokea mume amepotea au amefungwa jela kwa miaka mingi na ameacha mke, mamlaka hii ya Kiserikali inayotambulika kinchi kutoa talaka ni Mahakama. Kama mke akiona ndoa yake ya Kiislam haijunjiki kwa Mahakama au katika Mahakama ya Kiselula atabakia anateseka bila ya ufumbuzi, hili ni tatizo pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine na yanatokea katika jamii zetu tunayashuhudia katika taarifa za habari, katika magazeti tunasoma, ni kwamba yanatokea kabisa. Mume muislamu anapomuo mke muislamu halafu akawa na mke mwingine ambaye si muislam labda mkristo kwa ndoa ya Bomani anapofariki mume huyu muislamu atarithiwa na mke muislamu na mke mkristo. Marehemu muislamu kurithiwa na mkristo ni kinyume na mafundisho ya dini ya Kiislamu, na haya yanafanyika kwenye Mahakama zetu hili ni tatizo kubwa zaidi.

Sasa nayasema haya kwa sababu ya mafundisho yetu sisi ya kidini na mtu ambaye anatakiwa ayatatuwe haya kwa kufuata sheria zetu za kidini ni Kadhi kwa sababu kuna maelekezo mengi sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, madhara zaidi ni pale inapotokea makundi mawili ya waislamu msikitini yanapotofautiana kuhusu usahihi wa ibada fulani wakagombana wakapelekana Mahakamani halafu Hakimu siyo muislamu na anatakiwa atoe hukumu ni kundi lipi kati ya makundi haya mawili lipo sahihi kiibada. Sasa hili ni tatizo lingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa mwenyekiti, lakini vilevile cha ajabu ni kwamba katika kadhia hii Shehe akiitwa kuja kusaidia Sheria za Kiislamu Mahakamani jambo hilo linaonekana linafaa na linakubalika lakini ukifanywa mchakato ili shehe awe na Ofisi ya Mahakama, ahukumu hili ni tatizo lingine, ambaye hapa anatakiwa awe Kadhi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hapa mimi ninukuu tu kwa sababu gani nasema mambo ya mirathi, ndoa, talaka na yatima yote haya sisi yamebainishwa ndani ya *Quran* na tumeambiwa katika hukumu zake lazima mzifuate hivyo, ni amri ya Mwenyezi Mungu sisi hatuwezi tukakiuka. Sasa hiyo *concept* tuelewe na watuelewe wenzetu, lazima tuvumiliane kidini ili kuleta amani na utulivu haya mambo mengine yanatakuwa ni magumu kwetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano nikisema katika suala la talaka *Quran* inatuambia, nitaisoma kwa Kiswahili, *Suratil-bakara*, juzuu ya pili, aya 229, tunaambiwa; “Talaka ni mara mbili, kisha ni kukaa kwa wema au kuachana kwa vizuri wala siyo halali kwenu kuchukua chochote mlichowapa wake zenu.” (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunaambiwa hivyo, sasa nani atakayefundisha haya katika kuwasuluhisha wale watu wawili wanaoachana amba ni waislamu? Hizi sheria anayeweza kutafsiri ni Kadhi ya Shehe. (*Makofi*)

Vile vile aya ya 230 katika sura hiyo hiyo na kama mmempa talaka ya tatu basi si halali kwake baada ya hayo mpaka aolewe na mume mwininge, ukimuacha takala tatu huwezo ukamrudia yule mke ni lazima aolewe na mume mwininge, sasa huyo mume mwininge akimuacha ndiyo wewe unaweza ukamrudia. Huwezi ukamuacha talaka tatu halafu ukaenda Mahakamani ukafanya *lobbing* zako ukaja ukamuoa tena wewe utakuwa siyo muislamu sawasawa, mimi nazungumzia waislamu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika yatima *Quran* inatuambia katika *Suratil...* juzuu ya nne aya ya pili; “Nawapeni yatima mali yao wala msibadilishe kibaya kwa kizuri, kizuri cha yatima mkakichukua ninyi halafu kile kibaya mkawapa wao, hapana! Wala msile mali zao pamoja mali zetu, hakika yote hayo ni jukumu kubwa.” Jukumu kubwa hapa ni dhambi kubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona jinsi yatima wanavyodhulumiwa mali zao na haya matatizo yapo katika jamii yetu lakini kwa sisi waislamu tuna taratibu zetu za kumaliza haya matatizo, tunaisaidia Serikali. Sasa kila mambo yakienda Mahakama, Mahakama mambo mengine waislamu wanataka wafuate taratibu kama walivyoamrishwa na *Quran*. Sasa hili ni tatizo. Aya ya tatu inasema na ikiwa kuna watu wanaoa kwa wingi na wanazaa watoto wengi halafu mnashindwa kuwatunza wewe ukifa sasa unakuwa umeacha watoto yatima wengi wanapata taabu lakini *Quran* inatuelekeza tufanye vipi. Tunaambiwa kwamba; “Na ikiwa mnaogopa kuwa hamtawafanyia yatima uadilifu basi oeni mnaowapenda katika wanawake wawili au watatu au wanne na mkiogopa kuwa hamuwezi kufanya uadilifu basi mmoja tu.” (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah na huo ni ushahidi kwamba ulikuwa mtoto wa Kadhi, ahsante sana. Sasa ninamuita Mheshimiwa Mheshimiwa Hassan Kigwalilo, lakini simuoni lakini basi huu mpira naupeleka kwa Mheshimiwa Bernadeta Mushashu, atafuatiwa na Mheshimiwa Diana Chilolo na Mheshimiwa Mgana Msindai ajiandae. (*Makofi*)

MHE. BENADERTA K. MUSHASHU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi na mimi niweze kuchangia kwenye hoja hii. (*Makofi*)

Kwanza kabisa napenda kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wakurugenzi wote kwa kuandaa hotuba hii nzuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile ningependa kuipongeza Wizara hii hasa hasa kwa kuwateua Majaji wengi, hii inaonyesha kwa jinsi gani Wizara hii inavyotambua uwezo wa wanawake na mchango wao katika kuendeleza Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii mimi nitajikita kwenye sheria amba naona zinakinzana. Ya kwanza ni sheria ya mirathi. Mgawanyo wa mali hufanywa kwa

kuzingatia wosia lakini kama wosia hakuna basi kuna sheria tatu tofauti zinazotumika. Ya kwanza ni Sheria ya Kidini hasa hasa dini ya kiislamu ambapo inatumika kwa wafuasi wa dini ya Kiislamu. Kuna Sheria ya Urithi ya India ya mwaka 1865 ambayo inatumika kwa mtu ambaye hakuwa anafuata sana mambo ya dini, lakini vile vile hakuwa anafuata mambo ya kimila ambapo mjane anapewa moja ya tatu ya mali za marehemu na watoto wanapewa mbili ya tatu ya mali ya marehemu.

Vile vile kuna Sheria za Kimila zilizotangazwa kwenye kitabu cha Serikali cha mwaka 1963 ambazo zinawaweka warithi katika *grade* tatu. *Grade* ya kwanza ni mtoto wa kiume mkubwa ambaye anatoka katika nyumba kubwa na *grade* ya pili ni watoto wa kiume wengine na *grade* ya mwisho ya tatu ni watoto wa kike ambao huwa wanapewa mali ndogo sana, mjane hana chochote ambacho ni cha kwake, huruhusiwa kukaa kwenye nyumba hadi hapo atakapokuwa amefariki au atakapoolewa tena. Kama marehemu hakuacha mtoto basi mali zake zinarithiwa na ndugu zake yaani baba, mama na ndugu zake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria hii nasema kwamba inabidi irejewe kwa sababu vile vile ina kipengele kinachomruhusu mjane kurithiwa na shemeji zake na hii inaongeza UKIMWI. Sehemu kama Bukoba, Karagwe na Muleba kama mnavyojua sisi tuna mashamba ya kudumu yaliyolimwa na babu zetu na yamekaa kwa muda mwingi na kwa hiyo, mashamba yote na ardhi yote ni ya ukoo. Kwa maana hiyo basi, mtoto wa kike na mjane hawawezi kurithi ardhi kwa sababu ardhi yote ni mali ya ukoo. (*Makofi*)

Sasa nakumbuka siku moja nilikuwa nasoma kitabu kimeandikwa na *TGNP* wanaonyesha mama mmoja amefukuzwa na mume wake ana mzigo mmoja kichwani na mtoto mgongoni sasa kasema ngoja nikimbilie kwetu alipofika njia panda akakumbuka loh, na kwetu mali yote ni ya ukoo siwezi kurithi kwa sababu ardhi ile ni ya ukoo, akageuka kutaka kurudi kwa mume akakumbuka kwamba kule amefukuzwa na kule ardhi ni ya ukoo na yeye si mwanaukoo. Basi akasimama akasikitika, akajituliza akisema mimi ni mwanamke hivi kwetu ni wapi? Ninachosema ni kwamba Sheria za Kimila zimepitwa na wakati na zinaendelea kumnyanyasa mwanamke hivyo inabidi kurekebishwa. Lakini pia ninapenda Waziri atueleze basi ni lini hizi sheria tatu za mirathi zitaoanishwa kusudi waandae sheria moja tu ya mirathi ambayo itatumika katika nchi hii. (*Makofi*)

Sheria ya Ardhi, sheria ya Ardhi ya mwaka 1999 na Sheria za Ardhi ya Vijiji ya mwaka 1998, *article 20* na *article 60* zinamruhusu mwanamke kurithi ardhi vile vile zinaruhusu kabla ya mali ya familia haijauzwa kwamba wote waridhie mwanamke na mwanamume watoe ridhaa. Lakini sheria hii vile vile inakumbatia sheria za kimila kwa sababu inasema pale inapotokea utata lazima warejee kwenye Sheria za Kimila ambazo tumeshaona kwamba zinaendelea kumkandamiza mwanamke. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 ina upungufu mwingi sana na inaendelea kumnyanyasa mwanamke. Sheria hii inamruhusu mwanaume kuoa wanawake wengi *polygamy*, lakini inapofika kwa upande wa mwanamke imenyamaza kimya. Nasema huu ni ubaguzi! Sheria hii vile vile inamruhusu mtoto wa kike kuolewa

kwa ridhaa ya wazazi akiwa na umri mdogo wa miaka 15 na mtoto wa kiume kuoa kwa miaka 18 huu ni ukatili wa kijinsia kumuosa mtoto akiwa bado mtoto mdogo, kumchagulia mume badala ya yeye kungoja ufile muda kumchagua yule ampendaye. Hivi mimi najiuliza, ninyi mnaowaoa watoto wadogo wa miaka 15 mnapata raha gani? Kwa sababu kwa kawaida hawa watoto wanaozwa kwa wazee, unakuta mtoto wako wa miaka 15 kaolewa na libaba limoja la miaka 70 hivi utajisikiaje? (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Ndoa inakinzana na Sheria ya Elimu pamoja na Sera ya Elimu na Mafunzo ambazo zinaainisha umri wa mtoto wa kwa shulen. Hivi sasa Wizara ya Elimu inajitahidi kupanua elimu ya sekondari kusudi watoto wengi waweze kusoma sekondari. Je, kama mkiwaoa hawa mabinti wa miaka 15 ina maana kwamba mtakuwa mmewanyima haki yao ya msingi ya masomo ya sekondari. Watoto wako wengi wanaomaliza elimu ya msingi na akimaliza tu elimu ya msingi anaolewa akiwa na umri wa miaka 14 au 15, ukienda kushtaki yule aliyemuoa anasema mimi huyu nimemuo, sheria inaniruhusu ana miaka 15 na bahati mbaya mtoto yule unakuta amechaguliwa kuingia shule ya sekondari lakini hawezi kwenda kwa sababu lijibaba limoja limeshamuo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto kufukuzwa shule wakipata mimba. Takwimu tulizoziona wiki iliyopita zimeonyesha kwamba hadi mwaka jana yaani 2007 watoto wa kike zaidi ya 18,000 wamefukuzwa kutoka shulen kwa sababu ya mimba za utotonii. Ningependa kuiuliza Serikali hao watoto wa kike bila shaka wanapewa mimba na wanaume, je, ni wanaume wangapi ambao wamewapa wasichana hawa mimba wamekamatwa na kuchukuliwa hatua za Kisheria. Wengi wa watoto hawa wanaofukuzwa ni watoto wanaotoka katika familia zilizoduni na familia maskini. Unakuta kwamba wanakosa elimu, wanakuwa maskini, wanakuwa ombaomba na wengine wanazimika kufanya biashara ya ngono ili waweze kujitunza wenye na kumtunza watoto waliowazaa. Lakini nikuambie watoto wa watu wenye uwezo wakishapata mimba wanazaa na wazazi wanaendelea kulea wajukuu kisha wanawapeleka watoto wao kwenye *private schools* hata *international schools*. Kwa hiyo, sheria hii *actually* inawaumiza watoto wa walalahoi. Ni lini basi sheria hii itarekebishwa kwani imepitwa na wakati na vile vile inaonekana kwamba inamuadhibu mtoto wa kike peke yake. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninamuomba Waziri kabla hajahitimisha hoja yake atueleze hizi Sheria nilizozisema ambazo zinamnyanyasa mwanamke ni lini zitaletwa hapa ili kusudi ziweze kurekebishwa? Nasema hivyo kwa sababu nilipokuwa nasikiliza hotuba yake amesema kwamba sasa ndiyo wanaandaa kukusanya maoni. (*Makofî*)

Mwaka jana nakumbuka ulikusanyika mkusanyiko wa watu zaidi ya 800 wakachukua maoni yao na sasa hivi anasema kwa mwaka 2008/2009 wataendelea kukusanya maoni, nina wasiwasi itafika mwaka 2010 tutakuwa tumeshindwa kutekeleza Ilani ya Uchaguzi. Hizi Sheria zitakuwa zimeshindikana kurekebishwa. Napenda basi na naomba wakati anahitimisha hoja yake atueleze ni lini na atupe tarehe na wakati, ni lini hizi Sheria zitakuwa zimeletwa hapa kwa ajili ya marekebisheso? (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema najikita kwenye Sheria ambazo naona kwamba zinakinzana, kuna Sheria ya Maji ya mwaka 2002 na Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004. Sheria zote hizi zina vipengele vya utunzaji au kuhifadhi vyanzo vya maji. Sheria ya Maji hairuhusu kufanyika shughuli za kudumu za binadamu katika mita 200 kutoka kingo za mto au vijito na mita 500 kutoka kwenye maziwa au bahari. Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004 katika kipengele cha 57(1) hairuhusu kazi za kudumu za binadamu kufanyika kwenye maeneo ya vianzio vya maji mita 60 kutoka kwenye hivyo vianzio vya maji. Sheria hizi zinakinzana pamoja na kwamba kipengele namba 232 kinaipa uwezo Sheria ya mazingira kuamua umbali huo lakini ukienda sasa kwenye utekelezaji wananchi wanasumbuliwa. Akienda mtu wa mazingira anamuambia mita 60, akienda mtu wa maji anamuambia mita 200 au 500. Tunaomba hizi Sheria zioanishwe kusudi ziweze kurekebishwa na kuondoa utata huo ili kumsaidia yule mtekelezaji na kuondoa karaha kwa wananchi.

Misho, nakumbuka sana Rais alisema mikataba lazima yote irudiwe na kurejewa na tunajua kwamba Tanzania ipo mikataba mingi mibovu ambayo inawanufaisha wawekezaji. Hasa hasa mfano ni mikataba ya madini ambayo unakuta wawekezaji wanakuja wanachimba madini yetu, yataisha sisi tutabakia na mashimo wakati tumepata faida ndogo tu. Kwa hiyo, ili tuisimamie Serikali yetu vizuri na tuweze kusimamia raslimali za nchi yetu Wabunge wengi kwenye mijadala mbalimbali wameomba kwamba mikataba iletwe Bungeni, mikataba mikubwa mikubwa ili tuweze kuipitia. Naomba Waziri anieleze ni lini sasa Muswada wa kuliwezesha Bunge kuweza kupitia hiyo mikataba mikubwa ambayo inaingiwa na Serikali kusudi tuweze kudhibiti rushwa na kusimamia raslimali za nchi italetwa hapa ili kulipa Bunge nguvu ya kuweza kufanya kazi hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo naomba Waziri atakapokuwa anahitimisha basi atueleze hasa hasa hizo Sheria ambazo zimejadiliwa kwa miaka nenda rudi watu wa *TGNP*, *TAWLA*, *TAMWA*, *WLAC* na wote wanaharakati kila siku wanasema juu ya sheria hizi hizi lakini mtoto wa kike na wanawake wanaendelea kunyanyaswa. Ni lini zitakuwa zimerekebishwa ili kusudi tuweze kutulia? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Bernadeta Mushashu, mchango wako ulikuwa mzuri tu kwa sababu umefanya utafiti wa kutosha tunashukuru sasa.

Sasa nitamuita Mheshimiwa Diana Chilolo na atafuatiwa na Mheshimiwa Mgana Msindai, lakini sasa na Mheshimiwa Hassan Kigwalilo, nimemuona yeye atafuatia baada ya hawa wawili. (*Makofi*)

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, ili nami niweze kutoa mchango wangu kwa jioni hii ya leo kuhusu bajeti ya Wizara ya Sheria na Katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kutoa mchango wangu, naomba nitumie nafasi ya awali kabisa kuunga mkono hoja. Naunga mkono hoja nikiwa na maana kwamba, Mheshimiwa Chikawe, Waziri wa Sheria na Katiba, amejitahidi sana kuwasilisha bajeti yake, ameainisha vya kutosha na vipaumbele tumeviona, nawapongeza wote pamoja na Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Watendaji wote walioshiriki katika kuandaa bajeti hii, tunawatachia kheri, Mungu awatangulie ili waweze kutekeleza bajeti yao barabara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo, sasa naomba nijikite katika maeneo kadhaa ambayo nitahitaji ufanuzi wakati Waziri atakapokuwa anafanya majumuisho kesho. Naanza na uhaba wa Mahakimu katika Mahakama za Mwanzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemsikiliza Mheshimiwa Kaka yangu Chikawe kwa makini sana wakati akiwasilisha bajeti yake na jinsi ambavyo anajitahidi kuhakikisha Mahakimu wanatosheleza katika Mahakama zetu, lakini bado kazi hiyo haijafanyika ipasavyo. Nasema hivyo nikiwa na mifano sahihi kabisa, katika Mkoa wangu wa Singida, nitatoa mfano katika Wilaya ya Iramba, nikienda Tarafa ya Ndago, kuna Hakimu katika Mahakama ya Mwanzo ambaye anahudumia Mahakama tatu, Mahakama ya Ndago, Kaselya na Mahakama ya Urughu. Mahakama zote hizi tatu zipo mbali na eneo analokaa Hakimu, naye ni mmoja, je, hivi kweli atawenza kuhudumia hizi Mahakama tatu ukizingatia hata usafiri hana? Kutoka Ndago kwenda Urughu, ni kilomita ishirini na tano na ni pori tupu, Hakimu hana usafiri, je, Hakimu huyu atawenza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana Mheshimiwa Waziri pamoja na jitihada zake za kutafuta Mahakimu, atafute njia mbadala za kuwasaidia Mahakimu hawa ili waweze kufanya kazi zao barabara. Njia mbadala ambazo nadhani inaweza kumsaidia ni kuwapa usafiri. Nimemsikia ana pikipiki kama hamsini na ngapi sijui atazisambaza huko Mikoani lakini bado pikipiki hizo hazitoshi. Naomba sana kama kweli tunataka kuwasaidia Mahakimu ili waweze kufanya kazi zao barabara, tuhakikishe wote wanapata usafiri huo wa pikipiki angalau wasaidie kufika kwenye vituo vyao vya kazi ili waweze kuhudumia zile Mahakama mbili au tatu wengine wanassema mpaka tano. Bila kufanya hivyo, naona tutakuwa hatujasaidia Mahakimu wetu, watacaa kwenye kituo kimoja, kesi nyingine hazitaendeshwa kwa sababu si sehemu zote ambazo zina usafiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu kama Urughu, hakuna magari ya abiria, unafikiri Hakimu huyu atafika Urughu kwa staili gani na si eneo hilo tu hata ukienda Kiomboi, Hakimu yule yule anahudumia Kiomboi, Kisiriri na maeneo mengine. Kwa hiyo, yote haya ni kazi kweli kweli, tunaomba sasa Wizara pamoja na ufinyu wa bajeti tuwe wabunifu, tutafute mbinu mbadala za kutafuta fedha, tusitegemee fedha za kupewa na Serikali, tutafute mbinu nyingine za kupata fedha. Nina hakika kama tutakuwa

wabunifu, tutatatua matatizo mengine nje ya bajeti ya Serikali. Nadhani tukifanya hivyo, tutakuwa tumejitahidi sana kuhakikisha mipango inakwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hoja hiyo, nataka nizungumzie Mahakama ya Wilaya ya Iramba. Mahakama ya Wilaya ya Iramba tumeletewa Hakimu wa Wilaya ambaye amekaa pale miezi mitatu tu leo hii nimepiga simu naambiwa amestaafu. Hivi kweli unamhamisha mtendaji wa Serikali, unampeleka mbali, anakaa miezi mitatu anastaafu, bado tena umrudishe kwao Moshi, hivi kweli tunatunza fedha za Serikali? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba twende na *data*, kama kweli tunataka kusaidia Watanzania twendeni na *data*, tulikuwa hatuna sababu ya kumhamisha Hakimu kwenda kukaa miezi mitatu wakati tunajua anastaafu? Ni bora tungetafuta Hakimu ambaye angeenda kule na kukaa kwa muda mrefu ili aweze kuhudumia Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anafanya majumuisho, atuambie atatuletea Hakimu wa Wilaya katika Wilaya ya Iramba ama vipi kwa sababu Mahakama hiyo imekwishakaa kwa muda mrefu bila Hakimu, leo hii huyu kaja kakaa kwa miezi mitatu tu anaondoka. Tunaomba tufikiriwe kuletewa Hakimu kijana mwenye uwezo na nguvu, atakayekuja kufanya kazi pale kwa kipindi kirefu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuongea hilo, naomba nizungumzie kuhusu ujenzi wa Mahakama Kuu katika Mkoa wa Singida. Naishukuru sana Serikali kwa sababu inapenda kupokea hoja za Waheshimiwa Wabunge wanapositoa hapa Bungeni. Nakumbuka nilikwishawahi kuongea hapa mara kadhaa kuhusu tatizo la Mahakama Kuu Singida baada ya kupata maelezo ya kutosha kwamba kesi za mauaji Singida ni nyingi.

Mheshimiwa mtani wangu Mary Nagu, alipokuwa Waziri wa Wizara hii, akanijibu hapa kwamba tunapata Mahakama Kuu Singida hata kwenye bajeti hii nimesikiliza kwa makini, Mkoa wa Singida upo lakini cha kusikitisha hata senti tano ya kuanzia hatujabjetiwa. Kiwanja tumeshapata na kama mnavyofahamu wana-Singida ni wapenda maendeleo, shughuli za Serikali zinashirikisha wananchi, tayari tumeshajipanga kujenga, tuna eneo, hivi jamani Mheshimiwa Waziri ameshindwa kutupangia hata fedha kidogo tuweke hata msingi, hicho kiwanja kikija kuchukuliwa itakuwaje? Si kuna muda ambao kiwanja kikikaa bila kujengwa kinachukuliwa? Naomba sana Mheshimiwa Waziri katika majumuisho yake, atuambie atatupa shilingi ngapi angalau wana-Singida tuone *seriousness* ya Serikali katika kujenga Mahakama Kuu Mkoani Singida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuongelea hilo, nataka nizungumzie kuhusu posho za Wazee wa Mahakama. Wazee wa Mahakama wanafanya kazi nzuri, ni wazee wanaosaidia Mahakimu kufanya maamuzi mazuri kwa watuhumiwa wa kesi mbalimbali kwenye Mahakama zetu lakini wazee hawa kwa kweli tunawasahau kwa kiasi kikubwa sana. Hivi Mzee wa Mahakama, unampa kesi moja shilingi elfu moja na mia tano kesi yenye inachukua miezi mitatu, Mzee wa Mahakama bado anatembea Mahakamani kwa ajili ya shilingi elfu moja na mia tano. Jamani *is it fair*, tunawatendea haki hawa wazee? Kama kweli Serikali ya Tanzania tuna mkakati wa kumaliza rushwa, tufikirie kuwaongezea fedha wazee hawa. Tufanye hata shilingi elfu tatu kwa kesi, hatuwezi kumtembeza mzee wa baraza kila siku kwa kuifuata shilingi elfu moja na mia tano jamani, hivi mwenye tatizo lake hata kama hana haki, akimshikisha mzee wa Mahakama shilingi elfu kumi ataikataa, wakati uhakika wa kuishi nyumbani kwake hana, hawezi kukataa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana kupitia Bunge hili tutazame upya kabisa gharama ya kumlipa Mzee wa Mahakama anapoisimamia kesi moja katika Mahakama zetu. Naamini tukiwafikiria hawa wazee, ni namna mojawapo ya kuwasaidia kuachana na rushwa, vishawishi wanavipata kwa sababu ya ukata, kwa sababu ya kuisubiri shilingi elfu moja na mia tano kwa muda mrefu. Mheshimiwa Waziri, nina hakika amenisikia na atalitolea maelekezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba nizungumzie kuhusu maslahi ya Mahakimu hasa wa Mahakama za Mwanzo, Wilaya na Mkoa. Kwa taarifa ambazo ninazo, Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo ana *Diploma* lakini Hakimu huyu anapoanza kazi anaanza na kima cha chini, hivi kweli kama Hakimu anaanza na kima cha chini, je, mhudumu aanze na nini? Elimu yake yote aliyoisotea, kasoma mpaka *Form Six*, akaenda akachukua *Diploma* yake akarudi, leo anaanza na kima cha chini, si ndiyo maana tunakuwa na upungufu wa Mahakimu, anapoangalia mshahara wake anasema ahaa, anawahi eneo lingine, anasema nakwenda kuwa Mwanasheria katika Ofisi fulani, si fani inamruhusu bwana, anaondoka. Tuangalie namna ya kuboresha maslahi ya Mahakimu, nao vilevile ni binadamu na wanashawishika, tuwanyime vishawishi kwa kuwaongezea maslahi yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuongelea hilo, naomba sasa niongelee juu ya Tume ya Haki za Binadamu. Naipongeza Tume hii inafanya kazi nzuri na timesikia, wametembelea taasisi mbalimbali za Serikali na kutoa elimu na mambo ambayo yamefanikiwa kutokana na Tume hii tunayafahamu. Sasa naomba Tume hii ielekeze nguvu zake kwenye jamii, jamii ielimishwe na jamii itaelimishwa baada ya Tume hii kutoka Dar es Salaam kwenda Mikoani, Tume iende Mikoani ipige kambi, iwapokee wadau mmoja mmoja wenye kero zao. Wananchi wetu wana kero nyingi, wapo watendaji wa Serikali Miungu mtu, wananyanyasa wananchi, wapo wanaume wanaonyanyasa wake zao na wapo wanawake pia wananyanyasa waume zao na wako matajiri wanaonyanyasa maskini. Naomba Tume hii iwe *mobile*, suala la kukaa Dar es

Salaam halisaidii na wanakaa Dar es Salaam kwa sababu hawana fedha, wawezesheni waweze kwenda Mikoani kutoa elimu ili wananchi wapate haki zao. Sitaki kuliongelea kwa kirefu kwa sababu hata wenzangu wamelieleza sana na Serikali yetu ni sikivu, naamini hili litakuwa limesikilizwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nizungumzie Tume ya Kurekebisha Sheria, Mheshimiwa Mushashu, ameongea hapa, hivi kweli bado tunatumia Sheria za mwaka 1948, Sheria ya Kutoa Matunzo kwa Watoto, Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971, mpaka leo akinamama bado wanakosa haki zao, watoto wanakosa matunzo kwa sababu ya Sheria tu! Leo tumeambiwa tayari Tume imeshapitisha haya na kumkabidhi Waziri, Mheshimiwa Waziri atuletea hapa haraka, wananchi wetu wanaendelea kupata tabu, kukandamizwa, atuletee Sheria tuzipitishe ili zifanye kazi, tutapembua hizi Sheria mpaka lini, wazilete hapa tuzipitishe. Nina hakika zikiletwa hapa wananchi wetu watafurahi kwa sababu haki zao za msingi sasa zitapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumzia hilo, naomba sasa niongelee kuhusu ucheleweshaji wa nakala za hukumu. Tatizo hili lipo, kama Serikali ilikuwa haifahamu lipo sana. Watu wetu wanamaliza kesi, wanakwenda kuomba hati ya hukumu, lakini wanaishia kutembea hata mwezi au miezi miwili, hati ya hukumu hawajapata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilijaribu kulifuatilia suala hili, nimekuja kubaini kwamba tatizo ni ukosefu wa Makarani. Tunaomba Makarani waongezwe katika Mahakama zetu. Makarani wakiongezeka, kazi hii itafanyika na si Makarani tu hata vitendea kazi, miundombinu inayotumika imeshapitwa na wakati. Sasa hivi tupo kwenye teknolojia ya kisasa, tunakwenda na mambo ya *computer*, pelekeni *computers* kwenye Mahakama zetu ili wananchi wanapomaliza kesi zao waweze kupata nakala zao za hukumu kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuongelea hilo, naomba sasa nizungumze kuhusu ukarabati wa Mahakama. Ndugu zangu, ni kweli sasa mnapeleka Mahakimu wachache, tunawaona lakini wanakwenda kufanya kazi kwenye mazingira magumu sana, kwenye magofu, hata ile hadhi ya kumwita Mheshimiwa Hakimu, inakuwa haipo kabisa. Ndiyo maana hata wahalifu wanapopelekwa wanaona mazingira ya ajabu ajabu tu hata kule kubadilika tabia inakuwa kazi. Tunaomba pamoja na kuzalisha Mahakimu na ukarabati uende sambamba ili Mahakimu wetu waweze kufanya kazi katika mazingira mazuri, Mahakama zetu ziwe nzuri na vilevile tuwe na sehemu za mahabusu kwa sababu mahabusu kwa mfano Singida Mahakama zote za Mwanzo wanakaa Wilayani, hivi kuna magari mangapi ya kusambaza mahabusu hawa? Tunaomba sana katika ukarabati...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika
muda wa mzungumzaji)*

MHE. DIANA M. CHILOLO: Nimemaliza?

MWENYEKITI: Endelea!

MHE. DIANA M. CHILOLO: Nashukuru sana. Mheshimiwa Mwenyekiti.....

MWENYEKITI: Mheshimiwa Chilolo...

MHE. DIANA M. CHILOLO: Ni kengele ya pili?

MWENYEKITI: Nina wasiwasi ni ya pili.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

MHE. MGANA I. MSINDAI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami nichangie katika hotuba ya Wizara ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri anayofanya. Mheshimiwa Rais aliona anaweza kusimama peke yake na kweli akapandishwa akawa Waziri bila Naibu Waziri, hiyo yote ni kwa sababu ya uwezo alionao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwapongeza sana Katibu Mkuu, Jaji Mkuu na wengine wote ambao wanaongoza Wizara hii, ni Wizara ngumu, kubwa na fedha kidogo. Naiomba, Serikali katika miaka inayokuja iwaongezee fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asubuhi wakati Waziri anasoma hotuba yake, kuna kipengele kilinistua na nikaona nianzie na hicho. Walisomwa Makaimu sita, tena wanakaimu zile nafasi kubwa kubwa. Naomba kunukuu:-

“Kaimu Katibu wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Kaimu wa Tume ya Kurekebisha Sheria, Kaimu Mwandishi Mkuu wa Sheria, Kaimu Mkurugenzi wa Katiba na Haki za Binadamu, Kaimu Mkurugenzi wa Utawala na Kaimu Afisa Mtendaji wa RITA”.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiki kitu kimenigusa sana na ninapenda nijue wamekaimu kwa muda gani kwa sababu miongozo ya Serikali inasema mtu anakaimu kwa miezi sita baada ya hapo anakuwa *confirmed* au kama hafai anaondolewa. Inawezekena kabisa kama wamekaimu muda mrefu wameanza kukata tama. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri amalize tatizo hili, kama muda bado, asubiri lakini kwa wale ambao wameshaptisha miezi sita, ni aibu kuendelea kukaimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niongelee juu ya Chuo chetu cha Lushoto. Kile ndio chuo tunachokitegemea, ndio chuo ambacho kimeanzishwa na tukasema kitasaidia kutuondolea matatizo ya Waheshimiwa Mahakimu wa ngazi ya kati na Mahakimu wa Mahakama ya Mwanzo lakini inaonyesha chuo hicho hakitoshi na mpaka sasa kinakwenda kwa shida sana, bajeti yake ni ndogo sana. Naomba sana Serikali ikiangalie sana chuo hicho kwa sababu ndio jicho lake, hapo ndipo watatoka Mahakimu ambao wataondoa matatizo mengi ambayo yanaikabili nchi hii. Kwanza kwa sasa kiwezeshwe, kipewe vitendea kazi na vilevile kipanuliwe ili kichukue wanachuo wengi zaidi. Wote hapa tunalia uhaba wa Mahakimu, kwangu wapo wawili tu katika Jimbo langu lote, tutalia uhaba wa Mahakimu lakini hatutafanikiwa tusipofanya hivyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nimpongeze sana Mheshimiwa Rais, kwa kuteua Majaji wengi akina mama na hata Lushoto akinamama wengi sana wanamaliza. Nina imani kabisa watatusaidia wakiungana na hawa wa kiume tulionao na kazi zitakwenda vizuri sana. Akinamama ni watu ambao kwa kweli kushawishika kwa vitu vidogo vidogo, huwa ni wagumu sana na nitatoa mfano wa kule kwangu. Mahakama ya Mwanzo ya Nduguti, tulikuwa na usumbufu sana wa mambo ya ardhi na kila Hakimu alikuwa akienda pale anaishia kuzua migogoro lakini nilipowaomba viongozi wa Mahakama, wakamleta Mama Shani, kwa kweli amekaa pale kwa miaka mitatu, vurugu zikaisha na kutoka pale akaenda kusoma Lushoto, sasa kwa sababu ameshapanda, sijui nitarudishiwa au atakwenda pengine? Vilevile naomba wajue pale Nduguti hatuna Hakimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze sana Wizara hii, wamenijengea Mahakama ya Mwanzo na vilevile kama alivyosema Mheshimiwa Chilolo na Mahakama ya Wilaya tumejengewa nzuri, tunawapongeza lakini isiwe mwisho, waendelee kujenga na kwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nirudi kwenye Jimbo langu, bahati mbaya wiki hii, karibu Wizara hii kuwasilisha bajeti yake, kumetokea mambo Jimboni kwangu ambayo ni lazima niyaseme hapa. Kuna mtu mmoja katika Kijiji cha Lylelembu ameamua kuwanyanyasa wenzake na kila akikamatwa akipelekwa anarudi. Mwisho wa mwezi huu alikamatwa, akapelekwa Polisi, Polisi wakampeleka Mahakamani, Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo ya Iguguno, alipopokea lile jalada, akamwachia yule mtu kinyemela na kusema kwamba ametishiwa maisha kwa matusi na si kwa silaha, kwa hiyo huyu mtu hana kosa na sasa yuko nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii kwa sababu sasa hivi inafanya kazi, naomba ichukue ile kesi ya Iguguno iwe mfano, yule mtu akamatwe, sasa hivi anatamba kule kijijini, anasema mtanifanya nini, nimekwenda Hakimu ameniachia na hii siyo Iguguno tu inatokea sehemu nydingi. Naomba Mheshimiwa Waziri na wasaidizi wake watupie macho katika sehemu mbalimbali ili vitendo vibovu kama hivi vinavyotokea vikomeshwe na hawa wachache wanaofanya unyama huu wachukuliwe hatua hata ikiwezekana waachishwe kazi, tupate watu wengine wazuri zaidi, ni heri kuwa na upungufu kuliko kuwa na watu wabovu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wiki ya jana kule Ibaga, wananchi wamejikusanya na Serikali yao ya Kijiji cha Ibaga, nawapongeza sana na waliniipgia simu, wakamkamata Polisi anafanya kitendo cha mapenzi na mwanafunzi wa shule ya Sekondari ya Chemchem na walinijulisha. Nikawasiliana na DC na OCD kwa sababu Polisi walianza kuwa-*harass* vijana wa pale Ibaga, wale wakatumia sheria zao sasa hivi mambo ni shwari lakini mchezo umeanza kuchezwa Mahakamani. Yule kakamatwa *red-handed* anafanya kitendo na mwanafunzi wa sekondari, amepelekwa Polisi baadaye amepelekwa Mahakamani, nasikia Hakimu husika anacheza na hiyo kesi. Tutaendelea hivi mpaka lini? Kwa hiyo, tunaomba, kesi kama hizi ziko sehemu nydingi, tuna imani na Mahakama zetu, kwa kweli Mahakimu wengi na watendaji wengi wa Mahakama, ni waaminifu lakini wachache ndiyo wanaochafua na ndiyo maana unakuja huo msemo samaki mmoja akioza wote wameoza lakini si kweli, ni wale wachache ambao wapo maeneo mbalimbali hapa nchini kwetu. Tunaomba Mheshimiwa Waziri ajitahidi sana kuchukua hatua kwa watu wanaowapaka matope.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vitendea kazi kwa Mahakimu wetu havitoshi, tulishasema hapa hapa Bungeni kwamba jamani zile sheria zitafsiriwe kwa Kiswahili na zishuke kule chini, mpaka leo kuna Mahakimu hawana Sheria tunazopitisha hapa. Kama wanazo ni zile za zamani ambazo hazijawa- *amended*. Kwa hiyo, tunaomba hizo Sheria ziende huko na vilevile Katiba zetu za Kiswahili zitengenezwe nydingi ziende kule chini, wananchi wetu wana uwezo wa kununua na zitawasaidia sana kujuu haki zao, bila kuwasaidia tutaendelea kuwa na shida, tutaendelea kuwalaumu, kitu ambacho si kizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimboni kwangu nina Mahakama tano, ya Ibaga, Kirumi, Nduguti, Iambi, Kinyangiri na Iguguno. Ukienda kuziona, ukitoa ya Iguguno ambayo imejengwa mpya ziko kwenye hali mbaya sana, Mahakimu hawana nyumba wala usafiri. Kwanza, naomba sana hizi Mahakama zetu pale ambapo tunaona hatuna uwezo wa kujenga basi tukarabati zilizopo na kazi ya ukarabati si kubwa, tunaiomba Serikali iionee huruma Wizara hii ya Sheria na Katiba ili waweze kufanya kazi zao vizuri. Kwa kweli inatia aibu kuona Mahakama ilijengwa miaka ya arobaini mpaka sasa haijafanyiwa ukarabati, ili wapande, inabidi wapange mawe kwa sababu hawawezi kupanda, ilishaliwa na maji. Naomba sana tujitahidi kuwasaidia kwa kutekeleza hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, hata sisi humu kuna kipindi tulishaambiwa tukipitisha Sheria, tupewe lakini hata sisi hatuna hizo Sheria ambapo tungkuwa nazo tungkuwa tunawasaidia sana kule. Tunapitisha Sheria basi ndio mwisho wetu, huwezi

kupewa hiyo Sheria ukae nayo. Kule Majimboni tunakaa na Mahakimu na hawana Sheria, sasa tukiwa nazo unaweza kumpelekea atumie. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri, sijui yeje ndiye anahusika, awasiliane na wengine wanaohusika, Sheria zinapopitishwa na sisi tuwe tunapewa nakala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitaki kupoteza muda, ni haya tu ndiyo niliyokuwa nayo, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. HASSAN C. KIGWALILO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia hotuba ya Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Mathias Chikawe. Nampongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na *Attorney General*, Mheshimiwa Mwanyika, kwa kazi nzuri. Pia nampongeza kwa hotuba ambayo imekuwa ni kamilifu na imechukua maeneo mengi na naamini itatekelezeka. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa umahiri wake katika kujibu maswali vizuri Bungeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua pia fursa hii, kuwapongeza Jaji Mkuu, Majaji wote, Mahakimu wa ngazi zote pamoja na watumishi wa Wizara hiyo ambao wanafanya kazi katika mazingira magumu mno. Kabla sijasahau, napenda kusema, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia na sitamsumbua Mheshimiwa Waziri kwa lolote baada ya kukamilisha maelezo yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii, kusema kweli ina kazi nzito na kubwa. Mojawapo au mionganoni mwa kazi hizo, ni kuwaapisha viongozi mbalimbali wa Kitaifa akiwemo Rais na viongozi wa ngazi mbalimbali ili waweze kupata nyadhifa mbalimbali. La kushangaza pamoja na heshima hii, yote walijonayo lakini Serikali haiangalii Wizara hii vizuri ili kuendeleza heshima ya kuwaapisha viongozi. Kwa hiyo, nashauri Serikali iboreshe au iongeze kwa makusudi kabissa bajeti ya Wizara hii ili iweze kufanya kazi zake vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hali halisi ilivyo pamoja na utendaji kazi mgumu lakini pia Wizara hii haina vitendea kazi vizuri kwa mfano, hadi leo wanatumia *typewriter* na zingine sijui ni *Olivet*, *Olympia* na vitu kama hivyo, ukienda kuziangalia hapo zilipo, unakuta baadhi ya herufi zimefutika. Inashangaza kuona katika Halmashauri zetu sasa hivi karibu kila ofisi kuna *computer* lakini Mahakama ya Wilaya inashindwa kupata *computer*, kulikoni?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani lazima wawe na mikakati ya makusudi kabisa kuona wanaboresha hali hii ili angalau katika Mahakama za Wilaya waweze kuwa na kompyuta ambazo zitafanya kazi zake vizuri. Hilo ndilo tatizo kubwa ambalo hata unakuta watu wanbungu' unika kusema kwamba hukumu zao zinachelewa kuchapishwa ili waweze kwenda mbele ya safari, uchapishaji wenye kama ni wa aina hiyo, halafu wanakuja kutumia *stencil*, kusema kweli hali inakuwa ngumu na maandishi yake hayasomeki vizuri hata huko yanapopelekwa. Kwa hiyo, naomba kabisa Serikali katika kuboresha kazi katika Wizara hii, inunue kompyuta angalau katika Mahakama za Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata katika Jiji la Dar es Salaam, Mahakama za Wilaya zingine, bado zinaendelea kutumia *typewriter* za zamani. Sasa kama hivyo ndivyo na Jiji la Dar es Salaam ndiyo kioo cha Tanzania nzima, sijui tunakwenda wapina wapi tunataka kuanzia kuboresha vitendea kazi katika Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapendekeza Serikalini, hao Majaji ambao wanateuliwa na Mheshimiwa Rais, kila baada ya muda pia wakamilishiwe vitendea kazi vinavyowahusu, maana baadhi yao wanachangia magari, Majaji wawili kutembea katika gari moja si vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu, hao Majaji ikibidi washiriki katika shughuli mbalimbali katika maeneo yetu. Maana Majaji umuhimu wao unajulikana, lakini unakuta ni adimu kuonekana na ni adimu kwenda katika mazingira mbalimbali, wananchi wakawatambua na wakajua jinsi gani ya kufaidika nao kwa namna moja au nyingine na kupata elimu ya kutosha kutoka kwao kwa mfano kutembelea Mikoa na vitu kama hivyo. Lakini unakuta maadam wamekuwa Majaji, wapo tu mahali fulani au wamepewa Kanda basi wanabakia kwenye Kanda. Lakini mara nyingi unakuta kwa kuwa hawana usafiri mzuri huwa wanashindwa kwenda katika maeneo ambayo wao katika Kanda ile ndiyo wawakilishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya Mahakama nchini, kweli zipo katika hali mbaya sana na ukiangalia, unaweza ukafikiria kama ni gereji bubu. Sasa kwa hali kama ile, mtu anakwenda kuapishwa kwenye gereji bubu halafu anapewa wadhifa, atajisikiae? Naomba kabisa Wizara iongeze kasi ya kuboresha Mahakama zetu, wengine wapo kwenye magofu. Hii Wizara kusema kweli pamoja na unyeti wake, ninaamini mpaka sasa hajaipangwi mikakati ya namna gani ya kuweza kuboresha ili tuweze kufaidi matunda yake, majukumu ni makubwa, lakini uwezo wanaokuwa nao ni mdogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii pia, kuipongeza Serikali kwa kutujengea Mahakama, imeshirikiana na wananchi wa Liwale kwa kujenga Mahakama ya Kibutuka. Mahakama hiyo ni nzuri mno na pia ni ya kisasa, nashukuru sana. Napenda pia vilevile kusema kwamba Mahakama hiyo ambayo ni nzuri ilifunguliwa na Mheshimiwa Rais mwaka jana. Lakini pamoja na uzuri huo, bado tuna upungufu mkubwa wa Mahakimu wa Mahakama ya Mwanzo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba kwa makusudi kabisa, Wizara ipunguze urasimu wa kuwaajiri Mahakimu hasa wale wa Mahakama ya Mwanzo. Kwa kuwa, urasimu uliopo ni mkubwa mno kiasi kwamba wengine wanakata tamaa kupata ajira hiyo, si kwamba hawataki kwenda vijijini, wanakata tamaa kupata ajira hiyo. Ukiona unaletewa Hakimu, mara nyingi unaweza kukuta akiwa kijana hachukui muda, wanamhamisha, ila yule mtumishi anayekaribia kustaafu ndiyo wanakuletea, sasa kazi hii itafanyika vipi? Naomba kabisa watusaidie kwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri anatoka Nachingwea na ninaomba kabisa anapokuwa katika Jimbo lake wakati fulani fulani, anapokuwa na

nafasi ya kutosha, afanye ziara kwa Wilaya ya Liwale na kwa kuwa yeye ni Mwanasheria, kwa hiyo itakuwa ni rahisi kwetu sisi kupata mawaidha yake ili tuweze kuona namna gani tunaweza kuboresha Mahakama zetu kwa kujenga sehemu zingine pia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa niliyonayo ni kwamba Liwale imepangiwa gari, lakini mpaka hivi sasa, hiyo gari haijapelekwa katika Wilaya ya Liwale. Maelezo yaliyopo, wanasesma ni kwa sababu za kiutawala. Namwomba Mheshimiwa Waziri, atakapokuwa anahitimisha hoja yake, ajaribu kutuelimisha, hiyo gari sasa itafika lini Liwale? Liwale yenewe ukiangalia ina *square kilometre* 38,000 ambazo ukiangalia hata hiyo Mahakama ya Mwanzo ambayo nimesema imejengwa ipo kama kilomita 70 kutoka Liwale Mjini na Hakimu tunayemtegemea anatoka Liwale Mjini na siku zote anadandia *lift* za kumwezesha yeye kufika katika Mahakama ya Kibutuka, afanye kazi arejee tena Liwale. Hizo *lift* ambazo anadandia na hawezi kusema atumie balskeli kwa *distance* kama hiyo na pia ukizingatia kwamba eneo la Liwale lina wanyamapor wengi sana, tumewahi kupoteza Walimu kwa kuuawa na wanyamapor, tunaendelea kupoteza wanafunzi kwa kuuawa na wanyamapor, tusingetaka kupoteza Mahakimu amba ni adimu kupatikana kwa kuuawa na wanyamapor. Tafadhali sana Waziri azingatie kwamba na sisi tunahitaji gari kama kweli gari lilikuwa linakuja kwetu. Basi namwomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anahitimisha hoja yake, atueleze ni lini gari hilo litapelekwa Liwale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Wazee wa Baraza, kwa kuwa mengine yamekwishazungumzwa, lakini mimi ninataka kuongezea tu ili kuboresha hali za Wazee wa Baraza basi angalau wanetafutiwa posho ya *uniform*. Hawa Wazee wa Baraza kusema kweli pamoja na kwamba *allowance* yao ni ndogo, lakini ukiangalia wanapokwenda kufanya kazi hiyo, ukiambiwa kwamba huyu ndiye Mzee wa Baraza kusema kweli hana hadhi ya kuwa Mzee wa Baraza na Wizara inatakiwa impe hadhi hiyo aweze kuwa na nguo rasmi ya kuweza kufanya kazi hiyo na ndipo tutakapowez kuboresha heshima ya Mahakama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kutokana na hali ilivyo, sasa hivi unakuta Mzee wa Baraza anakuja na *mugolole*, mwagine anakuja na kitu gani sijui, umewapa kazi ambayo kusema kweli wanaipenda na pia wanaweza wakaifanya vizuri, lakini Wizara inatakiwa kuboresha hali zao, posho ya *uniform* inaweza kutolewa mara moja kwa mwaka ambayo pia inaweza ikamsaidia, awe na viatu vizuri, hata kama ni vya *size* anayoitaka yeye, lakini kuwe na hali fulani ya kuona kwamba hao wanaozungumza nao ni Wazee wa Baraza. Siyo hivyo tu, unakuta Hakimu anakwenda pale amevaa tai yake, lakini unakuta Wazee wa Baraza amba anawategemea kushauriana nao wapo katika hali ngumu. Naomba hilo pia liangaliwe vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo mengi yamezungumzwa kuhusu Mahakama. Lakini pamoja na hayo yote, kuna suala la rushwa. Mimi ninaona kwamba suala la rushwa lipate ufanuzi zaidi, kwa kuwa, sasa hivi inaonekana kwamba kila kitu kinachotendeka Mahakamani, ni rushwa ambapo mimi siamini kama ni kutokana na rushwa ama wakati mwagine kutokana na mwananchi mwenyewe haelewi. Kwa hiyo,

kuwepo na elimu na ikibidi pawepo na aina fulani ya mashauri katika Mahakama zetu. Maana yake yeye anachoona ni kwamba ameshtakiwa pale kwanza hataki kukubali kosa, kwa hiyo, anachoamua sasa ni kuona kama anaweza kumshawishi Hakimu au anaweza kumshawishi Karani wa Baraza ili kesi yake ifutwe au isifanywe kwa namna moja au nyingine. Sasa hapo unakuta ni elimu ndiyo tunayohitaji kuisisitiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia basi, hii rushwa imeanza kwenye *society* yetu, maana kwa nini wewe umekosa ufikirie sasa namna ya kukwepa? Maana hata Dereva akiwa kwenye basi akiambiwa simama, anakimbia kutoka kwenye basi anakwenda nyuma kumfuata Trafiki, anakwenda kufanya nini? Kwa nini asingoje Trafiki aje pale kwenye gari azungumze naye na amkamate vizuri? Sasa unakuta *society* yetu pia ina matatizo na ina walakini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu, ukiangalia katika suala la Mahakama, kuna mambo mengi yapo *connected* au yamechanganyika, unakuta mshtakiwa haletwi Mahakamani...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa
muda wa mzungumzaji)*

MHE. HASSAN C. KIGWALILO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Hassan Kigwalilo, ahsante sana. Sasa nitamwita Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir, atafuatiwa na Mheshimiwa Emmanuel Luhahula.

MHE. MUDHIHIR M. MUDHIHIR: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, hoja ambayo ninaiunga mkono kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mambo kadhaa wa kadhaa yanayotutofautisha jamii za samaki na wanyama kwa upande mmoja na jamii za wanadamu kwa upande wa pili. Lakini moja ya sababu hizo au mambo hayo, ni utawala wa Sheria. Kwenye ulimwengu wa samaki, nguru akipita mbele ya papa, ndiyo kiama chake, hivyo hivyo, chaa akipita kwa chewa, ndiyo mwisho wake. Kwa wanyama kama paa akipita kwenye anga za simba anakuwa kitoweo na kadhalika na kadhalika. Kwetu wanadamu ni tofauti, mtoto mdogo anajisikia yupo salama kwa jitu lenye mabavu makubwa kwa sababu sisi tunatawaliwa na Sheria. Madhumuni ya Sheria siku zote ni kuhakikisha kwamba jamii husika inaishi kwa amani, utulivu na raha bila kuwa na wasiwasi wa kudhulumiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini utawala wa sheria siyo kuwepo tu kwa Sheria yenye, lakini lazima Sheria hiyo iwe sheria ya haki. Haya ninayoyasema, yananifanya nikumbuke kauli aliyoitao Mheshimiwa Jaji Mwalusanya katika *Miscellaneous Criminal Case* Na.4 ya mwaka 1988 kule Mwanza *High Court, ni unreported*, kwamba utawala wa

sheria siyo tu kwamba Serikali inafuata yaliyoandikwa ndani ya Katiba na Sheria lakini lazima Sheria yenyewe iwe ni ya haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuwa na sheria ya haki peke yake hakusaidii, lazima hiyo sheria ielewewe. Angalia sisi Waheshimiwa Wabunge hapa, tunafanyiwa semina kabla hatujapitisha Sheria ili tuifahamu, lakini hata hiyo Sheria ikishapita wale watekelezaji huko Serikalini, ile Wizara husika na ile Sheria watakwenda kwenye *workshop* Bagamoyo, watakwenda sijui wapi, kuhakikisha kwamba wanaijua ile Sheria wanayoisimamia. Lakini inashangaza kwamba Sheria hiyo hiyo tunataka ikimfikia mwananchi kule ambaye hakuwepo wakati wa kutungwa, hakupata semina, tunamtegemea siku ile ajue Sheria, huo ni udhaifu katika utawala wa sheria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria si jambo la silika kwamba mtu anazaliwa nalo, Sheria ni jambo la hulka ambalo mtu anajifunza pale inapokuja. Watendaji kule mkisikia wanawakamata watu, wanawaweka ndani kwa sababu hawakuchangia michango ya shule za sekondari, si kweli kwamba wananchi hawapendi kujenga shule za sekondari, si kweli kwamba wananchi wanakataa kujenga Vituo vya Afya na Zahanati katika kila kijiji, lakini wananchi wanahitaji kuelimishwa, ile *awareness* ni jambo la msingi na huo ndiyo utawala wa sheria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka kuipongeza Serikali kwa hatua ambayo ilichukuliwa juzi humu Bungeni. Waheshimiwa Wabunge tulilalamika juu ya Waraka wa Mkurugenzi wa Uvubi, lakini Serikali mara moja ikaona kwamba malalamiko yale ni ya msingi, ikatoa kauli humu ndani. Huo ndiyo utawala wa sheria ambazo tunauhitaji na kwa kweli unafaa ufuatwe katika maeneo karibu yote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakumbuka mwaka 1988, nilipata bahati ya kusoma kitabu cha Dr. Harrison Mwakyembe kinaitwa “Pepo ya Mabwege” ambacho kilikuwa kinatumika kwenye fasihi ya *High Level*. Uongozi wa Serikali hiyo, ambayo yeye anaijua, unataka kuwapeleka wale watu kama wao wapo katika *honeymoon*, lakini wale wananchi ni mabwege wafuate tu. Mwananchi kwa kawaida anaitii sana sheria anayojua, kuliko ile ambayo anapelekwapelekwa tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi ninaomba kutoa ushauri, Wizara yetu ya Katiba na Sheria pamoja na kwamba imeanza kugawa vipeperushi, lakini hebu izifikie shule zetu za sekondari, sasa hivi zipo katika kila Kata. Ukienda kule Europe mtoto siku anaanza *nursery school* anaambibiwa pale pale wewe ni mtu kamili mwenye heshima zako na nini, ukimshika tu anakwenda kusema kwa mama yake, ukimgusa mahali popote anakwenda kusema kwa Mwalimu wake. Sisi hapa inafikia mahali mtoto wa umri wa miaka miwili, mitatu, anaambibiwa mchumba, mchumba mpaka anapata mimba, hajui haki zake, haya ni mambo tunatakiwa tuyaanzu kuanzia *nursery school* kule mpaka kufika shule za sekondari. Tutapungukiwa na matatizo mengi ya kubaka watoto kama alivyokuwa analalamika mama yangu Mheshimiwa Maria Hewa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 12(2) ya Katiba yetu inasema:-

“Kila mtu anastahili heshima ya kutambuliwa na kuthaminiwa utu wake.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, heshima ya mtu huyu, haitenguki pale anapotoka peke yake akaingia kwenye kabilia lake au kwenye Chama chake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana nilisimama hapa kueleza machungu tuliyonayo sisi Wamachinga kwa kabilia kwamba Serikali sasa imeamua ku- *formalize* kwamba Wamachinga hao ndiyo watu amba wanavaa kandambilii kuanzia Jumatatu mpaka Jumapili, nguo zimekuwa ngozi hazivuliwi, hazibadilishwi. Nilitaka kupata maelezo ya Serikali kwa nini inalifurahia suala hili. Mimi ninataka nikubali kabisa kwamba sisi wa kutoka Lindi na Mtwara kwa sababu ya mazingira yetu ya wakati ule, tulilazimika kuja Dar es Salaam kufanya biashara ndogo ndogo, walivyotuunga mkono wenzetu tumekuwa wengi, sasa kuna Wamachinga na wasiokuwa Wamachinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hivi kweli Serikali inakupendezeni kwa sababu tu sisi tulikuwa waanzilishi basi sasa kila anayefanya biashara hiyo ni Mmachinga? Maana mkiruhusu hilo, msikataze na mengine. Tunajua kuna kabilia waanzilishi wa kuombaomba pale Dar es Salaam, lakini Serikali hajja-*formalize* kwamba wale omibaomba wapewe jina la hilo kabilia anzilishi. Hili mimi silizungumzii kwa masihara, nalizungumza muone uchungu ule, tuna uhakika tukitaja kwa jina hapa tutashtakiwa na tutaambiwa na Kanuni. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukienda Kigamboni kuna Wagema wa tembo, pombe ya mnazi, ukimwona unajua anatoka Mkoa gani lakini wapo na Wagema wa makabila mengine mbona hatuwaiti kwa makabila yao? Lakini kuna watu walikuwa wanafanya biashara ya miili yao Dar es Salaam, sasa hivi wameunganika na wengine lakini hawaitwi kwa kabilia lao wanaitwa changundoa. Hivyo sisi Wamachinga tuliandikwa na wino gani katika vitabu vya Mungu hata Serikali iamue kutuvunjia heshima kiasi hicho? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimekaa Zanzibar miaka 12, nikiwa mtumishi wa Serikali, sisi watu wa Bara tulikuwa tunaitwa ama Machogo au Wanyamwezi, lakini kwa sababu Serikali ilikuwa haishabikii tulikuwa tunamalizana wenyewe tu. Mimi Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir akiniita “*Chogo*”, mimi namwambia wewe “*Komo*” tumemalizana. Lakini Serikali isijijingize katika hili na yenye ika-*formalize* sasa kwamba kabilia la Wamachinga basi ni kabilia la kurandaranda tu, itatufikisha mahali pabaya. Nimetoka huko, wanaweza kuamua watakavyotuamulia, maana hakimu bwana anatawaliwa na Sheria pale, lakini anatawaliwa vilevile na mazingira yake aliyokulia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, yupo mfalme mmoja alikuwa na watoto watano lakini alichelewa sana kupata wale watoto. Siku moja katika *palace* (kasri) lake, mtu mmoja akapita kule uani akamkuta binti yake anaoga, mtoto akapiga kelele, nachunguliwa. Akakamatwa yule mtu akafikishwa kwenye Baraza la Mfalme kwamba huyu amemchungulia binti yangu wakati anaoga kwenye *swimming pool*. Yule Mfalme akasema mimi nina watoto wakubwa bwana, watoto wangu ndiyo watatoa hukumu,

mtoto wa kwanza unasemaje? Akasema huyu bwana mimi ninachosema apasuliwe kwa msumeno ule mkubwa wa kuangushia magogo kutoka katikati ya utosi mpaka katikati ya nyonga iwe mwisho wake. Mfalme akamuuliza mtuhumiwa umekubali, akasema naam nimekubali. Mtoto wa pili akasema, huyu apigwe na ule msumari mkubwa kwenye utosi mpaka uzame wote, mtuhumiwa umekubali, akasema naam nimekubali. Mtoto wa tatu, akaambiwa vipi kuhusu huyu, akasema huyu kamwangalia dada yetu wakati yu mtupu na ye ye ana haki ya kuangaliwa utupu, kwa hiyo huyu amuo e dada yetu, mtuhumiwa unasemaje, akasema ninakubali. Mfalme akamwambia wewe huna adabu, kila kitu unakubali maana yake nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, akamwambia Mfalme, ninajua utakwenda mpaka mwisho, kamuulize na mama wa nchi hii, Malkia Mtukufu. Alipoulizwa yule mama akasema Mfalme ulikuwa unanilaumu kwa nini ninasali usiku, nilikukosea. Baada ya kuona hatuna watoto kwa muda mrefu basi nililazimika mimi yule Fundi wa kwanza wa kupasua mbaao za kujenga hili kasri, mimi nilifanya naye mapenzi ndiyo nikapata huyu mtoto aliyetao hukumu ya huyu bwana apasuliwe kwa msumeno. Lakini huyu wa pili walipokuja wale mafundi kujenga, yule aliyekuwa anapiga misumari mwenye mibavu, ndiyo mtoto wake huyu wa pili aliyetao hukumu, huyu apigwe misumari. Ila huyu wa tatu, huyu binti ndiyo wako. Hayo ndiyo mazingira ya watu wenyewe kuhukumu. Kwa hiyo, mtu ana hiari ya kutaka kukaa kwenye mazingira gani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninalotaka kulisema lingine ni la Kadhi, najua muda umwekishwa, lakini nitawahi kidogo. Katika Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Sura ya Tano, tunaitambua Mahakama ya Kadhi kule Zanzibar. Sehemu ya Nne, Ibara ya 114, inasema:-

“Kwa madhumuni ya ufanuzi wa Sura hii ya Katiba hii, ifahamike kwamba masharti yaliyomo katika Sura hii hayazuii kuendelea kuwapo au kuanzishwa, kwa mujibu wa Sheria zinazotumika Zanzibar kwa Mahakama Kuu ya Zanzibar au Mahakama zilizo chini ya Mahakama Kuu za Zanzibar.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, miiongoni mwa Mahakama zilizomo chini ya Mahakama Kuu ya Zanzibar, ni pamoja na Mahakama ya Kadhi. Haiwezekani ndani ya Katiba hii hii ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, upande mmoja wa Jamhuri unabaguliwa kuwa na Mahakama ya Kadhi, lakini upande wa pili, tunaona jambo hili ni kichefuchefu, linahatarisha vilevile na Utaifa wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna haja ya kuwa na hofu na sheria hii, imeelezwa vizuri na Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, jambo ambalo halimhusu Muislam, haliingizwi katika Mahakama hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika *Suratil-bakara*, Aya ya Kwanza na mimi nitaisema kwa Kiswahili leo, tunaambiwa kwamba:-

“Hiki ni kitabu kisicho na shaka ndani yake kwa wale wenyewe kuamini.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mahakama ya Kadhi ni kwa ajili ya sisi tunaoamini. Watu wanasema mkigombana, si mwende tu Mahakamani mkaachane? Ndoa katika Uislam ni Ibada siyo suala la kufunga *nikahi* na kuandika talaka basi, hapana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, katika halali ambazo Mwenyezi Mungu anazichukia kwa mujibu wa *Quraan*, ni talaka. Ndiyo maana hata ukitoa talaka, yule mama ukae naye mle mle ndani mpaka eda yake iishie na akiwa anatoka kuoga bahati mbaya ukimgusa bega, umerejea, Mungu haitaki talaka hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kazi ya Kadhi hapa siyo kwenda kutenganisha watu, kazi ya Kadhi ni kwenda kuitafasiri *Quraan* juu ya faida ya mume na mke kuendelea kuishi mpaka siku wanaachana kwenda kaburini. Haya yanawezekana kufanywa na Kadhi, siyo kila Muislam tu anaweza kuwa Kadhi. Mimi siwezi kuwa Kadhi sijui mambo hayo na humu ndani nafikiri nusu au robo tatu ya Waislam, hatuwezi kuwa Makadhi kwa sababu hatujui.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale Masheikh mnaowaona, kila mtu na taaluma yake, kuna wanaojua mambo ya Sheria tu. Sasa mnahofu ya nini? Tutagombana, mbona Zanzibar hawagombani, mbona Kenya hawagombani!

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waislam sisi tuna *tolerance* ya ajabu siyo kwa kutaka kwa kulazimishwa na Mungu, ndiyo, Mungu alimwambia Mtume na sisi ndiyo tunafuata kwamba usigombane na wasioamini kwa sababu wao wana Mungu wao na dini yao na wewe una dini yako na Mungu wako “*Suratil-kaafiruna*”. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hata Waislam waliponyanyaswa na ndugu zao Makka, mara ya kwanza, walikimbilia kwa Mfalme Najafu wa Absinia, Mfalme Najafu alikuwa Mkristo! Ugomvi wa Waislam na Wakristo unatoka wapi mpaka mnakuwa na hofu, Taifa litayumba, hakuna matatizo mnakuwa na hofu tu, ila mkiwanyima haki hii, watu watanung’unika ndani kwa ndani mwisho wake wakiamua kupumua, wakipata *oxygen*, hapo tutaanza kuwa na matatizo ambayo hayana sababu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kusema haya tu, naomba niikumbushe tena Serikali, tafadhalini, mtatoho maneno ambayo hayamo kwenye Kiswahili, wafanyabiashara ndogo ndogo wapo hakuna sababu ya kutumia kabilia la watu liwe ndiyo mbadala ya wafanyabiashara ndogo. Tumieni neno la wafanyabiashara ndogo ndogo, kila kitu mnatoho tu, Wamachinga, oooh, ni *Marching Guys*, mbona Wanajeshi hamuwaiti Wamachinga na wale ndiyo wana-march kila siku kwenye paredi na kila kitu. Jamani, nilisema ningete Hoja Binafsi juu ya suala hili. Nimemaliza, ninakushukuruni sana, ahsanteni. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Emmanuel Luhahula ili atumalizie mjadala.

MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi, inawezekana ikawa nafasi ya mwisho kwa siku ya leo ili niweze kuchangia katika hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa sababu ametupa uzima na ndiyo maana tupo katika siku ya leo na katika Bunge lako Tukufu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo, nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Jaji Mkuu na watendaji wote, kwa ujumla katika Wizara kwa kazi wanazozifanya. Kazi zao ni ngumu, inahitaji hekima, lakini hata namna ambavyo Mheshimiwa Waziri ameweza kuwasilisha hotuba yake, ninaamini Mungu atambariki na hakika mambo yake yatafanikiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongozi hizo, niende kwenye suala la mauaji ya Maalbino na suala la mauaji ya vikongwe katika maeneo mbalimbali hususan Kanda ya Ziwa na sehemu zingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tumekuwa na tatizo kubwa sana katika nchi yetu ambalo ni tatizo la mauaji ya Maalbino na limekuwa ni ajenda katika nchi hii. Pia mauaji ya vikongwe hasa katika Kanda ya Ziwa ni jambo ambalo limeshamiri sana. Ninachotaka kuomba na kuishauri Serikali, ninaamini wanaoshawishi watu kwenda kuua Maalbino ni baadhi ya Waganga wa Jadi ambao wanawadanganya kwa ajili ya kupata utajiri. Ninaamini tukiwatumia Waganga hao wa Jadi kwa umoja wao, kupitia vyama vyao inawezekana kabisa tatizo hili litafika hatua tulimalize.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini Serikali ina uwezo mkubwa, Serikali ina uwezo kuanzia ngazi ya kijiji, tutambue, tutumie vyama vyao, tuvipe mamlaka katika Wilaya, ikiwezekana kuwe na Sheria inayowalinda na kuwajua na hao Waganga wa Jadi ndiyo watakaoweza kutusaidia. Kwa kweli sasa hivi wanadamu tumegeuka kuwa kama wanyama, hali siyo nzuri, wanakatilia mbali uhai wa mwanadamu wakati ambaye ana uwezo wa kutoa uhai wa binadamu ni Mwenyezi Mungu kwa ruksa yake, lakini leo binadamu wamefikia pale!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, mimi ninalo tatizo katika Wilaya yangu, juzi juzi tu ndani ya wiki hiki, mama mmoja na mume wake wameuawa kikatili kweli katika Kata moja ya Ikanguigazi. Kwanza, niwape pole wananchi wa kule pamoja na Mheshimiwa Diwani. Nafikiri mmesikia hata kwenye vyombo vya habari, watoto wamemuua mama yao, wamemuua baba yao, wakachukua sehemu za siri za baba, wakachukua titi moja la mama, ni vitu ambavyo ni vya ajabu vinahitaji kulaaniwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Bunge lako Tukufu, niiombe Serikali na viongozi katika Wilaya wawatafute hawa watu, wawakamate na Mahakama zetu tuombe wanapofikishwa watu hawa, tunahitaji ushahidi gani? Hao wanapofika pale ni lazima wahukumiwe. Lakini tunapata shida kwa sababu wakati mwingine akifika kwa Hakimu bado upelelezi unaendelea, matokeo yake inakuwa haina maana yoyote, kwa kweli sio

suala zuri. Serikali ifanye utaratibu wa lazima wa kuhakikisha kwamba watu hawa wanakamatwa kila inapobainika na tutumie vyama vyao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya suala hilo, niongelee suala la upungufu wa Mahakimu. Najua Wabunge wengi sana wamezungumzia tatizo hili. Tunalo tatizo la upungufu wa Mahakimu hasa Mahakama za Mwanzo. Katika Wilaya ya Bukombe, tunazo Mahakama za Mwanzo nne, Wilaya yenye watu zaidi ya 500,000, lakini tunao Mahakimu watatu wanaozunguka katika eneo lile. Haki kwa mwananchi inaweza kuwa ni ngumu sana kwa sababu Mahakimu hawa kwanza hata vyombo vyaa usafiri hawana. Mara nyingi wakati mwingine tukiwa kule sisi ndio tunawasaidia labda kama unakwenda kituo fulani unaondoka na Hakimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba mtusaidie katika mambo yafuatayo, tuongezewe Mahakama za Mwanzo kwa mfano maeneo makubwa makubwa kama hilo la Bukombe lakini tuongezewe Mahakimu katika Mahakama hizo za Mwanzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru katika hotuba yake Mheshimiwa Waziri amesema wataanza kuwatumbia Wanasheria wa Awali waende katika Mahakama za Mwanzo. Pia kwenye hotuba yake, ameeleza kwamba wameajiri, ni sawa, lakini inafikia hatua wakati mwingine inashangaza tunapoona kwamba wanasema tuna upungufu wa Mahakimu, wapo wanaomaliza Lushoto na mimi ninao mfano, ninaye Mtendaji wangu wa Kata, amemaliza Lushoto lakini mpaka leo kila akituma maombi hapati kazi. Vyeti vyake ni vizuri na mimi nilikuwa nafikiri ni vyema muwachukue watu kama wale, ni rahisi sana kupata *MA-WEO* kwa sababu *Form Six* wapo na *Form Four* watafanya hizo kazi lakini Mahakimu kama wale wamesoma tuwa-*promote* kwa namna hiyo. Tuombe sana mtusaidie na katika Wilaya yangu, naomba mtuongezee Hakimu kwa ajili ya Mahakama hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee suala la Sungusungu. Tuna tatizo la ulinzi katika maeneo yetu na Sungusungu limekuwa ni Jeshi ambalo linatusaidia sana katika kuimrisha ulinzi katika maeneo yetu hasa Kanda ya Ziwa na hasa katika Wilaya ya Bukombe. Lakini wasiwasni wangu nilionao, sina uhakika hawa Sungusungu wanalindwa na Sheria gani. Mara nyingi Sungusungu wanafanyiwa hisani, wakikamatwa wakifanya kazi zao vizuri lakini mjanja mmoja mhalifu akakimbilia kwenda Polisi, wale Sungusungu wanakamatwa, wanageuziwa kibao na wale ndio wanafungwa. Tunaomba Serikali isaidie au pengine ni uelewa wangu, sifahamu, mtusaidie kujua wanalindwa na Sheria gani hawa Sungusungu wanapofanya kazi zao? Kazi yao ni kubwa sana, ni kazi ya kujitolea haina maslahi, maslahi yao ni kuhakikisha usalama kwa wananchi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana mtusaidie kwa sababu tusipofanya hivyo kwa mfano Wilaya yangu ya Bukombe, nafikiri wengi mnajua ni Wilaya ambayo ina wimbi kubwa sana la ujambazi, niwashukuru sana wananchi na viongozi wa Wilaya ya Bukombe imefika hatua tukakubaliana kwa dhati sisi viongozi kwa ushirikiano wetu kwamba tuwaruhusu Sungusungu wafanye kazi zao na sisi tuendelee kuwalinda kwa kuwasimamia. Lazima tuelewane *DC* awe pamoa na Mbunge, Mbunge awe pamoa na Mheshimiwa Hakimu na wanasiasa wengine ili tuwalinde. Sasa tutawalinda mpaka lini?

Inawezekana hawa viongozi waliopo wakatoka katika Wilaya ile, majambazi yanatamba, Maaskari hawatoshi, yakikamatwa hakuna ushahidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sana mtusaidie vinginevyo itafika hatua kwa sababu hawa Sungusungu nao wakichoka wakaona wanakamatwa wananchi watajichukulia Sheria mkononi kitu ambacho tunawashauri wasifanye lakini inaweza ikafika katika hali mbaya wakati wanapoona kabisa kwamba majambazi yanatokea wakiwakamata Sungusungu pengine akienda kwenye mikono ya sheria yanaachiwa kwa sababu hayana ushahidi, wakiona kule nyuma si lazima wafanye vitu vyao. Ni kitu ambacho tunaomba Mheshimiwa muwasaidie Sungusungu, muwalinde, wafanye kazi yao kwa uhakika na wajue kabisa kwamba kazi wanayoifanya Serikali inatambua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, niombe kwa dhati kabisa, niishukuru Serikali lakini nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kulitekeleza ombi langu la muda mrefu katika Wilaya ya Bukombe. Wilaya ya Bukombe tumekuwa tukiomba tupatiwe Hakimu wa Wilaya. Ninampongeza Waziri kwa sababu Hakimu wa Wilaya tulishampata na jengo la Mahakama lipo limeshakarabatiwa, nataka nikuhakikishie na tarehe 30 Julai, Msajili wa Mahakama alikuwa pale Bukombe akiangalia eneo lile. Kwa kweli ni lazima tuipongeze Serikali, watu wa Bukombe wamepata shida sana kutembea kwa muda mrefu kilomita 100 kupeleka kesi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tatizo ambalo lipo na ninaendelea kuomba tuitangaze kwenye Gazeti la Serikali. Nasikia Hakimu yuko Kahama bahati mbaya sijakutana naye lakini anafanya kazi pale Kahama kwa muda. Nilipouliza wanasema kwa sababu haijatangazwa kwenye Gazeti la Serikali, Mheshimiwa Waziri unihakikishie ulisema kabla ya Bunge hili halijaisha kazi hiyo itakuwa imekamilika. Ninaamini utendaji wako wa kazi na ninaomba sana tuhakikishe kwamba tunaitangaza kwenye Gazeti la Serikali ili Hakimu yule arudi pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini bado kuna tatizo la mahabusu katika eneo lile, tunaomba muendelee kushughulikia tatizo lile, jengo lililopo ni jengo la Halmashauri ya Wilaya. Ni la wananchi, wamejitlea wakasema kwa ajili ya usumbufu, tutoe jengo hili kwa ajili ya Hakimu wetu wa Wilaya, wakatoa na nyumba. Kwa hiyo, tunacho kiwanja cha Mahakama tulichokitenga katika Wilaya. Tunaomba Mheshimiwa Waziri, tenga fedha, peleka fedha ukawalipe fidia wananchi wale katika kiwanja chako, peleka fedha ukaanze kujenga jengo lako sasa la Wilaya. Ninaamini katika bajeti ya mwaka 2006/2007, tulipitisha bajeti hapa ya kujenga Mahakama ya Wilaya ya Bukombe nitaomba njue kama hizi fedha ziliendelea kuwepo, zinasimamiwa na lini zitakwenda kukamilisha shughuli hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, napenda kumpongeza tena kwa sababu ya hotuba yake nzuri, hotuba ambayo kwa kweli imeweza kutusaidia lakini niombe sana tuongezewe Hakimu katika Wilaya yetu, Mahakama ya Mwanzo na mwisho tupatiwe gari kwa ajili ya Hakimu wa Wilaya la kufanya shughuli zake. Unajua Jiografia ya Bukombe, ninaamini kama huifahamu pata muda uitembelee uijue,

ninaamini kama utafika pale utaweza kuyafanya kazi vizuri sana tunayoyasema kwa sababu utakuwa unapafahamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaomba niunge sana mkono hoja hii lakini nizidi kusisitiza moja kwamba yako mengi ambayo tunayazungumza yanayoweza kuleta hata mvutano, naomba tumwachie Mwenyezi Mungu ye ye ataamua. Nashukuru sana. (*Makofifi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Luhahula.

Waheshimiwa Wabunge, muda tulionao, haumtoshi mchangiaji anayefuata kuweza kuchangia kwa muda wa robo saa kama ulivyo utaratibu. Kwa maana hiyo, napenda nichukue nafasi hii niwataje wachangiaji watano ambao watachangia kuanzia kesho asubuhi. Kwanza kabisa, atakuwa Mheshimiwa Dr. Harrisson Mwakyembe, atafuatiwa na Mheshimiwa Mohamed Missanga, atafuatiwa na Mheshimiwa Shally Raymond, atafuatiwa na Mheshimiwa Manju Msambya na mtu wa tano atakuwa Mheshimiwa Godfrey Zambi.

Waheshimiwa Wabunge, mpaka hapo nadhani tutakuwa tumemaliza michango ya siku ya leo. Kwa hiyo, niseme kwamba naliahirisha Bunge hili mpaka kesho, siku ya Alhamisi tarehe 14 Agosti, 2008 Saa Tatu Asubuhi.

(*Saa 1.40 usiku Bunge lilahirishwa mpaka siku ya Alhamisi,
Tarehe 14 Agosti, 2008 Saa Tatu Asubuhi*)